Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 24 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza Kikao, nitoe taarifa ya maandalizi ya mazishi ya Marehemu Mheshimiwa Margareth J. Bwana.

Baada ya mawasiliano na familia yake wamepanga mazishi yafanyike kesho jioni, siku ya Jumamosi, Jijini Dar es Salaam ya saa kumi hivi. Mwili wa Marehemu utatoka *mortuary* kwenda nyumbani kwa kaka yake, Mheshimiwa Jaji Bwana, majira ya saa sita hivi kwa ajili ya taratibu za kutoa heshima za mwisho.

Kama utaratibu wetu wa kawaida ulivyo, Bunge litakuwa na wawakilishi rasmi kwa makundi yafuatayo. Kwanza ni Bunge zima ambalo litawakilishwa na Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa kwa sababu yeye alikuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa wakiongozwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

Halafu kutakuwa na mwakilishi kutoka Kamati ya Bunge ya Kudumu aliyokuwa Mjumbe. Kutakuwa na mwakilishi wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM kwa kuwa alikuwa ni Mjumbe wa Kamati hiyo na kutakuwa na uwakilishi mkubwa kidogo wa Waheshimiwa Wabunge wanawake kwa sababu walifanya kikao jana na wakaamua hivyo. Kwa hiyo, tutawapa usafiri wawakilishi rasmi wote hawa leo mchana kwenda Dar es Salaam ili kesho waweze kushiriki katika kutoa heshima za mwisho na baadaye kwenye mazishi. Lakini Waheshimiwa Wabunge wengine wote wanaopenda kwenda watakuwa na nafasi ya kufanya hivyo kwa sababu kesho hatuna Semina tuliyoipanga.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa maelezo. Kikao cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Ishirini kinaanza. Agenda za leo, Katibu endelea *Order Paper.*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 129

## Utaratibu wa Vijiji kuwa Miji Midogo

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika sehemu mbalimbali nchini kumekuwa na maombi kutaka vijiji kuwa miji midogo na mwaka 1996 kwa *GN.176* ilitolewa *Planning Area Order* kwa vijiji vya Kilosa, Gairo, Kimamba, Mikumi, Ruaha, Dumila, Magubike na Kisanga:-

(a) Je, utaratibu wa kuendeleza vijiji kuwa miji midogo ukoje na hatua gani zinastahili kutekelezwa?

(b) Je, *GN.176* ya mwaka 1996 ilitolewa kwa madhumuni gani?

(c) Je, *G.N* hiyo ilikuwa ni moja ya hatua zilizochukuliwa kuzitaka mamlaka husika kuchukua hatua na taratibu za kuvifanya vijiji hivyo kuwa miji midogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kijiji kiweze kupewa hadhi ya kuwa Mji Mdogo, kinatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

(i) Wakazi wasiopungua 10,000.

(ii) Kuwa na huduma kama kituo cha afya, shule ya sekondari, Mahakama, maduka angalau yasiyopungua 20 na soko.

(iii) Kijiji vile vile kiwe Makao Makuu ya Kata au Tarafa.

Hatua zinazostahili kutekelezwa ili kupata hiyo hadhi ni:-

(i) Kijiji husika kuomba kwenye Halmashauri kuwa mji mdogo.

(ii) Halmashauri itajadili ombi na kama kimetimiza sifa.

(iii) Kijiji chenye sifa kitaandaa maelezo ya mipaka na ramani ya kijiji kwa kushirikiana na Halmashauri.

(iv) Halmashauri ya kijiji watabuni nembo itakayotumika kutambulisha Mji mdogo.

(v) Baada ya kukamilisha taratibu zitawasilishwa katika Ofisi yetu kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kijiji kutangazwa kuwa mji mdogo, kijiji hicho kitapoteza sifa ya kuwa kijiji na kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilituma maombi Serikalini ili vijiji vya Kilosa, Kimamba, Mikumi, Ruaha, Dumila, Magubike na Kisanga vitangazwe kuwa miji midogo. Serikali iliyatangaza maeneo hayo kwa kuzingatia Sheria ya Mipango Miji na Vijiji, Sura ya 378(13). Tangazo hilo, *GN.176,* lilitolewa tarehe 9/8/1996.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilitakiwa kuandaa michoro na kutuma Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

(c) Mheshimiwa Spika, tangazo lililotolewa ni hatua mojawapo iliyochukuliwa na Serikali ili kuzitaka Mamlaka husika kuchukua hatua na taratibu za kufanya vijiji hivyo kuwa mamlaka ya miji midogo.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Inavyoonekana kwa vigezo vyote alivyovitaja kijiji cha Gairo kinastahili kuwa Mjini Mdogo sasa inapokuwa Halmashauri inachelewa kuchukua hatua zinazohusika, Wizara haioni kwamba ina jukumu la kuzishinikiza Halmashauri kuchukua hatua zinazostahili haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, si utaratibu mzuri sana kwa upande wa Wizara kuingilia taratibu hizi katika kuanzisha mamlaka mbalimbali hapa nchini lakini Mheshimiwa Waziri wa Nchi amekuwa akifanya hivyo ili kuhakikisha kwamba tunapunguza matatizo ambayo baadaye yanaweza yakatusibu kama hatutachukua hatua hizi haraka. Ndio maana mara ya mwisho alitangaza mamlaka za miji 90 kwa kutumia mamlaka aliyonayo. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Dr. Chiduo kwamba pale itakapobidi basi Waziri atashauriwa ili hatua kama hizo ziweze kuchukuliwa kwa maeneo mbalimbali.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imetangaza na kupandisha hadhi miji midogo mingi kuwa miji na Manispaa na mingine kuwa majiji lakini tatizo kubwa ni miundombinu ya kuifanya miji hiyo ifanane na miji. Je, Serikali imejiandaa vipi kuifanya miji hiyo iliyotangazwa iwe kuwa na miundombinu inayostahili? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, moja ya sababu kubwa ambayo imefanya Waziri wa Nchi achukue hatua hizo, ni kutaka sasa maeneo hayo yaingie katika utaratibu utakaowezesha kuandaa miundombinu ambayo inahitajika sana katika maeneo ya Mijini. Kwa jinsi mfumo ulivyo sasa ukiwa na Halmashauri ya Wilaya ambayo ndani yake fedha ile ile inatumika kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya Mjini na vijijini, mara nyingi inakuwa sio rahisi sana kutoa huduma hizi kwa uwiano unaotakiwa.

Kwa hiyo, lengo la zoezi hili ni kuiwezesha Serikali sasa kuanza kuvitazama vyombo hivi kama vyombo viwili tofauti kila kimojawapo kikiwa na Bajeti yake kutoka Serikalini na vile vile kwa kutumia vyanzo walivyonavyo. Kwa hiyo, tuna hakika pamoja na *programs* nyingine ambazo zinalenga mamlaka za miji mbalimbali, jambo hili sasa pole pole tunaweza kuondokana na miundombinu ambayo ni hafifu.

Na. 130

**Zahanati za Dohomu, Mandi na Duru**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Zahanati za Dohomu, Mandi na Duru zilijengwa kwa nguvu za wananchi na ni muhimu sana Kijiografia kwa kuwa zinahudumia pia shule mpya za Sekondari za Dabil na Dohomu:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka dawa (*kits*) na watumishi katika Zahanati hizo kuanzia Julai, 2005?

(b) Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Zahanati ya Gidas iliyoko km.45 kutoka hospitali za Murara (Babati) na Dareda kuwa kituo cha afya ili iweze kuwahudumia wananchi wa Boay, Gijedaboshka Gidas, Duru na Endagwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damasi P. Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Zahanati za Mandi na Duru licha ya kuwa zimejengwa kwa nguvu za wananchi bado hazijakamilika. Pindi zitakapokamilika, Halmashauri ya Wilaya ya Babati itaziweka katika mpango wa Halmashauri ya Wilaya wa kuzipatia Zahanati hizo watumishi na madawa. Zahanati ya Dohomu inamilikiwa na Kanisa Katoliki na iko chini ya hospitali ya Dareda. Zahanati hiyo tayari inao watumishi wanaolipwa mishahara na Kanisa Katoliki. Aidha, Zahanati hupatiwa dawa na Kanisa hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kanisa Katoliki bado halijaomba Serikali au Halmashauri ya Wilaya ya Babati misaada anayozungumzia Mheshimiwa Damas P.

Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi. Ingefanyika hivyo, tunaamini Halmashauri au Serikali ingekaa chini na kutazama nini ifanye.

(b) Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba Zahanati ya Gidas iko umbali wa km.45 kutoka hospitali ya Murara na hospitali ya Dareda. Mojawapo ya kigezo muhimu cha kuanzisha kituo cha afya ni kuwepo kwa idadi ya watu watakaohudumiwa na kituo hicho wasiopungua 50,000. Lakini kutokana na sensa ya mwaka 2002, vijiji vyote vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge vikichanganywa pamoja, idadi yake inafikia watu 14,650 kwa maana hiyo kiwango chake kiko chini. Hata hivyo, kwa taarifa zilizopo ni kwamba Zahanati ya Gidas kwa upande mwingine ina idadi ndogo sana ya vyumba, hakuna chumba hata kimoja kinachofaa kufanywa wodi na eneo lililopo la Zahanati ya Gidas ni dogo kiasi kwamba haliwezi kuruhusu upanuzi wa aina yoyote kufanyika. Hivyo naishauri Halmashauri ya Babati kwanza iwashawishi wananchi wa eneo hilo waone umuhimu wa kuongeza eneo ili liweze kuwasaidia kupata kituo cha afya. Aidha, Halmashauri inaweza vile vile ikatafuta eneo lingine kama inaona hapana budi ili kuwezesha kituo cha afya kiweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali itakuwa radhi pamoja na mazingira hayo ya kutokuwa na idadi kubwa ya watu lakini kwa sababu za kijiografia zilizopo pale, inaweza kabisa ikafikiria kuwapa kibali cha kuweza kujenga kituo cha afya.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Ni kweli kwamba Zahanati ya Dohomu ilijengwa kwa nguvu za wananchi lakini kwa msaada wa mfadhili ambaye ametokea upande wa Kanisa lakini kwa ujumla ni Zahanati ya Serikali ya kijiji. Kwa hiyo, sio kweli kwamba Zahanati ile inamilikiwa na Kanisa Katoliki na kwamba haijatoa kibali. Mimi binafsi nimepeleka suala hilo Wizarani na ni mwaka wa tatu nafuatilia suala hilo Wizara ya Afya. Je, kwa kauli hii ambayo naitoa sasa hivi kwamba ni Zahanati ya kijiji iliyopata msaada kutoka Kanisani, Serikali iko tayari kuchukua hatua na ikazingatiwa kwamba Zahanati yoyote inaweza kupata huduma ambazo zimetoka Serikalini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi zake za kusaidia wananchi hasa katika sekta hii ya afya na naomba nimhakikishie tu kwamba siku zote ni kujitahidi tusikate tamaa. Kwa hiyo, kama ulijaribu pengine hakupata maelezo yoyote, mimi naomba tusaidiane tena kufufua wazo hilo upya, tujaribu tena kuzungumzia na Wizara ya Afya ili tuone namna tunavyoweza kusaidiana na wananchi wa eneo hilo kuona kama kituo hicho kinaweza kupata msaada kutoka Serikalini.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu lake la msingi, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba atakuwa tayari kupeleka *kit* na Madaktari katika sehemu ambazo wananchi wameshirikiana na Serikali kujenga kwa mfano Zahanati na kwa kuwa sehemu kama Isagawa na Udekwa kule Kilolo wananchi walishirikiana na *TASAF* kujenga Zahanati na kwa kuwa sasa hivi Zahanati hizo zimeshakamilika. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kupeleka *kit* na Madaktari ili wananchi wasivunjike moyo kushirikiana na Serikali kujenga Zahanati hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri wakati Mheshimiwa Mama Anna Abdallah anaingia hapa kaninong'oneza jambo zuri tu. Kwa hiyo, ili mradi mambo yako yako pale kwenye Ofisi ya mama, nafikiri mambo yatakwenda vizuri, tutaangalia tuone namna ya kulisukuma sukuma ili uweze kupata hayo mambo mawili katika muda mfupi kadri inavyowezekana.

Na. 131

**Kero za Muungano**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (K.n.y. MHE. ALI AMEIR MOHAMMED** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja kati ya ahadi za Rais wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipoanza Awamu ya Tatu ya uongozi wake ilikuwa ni kushirikiana na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kutatua kero za Muungano:-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge kuwa ni kero zipi kubwa zilizopatiwa ufumbuzi katika utekelezaji wa ahadi za Serikali?

(b) Je, ni kero gani kubwa ambazo Serikali inafikiri kuwa hazijapatiwa ufumbuzi na ni kwa nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya juhudi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa vikwazo vinavyojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano vinapatiwa ufumbuzi.

Kwa lengo la kuhakikisha kuwa vikwazo vinavyojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano vinapatiwa ufumbuzi, vikao mbalimbali vya ushirikiano kisekta vinavyohusisha wataalamu wa Serikali zote mbili, vimeendelea kufanyika. Masuala muhimu yanayohusu sera na kubadilishana mawazo, uzoefu na utaalamu katika sekta mbalimbali yanajadiliwa kwa pamoja.

Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Kamati maalum chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu Mwandamizi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Bwana Raphael Mollel, ili kushughulikia masuala mbalimbali yakiwemo ya uchimbaji mafuta Pemba na uvuvi kwenye Ukanda wa Bahari Kuu. Wajumbe walioteuliwa katika Kamati hiyo ni pamoja na Wanasheria Wakuu wa Serikali zote mbili, Makatibu Wakuu wa Sekta za Madini na Nishati, Maliasili na Uvuvi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Kiongozi pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara za Fedha wa Serikali zote mbili. Aidha, kulikuwa na waalikwa ambao ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Mapendekezo ya Kamati hiyo yamewasilishwa Serikalini na yanafanyiwa kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, si jambo jepesi kuorodhesha kero ndogo au kubwa. Jambo la msingi ni juhudi mbalimbali za Serikali za kutatua matatizo au kero katika Muungano wetu kupitia utaratibu wa vikao kwa lengo la kuudumisha Muungano wetu kama tusemavyo: “Muungano Daima”.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa jambo kubwa linalosababisha matatizo au migogoro katika Muungano ni umasikini na taratibu ambazo sio nzuri za utekelezaji wa kero hizo. Je, si vema kukaundwa Wizara Maalum ambayo itashughulikia shughuli za Muungano tu kuliko kuunda vikamati ambavyo havileti ufanisi katika kuondoa kero za Muungano? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba suala la umasikini uliokithiri linachangia sana katika mambo haya ambayo tunayaita kero za Muungano lakini nina hakika sote sasa tunaanza kuzoea kutamka neno MKUKUTA (Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupambana na Umaskini).Kama ni Wizara mimi sijui kama unaweza kusema kuna Wizara sijui kama ni kubwa au muhimu zaidi kuliko Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, mimi nadhani tatizo sio Wizara lakini tatizo ni tutavyotekeleza suala zima la MKUKUTA. (*Makofi*)

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Moja katika kero ambayo inaikumba Zanzibar ni mamlaka na madaraka ya Rais wa Zanzibar katika Serikali ya Muungano, Mheshimiwa Waziri anasemaje katika suala hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA:** Mheshimiwa Spika, mamlaka na madaraka ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yameainishwa barabara na kwa yakini katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Katiba ya Zanzibar.

Kwa upande wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sote hapa tumekula kiapo cha kuilinda, kuihifadhi na kuitetea. Kwa kufanya hivyo, tunalinda, tunahifadhi na kutetea mamlaka na madaraka ya Rais ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Na. 132

**Mawasiliano ya Simu – Wilayani Same**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika milima ya Wilaya ya Same Mkoani Kilimanjaro ipo miundombinu duni ya barabara na hakuna mawasiliano ya simu; na kwa kuwa, wananchi wengi Wilayani humo ambao ni asilimia 75 wanaishi milimani; na kwa kuwa, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inasema bayana kuwa Shirika la Simu la *TTCL* halina mpango wa kupeleka huduma ya simu vijijini kwa sababu ni kinyume na matarajio yao ya biashara; na kwa kuwa, hivi sasa huduma ya simu za *Celtel* imepelekwa maeneo mengi vijijini:-

(a) Je, Serikali kwa kulifahamu hilo ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano ya simu za Celtel katika milima ya Same Kata za Mhezi, Videe, Mshewa, Msindo, Kisiwani, Dido, Vumari, Ruvu – Muungano, Gonja Bombo, Mtii, Mamba Bwambo, Mpinyi, Ivuga, Kirangare, Vunta na Mwala?

(b) Je, Serikali inafahamu mazingira na jiografia ya Milima ya Same na athari za kijamii, kiuchumi na kisiasa zinazowakabili wananchi wanaoishi milimani Same kwa kukosa mawasiliano ya simu na ni lini Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi atatembelea maeneo hayo na kujionea mwenyewe mazingira hayo?

(c) Je, ni kikwazo gani kinachozuia huduma za simu kwa wananchi wa Milima ya Same lakini sehemu zingine wanapata?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John E. Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kampuni ya *Celtel* ina kila nia ya kuhakikisha kuwa wananchi waishio kwenye Milima ya Same wanapata huduma ya simu za mkononi. Wananchi wa Same Mjini wanapata huduma ya simu za mkononi ya *Celtel.* Hivi sasa *Celtel* iko katika hatua za mwisho za kupeleka mawasiliano katika Kata za Ndungu na Gonja. Ni matarajio yetu kuwa vijiji vilivyo katikati ya maeneo hayo navyo vitapata huduma za *Celtel* pale zitakapoanza kutolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu mazingira na jiografia ya Milima ya Same na athari za kijamii, kiuchumi na kisiasa zinazowakabili wananchi wanaoishi Milimani Same za kukosa mawasiliano ya simu. Mheshimiwa Waziri ameshawahi kutembelea maeneo hayo ya Same.

(c) Mheshimiwa Spika, kikwazo kikubwa kinachoweza kuzuia huduma za simu kwa wananchi wa Milima ya Same inawezekana ikawa ni sababu za kijiografia.

Utaalam uliokuwa unatumiwa na Kampuni ya Simu ni ule wa *Wireless Lock Loop (WLL )* ambao ulishindwa kuleta ufanisi wa kutosha katika maeneo yenye milima na miti mirefu. Maeneo yaliyo nyuma ya milima hiyo au miti mirefu, yalizuiliwa kupata mawasiliano kutoka kwenye minara ambayo iko upande wa pili.

Hili lilisababisha kitu ambacho kitaalam kinaitwa *Black Spot*. Hali hii inaweza kuyakumba pia maeneo ya Milima ya Same. Hata hivyo, wataalam wanaendelea kutafuta njia mbadala ya kutatua tatizo hili.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika …

*(Hapa Wabunge wote walishangilia kwa kupiga makofi wakati Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, akiingia Bungeni)*

**SPIKA:** Subiri kidogo Mheshimiwa Singo makofi ya kumkaribisha Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje yatulie. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Singo, sasa unaweza kuuliza swali lako la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alitembelea eneo la kisiwani yapata mwaka mmoja sasa na kuahidi wananchi wale kwamba wangepata mawasiliano ya simu ndani ya miezi mitatu na sasa ni zaidi ya mwaka mmoja umekwisha na wananchi wale bado wana matumaini ya kupata huduma ambayo Mheshimiwa Waziri aliahidi. Je, kumetokea nini?

(b) Kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema kuna kizuizi kinachoitwa *black spot* kinachozuia mawasiliano juu ya Milima ile ya Same. Je, wataalam watachukua muda gani kutatua tatizo hilo la *black spot* ama haliwezi kutatulika?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Singo kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alitembelea maeneo yake kwa wakati huo.

Napenda nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Waziri aliyafikisha maombi ya wananchi wa maeneo hayo kwa makampuni ipasavyo ndio maana sasa hivi wanashughulikia masuala ya Dunga kama nilivyosema na maeneo mengine kufikisha mawasiliano ya simu kwa kujenga minara.

Pili, suala la *black spot* linatokea kama tunatumia utaalamu wa *Wireless Lock Loop (WLL)* katika maeneo ambayo yana miti mirefu yanaziba mawasiliano ya simu lakini njia mbadala zipo na ndio hizo za kuweka minara mirefu kwenye milima ambayo itaweza kufikisha mawasiliano ya simu katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Singo kwa juhudi zake za kufuatilia matatizo yanayowakera wananchi wake wa Same na namwomba asikate tamaa japo muda ni mfupi lakini wananchi wameshaona juhudi zako Mheshimiwa Singo ulizozichukua.

Na. 133

**Mawasiliano ya Simu – Liliondo**

**MHE. ELISA O. MOLLEL (K.n.y. MHE. MATHEW TAKI OLE-TIMAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro – Loliondo ni miongoni mwa Makao Makuu ya Wilaya hapa nchini ambayo hayana mawasiliano ya simu za mkononi:-

Je, ni lini Makao Makuu ya Wilaya hiyo ya Ngorongoro (Loliondo) yatapatiwa huduma hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Taki Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini ya soko pamoja na ukaguzi wa maeneo yanayoweza kufikiwa na mawasiliano kwa ajili ya kuipatia huduma za simu za *Celtel* Ngorongoro imekamilika.

Hata hiyo, kutokana na sababu zisizoweza kuzuilika ambazo ziko nje ya uwezo wa Kampuni ya *Celtel* kwa hivi sasa kidogo itakuwa vigumu kutamka ni lini *Celtel* itafikisha huduma za simu Ngorongoro.

Lakini kwa upande mwingine, Kampuni ya simu ya *Mobitel* imeshakamilisha utekelezaji wa mikakati wa kufikisha huduma za simu ngazi ya Mkoa. Hatua inayofuata ni kufikisha huduma katika ngazi ya Wilaya.

Kwa hiyo, hivi sasa katika ngazi hiyo ya Mikoa hususan ya Kaskazini, Kampuni imeelekeza nguvu zake katika Mikoa ya Arusha na Manyara.

Kwa Mkoa wa Manyara, Kampuni imelenga kufikisha huduma hizo katika Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro ndani ya kipindi cha miezi sita (6) kuanzia sasa.

Kwa upande wa Kampuni ya simu ya *Vodacom* ni kwamba tathmini ya soko imekwishafanyika na mpango wa utekelezaji *Action Plan* wa kufikisha huduma hizo Wilaya ya Ngorongoro unaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Ngorongoro wavute subira kwani juhudi zinafanywa na makampuni husika kuhakikisha kwamba wanafikisha huduma ya mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Loliondo.

Na. 134

**Utafiti wa Mafuta**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:

Kwa kuwa, zipo tafiti/chunguzi nyingi zilizofanyika na zinazoendelea kufanyika kuhusu upatikanaji wa mafuta hapa nchini:-

(a) Je, kuna matumaini yoyote hadi sasa kwa nchi yetu kupata mafuta?

(b) Kwa kuwa, ni kwa mara ya kwanza nchi yetu kutumia gesi kutoka Songosongo na kupata nishati ya kuendeshea mitambo. Je, kuna tahadhari gani zimechukuliwa

kuwalinda na kuwawekea bima wananchi wanaoishi au kufanya kazi kwenye maeneo ambayo gesi hiyo hupita au kutumika endapo kwa bahati mbaya litatokea janga lolote kutokana na gesi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa zipo tafiti / chunguzi nyingi zimefanyika na zinaendelea kufannyika kuhusu upatikanaji wa mafuta hapa nchini.

Mheshimia Spika, kumekuwa na juhudi kubwa za utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali yenye kuonyesha viashiria vya kuwepo kwa miamba tabaka. Maeneo hayo ni pamoja na ya mwambao wa ukanda wa Bahari ya Hindi, vilindi vya Bahari na maeneo ya Bonde la ufa.

Shughuli za utafutaji mafuta na gesi zinatekelezwa chini ya sheria ya Muungano ya utafutaji na Uzalishaji mafuta ya mwaka 1980.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu wa mkataba wa uzalishaji yaani *Production Sharing Agreement (PSA),* Serikali huingia mikataba na kampuni zinazoonyesha nia ya kuja kutafuta mafuta nchini, ambapo kampuni husika hugharamia shughuli zote za utafuta mafuta. Gharama za utafutaji zitarejeshwa kwa muwekezaji kutoka katika mgao wa mafuta yanayozalishwa yaani (*cost oil*) endapo mafuta yatagundulika. Endapo mafuta hayatagundulika gharama hizo hazitarejeshwa.

Aidha, endapo mafuta yatagunduliwa, mafuta ya faida (*profit oil*) hugawanywa au yatagawanywa baina ya Serikali na kampuni husika. Hadi sasa Serikali ina mikataba ya utafutaji na uzalishaji mafuta na kampuni kama *Petrobras* ya (vilindi vya bahari mashariki ya Mafia – Kitalu Na. 5) *Maurel and Prom* (Bigwa - Mafia), Ndovu (Nyumi) *Pan Africa* Mashariki ya Songosongo(*East of Songosongo*) na *Antrim* (Pemba and Zanzibar).

Kampuni nyingine ambazo zimeonyesha nia ya kuja kuwekeza katika utafutaji mafuta hususan maeneo ya vilindi vya bahari ni *Shell, Stat oil, Norskhydro* na *Texaco*.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu bado haijagundua mafuta ingawa kuna dalili za kuwepo mafuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi ya Songosongo, ajali au janga linaloweza kutokea kuhusiana na gesi asilia ni pamoja mlipuko na moto katika visima vya gesi asilia, mitambo ya kusafishia gesi au mabomba yatumikayo kuisafirisha gesi hiyo. Mheshimiwa Spika, kuhusu tahadhari ambazo zimechukuliwa:

Kwanza, Bomba la gesi ya Songosongo limepitishwa katika njia yake (*way leave*) endapo wananchi walioko katika njia hiyo wamefidiwa na wameondolewa.

Pili, Wananchi hawaruhusiwi kulima karibu na bomba.

Tatu, Wananchi wanatahadharishwa kuwa ni hatari kugongagonga bomba la gesi kwa panga au kitu chochote.

Nne, Sasa hivi kuna kampeni / elimu kwa umma ya namna ya kutambua harufu ya gesi ili inaposikika harufu hiyo taarifa zitolewe haraka kwa kampuni ya *Songas*.

Tano, Wananchi wanapoona moto wasikimbilie uliko moto bali waukimbie moto huo wakimbe mbali.

Sita, Wananchi wasijenge tabia ya kulizoea bomba la gesi, walione kuwa ni hatari hata kulisogelea.

Saba, Unene wa bomba la gesi Kusini mwa Dar es Salaam ni mm 6.4 lakini unene huu umeongezwa kufikia mm 11.3 katika Jiji la Dar es Salaam katika kuhakikisha kwamba kuna usalama.

Nane, Kuna bima ya wadau wote ya karibuni Dola za Marekani milioni 25.

Tisa, Kuna waendeshaji waliofuzu mafunzo rasmi ya kusimamia visima na mitambo ya kusafishia na kusafirishia gesi saa 24 kwa siku.

Kumi, Kuna ukaguzi wa mara kwa mara katika njia ya kusafirishia gesi. Mwisho, Kuna walinzi katika vituo vyote vya vali (*valves*) vilivyopo katika njia ya bomba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zote hizo kinga kubwa zaidi ni uangalifu. Napenda kuchukua nafasi hii kuwatahadharisha wananchi wote waishio karibu na bomba la gesi ya Songosongo kuwa waangalifu na kutofanya shughuli zozote kwenye mkuza wa bomba la gesi ili kulinda usalama wao na usalama wa bomba. Aidha wananchi wanatakiwa wawe macho na watu wowote wanaoweza kufanya hujuma katika miundo mbinu hii muhimu kwa Taifa letu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nashukuru pia kwa majibu mazuri sana ya Naibu Waziri kama kawaida yake,

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme ni ghali na Serikali imeshindwa kabisa kupunguza umeme hasa kwa watu wanaoutumia majumbani. Je, Serikali inachukua hatua

gani kubadilisha gesi ya Songosongo ili iweze kutumika majumbani kwa bei nafuu?(*Makofi*)

Pili, ziko tetesi kwamba kuna dalili nzito au nzuri zaidi za kupata mafuta katika bahari yetu kuu hasa kwa upande wa Pemba lakini pia ziko tetesi kwamba kuna hitilafu katika makubaliano ya Serikali zetu mbili. Je, Serikali inatamka nini katika hili ili wananchi wajue?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekiffu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu bei ya umeme kuwa ghali ni kweli kwamba bei ya umeme ni ghali lakini kama ambavyo tumesema mara nyingi hapa Bungeni suala hili linatokana kwa upande mmoja na mfumo wa uzalishaji umeme ulivyo hivi sasa kuwa ni ghali na ndiyo maana Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuweka aina ya mfumo wa uzalishaji wa umeme ambao hatimaye utatuletea unafuu katika bei ya umeme na mfano bora ni huu utumiaji wa gesi ya Songosongo.

Uwekezaji katika gesi na utumiaji wa gesi ya Songosongo ili kuhakikisha kwamba mfumo wa uzalishaji wa umeme hautegemei uzalishaji wa umeme unatumia mafuta tu ambao ni ghali au hautulazimishi wakati wa ukame ambapo hakuna maji kununua umeme ambao unatokana na mafuta. *(Makofi)*

Hii ni hatua moja lakini zipo hatua nyingine zinazochukuliwa na hatimaye naamini tutafika hapo.

Pili napenda niunganishe na hili kwa kusema kwamba upo mpango wa kuhakikisha hapo baadaye gesi hii ya Songosongo inatumika majumbani na kwa kuwa tuko katika hatua za awali ningemwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri wakati mpango huu utakapokamilika basi tunaweza kutoa taarifa za kina zaidi.

Lakini kwa hivi sasa gesi hii pia inatumika katika baadhi ya viwanda vyetu katika kutuletea unafuu na kwa sababu viwanda hivi vinavyotumia gesi na wao gharama zao za uzalishaji zinapungua kwa upande mwingine pia zitakuwa zinanufaisha wananchi kwa bidhaa watakazokuwa wanazinunua kutoka kwenye viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta na matatizo ambayo aliyataja baina ya pande mbili za Muungano. Asubuhi hii Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais alikuwa akijibu swali juu ya kero za Muungano na katika majibu yake alizungumzia juu ya kamati iliyoundwa ambayo inahusisha pande mbili za muungano na katika wajumbe waliotajwa katika Kamati ile ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na hii ni kuonyesha kwamba hata masuala ya Nishati na Madini au masuala ya

Nishati ambayo ni pamoja na suala hili ambalo amelizungumza limo katika majadiliano baina ya pande mbili za Muungano.

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba Taarifa hii sasa imewasilishwa Serikalini na inafanyiwa kazi basi ningemwomba Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu tuwe na subira tusubiri Serikali ifanyie kazi taarifa hii.

**MHE. ABDULKARIM E. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama alivyosema kwamba upo utafiti unaofanyika katika maeneo ya visiwa vya Mafia kwa maana ya Nyuni, Ukuza na maeneo ya Kusini na mwezi mmoja uliopita na nusu.

Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Mafia na bahati tulimpeleka kwenye moja ya visima viwili ambavyo vimechimbwa mwaka 1954/1956 na Kampuni ya *BP* na pale panasemekana kwamba mafuta yapo au gesi na aliahidi wakati tulipokuwa pale kwamba atapeleka wataalama.
*(Makofi)*

Je, anaweza kuwaeleza au kuwaambia wataalam wake hivi sasa waende wakafanye utafiti au kuvifungua vile visima vijulikane kama kuna mafuta au gesi kwa ajili ya maendeleo ya Kisiwa cha Mafia na Tanzania kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba nilitembelea Mafia kama alivyosema na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Mafia kwa ushirikiano walionipa wakati nilipokuwa katika Kisiwa hicho.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kweli kwamba nilikwenda kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge na Viongozi wa Mafia walinifahamisha kwamba palikuwa na utafiti uliofanyika miaka ya nyuma wakati wa ukoloni na sehemu ambayo kuna visima ambavyo vimezibwa na baada ya pale niliwafahamisha kwamba ningelishughulikia baada ya kufika Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niliambie Bunge lako Tukufu na kuwaambia wananchi wa Mafia kwamba baada ya kuwasiliana na wataalam wetu wa *TPDC*, kwanza nilifahamishwa kwamba wao wanalifahamu jambo hili na kwamba tathmini yao ya awali ilionyesha kwamba pale palikuwa hapana mafuta lakini kwa sababu kuna wasiwasi mkubwa kwamba inawezekana palikuwa na mafuta na wakoloni wale wamefunga vile visima na kadhalika.

*TPDC* wamekubali kuendelea na utafiti wa eneo lile na kwamba watalitangaza eneo lile kwa watu wanaotaka kufanya utafiti na wao wenyewe watasimamia zoezi hilo. (*Makofi*)

Na. 135

**Mpaka wa Eneo la *Geita Gold Mine Ltd.***

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:

Kwa kuwa, baada ya mgodi wa dhahabu wa *Geita Goldmine Ltd*. Kuwekewa mawe ya mpaka wapo baadhi ya wananchi walibaki ndani ya eneo la mgodi kama vile Magema, Maketani, Nyamalembo, Nyakabale, Katoma na Nyamatagata:-

(a) Je, wananchi walioko ndani ya eneo hilo watafidiwa lini ili waweze kutoka katika eneo hilo?

(b) Je, kuna sheria gani inayomruhusu mtoa fidia kujipangia kiwango bila kumshirikisha mwananchi anayekutwa ndani ya eneo lake?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya wananchi na hata viwanda vya kuchambua pamba na viwanda vya mbao ambavyo vimo ndani ya eneo la leseni ya mgodi wa Geita. Aidha wakazi hao wamekuwa wanaishi kwa amani na utulivu bila ya bughudha yoyote kutoka mgodini. Endapo mgodi utakusudia kutumia ardhi inayotumiwa na wakazi hao au viwanda hivyo ndipo utakapolazimika kwanza kuwapa taarifa na muda ili kujitayarisha kuhama pamoja na kulipa fidia.

Kwa sasa mgodi haukusudii kutumia maeneo haya na hivyo wataendelea kuishi bila kubughudhiwa. Hakuna utaratibu unaoruhusu mtoa fidia kujipangia kiwango au kiwango cha fidia bila kumshirikisha mwananchi anayekutwa ndani ya eneo lake. Mtoa fidia na mlipwaji wote wanafuata sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu juu ya malipo ya fidia.

Fidia hulipwa kwa kuzingatia mwongozo wa Serikali wa ulipaji fidia kama ulivyoainishwa kwenye Sheria ya Uthamini na Fidia ya mwaka 2001 yaani *The Land (Assessment of the Value for Compensation) Regulation, 2001*. Fidia hiyo huhusisha ardhi, mazao na mali nyingine zisizohamishika. Utaratibu uliopo wa kuhakiki mali unawahusisha mwenye kufidiwa, mtoa fidia, wajumbe wa nyumba kumi kumi pale inapohusika, wenyeviti wa vjijiji, wawakilishi wa Halmashauri ya Wilaya, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mtathmini wa Serikali. Wahusika wote hawa ni lazima waweo katika kuhakiki mali ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mgodi wa Geita ni wa wazi *Open Cast* na wananchi wanaokaa maeneo ya pale wanapata adha ya kuwa na mavumbi pamoja na mlipuko wa ajabu ajabu kiasi ambacho wananchi wengi wanapata magonjwa ya moyo na mimba kuweza kutoka. Je, Serikali inasemaje kuhusu hao wananchi kuwafidia ili waondoke katika maeneo hayo? Pili, kwa kuwa Geita ni eneo lenye madini na sasa hivi kuna Kampuni moja ambayo imeshaingia pale ambayo iko Mgusi inaitwa *Shanta Mine* inaongozwa na Ndugu Emmanuel Kitike baada ya kufika pale imewalazimisha wananchi kuweka uzio ndani ya eneo la wananchi. Je, Serikali inasemaje kuhusu Kampuni hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Naoma kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mabina kama ifuatavyo:-

Uchimbaji wa madini ambao si wa chini ya ardhi yaani *Open Cast* kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni uchimbaji ambao unaambatana na hatari mbalimbali ikiwemo mawe yanayoweza kurushwa wakati wa milipuko na kadhalika na kadhalika. Ni kwa sababu hiyo basi Serikali wakati wowote imekuwa ikiwataka wananchi ambao wanakaa katika maeneo ya karibu ya maeneo hayo kuchukua tahadhari au kuondoka katika maeneo hayo pale wanapopata fidia.

Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amezungumzia suala ambalo linawahusu wananchi wa eneo ambalo wanapata adha hii, na kwa kuwa Serikali hii inajali sana maslahi ya wananchi wake. Mheshimiwa Mbunge mimi nadhani hili ni jambo ambalo baada ya Bunge hili tukutane ili tuweze kulitafutia ufumbuzi unaofaa na wa kudumu.

La pili, kuhusu Kampuni ya Shanta ambayo kwa mujibu wa taarifa za Mheshimiwa Mbunge imewalazimisha au imewatilia uzia wananchi. Mimi taarifa hizi ndiyo nazipata sasa na kwa maana hiyo ningependa nipate muda wa kuifanyia kazi lakini ningemwomba nipate muda wa kuifanyia kazi lakini ningemwomba Mheshimiwa Mbunge tuonane baada ya Bunge ili Serikali iweze kulifanyia kazi jambo hili.(*Makofi*)

**MHE. MUTTAMWEGA G. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo Geita eneo lote la Mwibara ambalo lina madini tayari wameshapewa makampuni ya kigeni ambayo ni wazungu, na kwa kuwa hivi sasa wananchi wa Mwibara wanauwezo wa kupata vifaa vya kisasa kama ilivyo makampuni hayo.

Je, Serikali iko tayari kurudisha eneo hilo kwa wananchi wa Mwibara waweze kuchimba wao ili kusaidia uchumi wao kuendelea badala ya kuwa chini ya hawa wazungu na kuwa vibarua kwa wazungu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgaywa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeweka sera madhubuti sana inayohusu uwekezaji kwa ujumla na uwekezaji katika sekta ya madini. Sera hii haibagui aina ya wawekezaji ili mradi wanafuata taratibu na sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hawa wawekezaji ambao anawazungumzia Mheshimiwa Mbunge watakuwa wamepata eneo hilo kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu zetu. Hii si nchi ambayo leo unawatangazia wawekezaji waje kuwekeza kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo halafu kesho unakurupuka tu na kuanza kuwafukuza hapana.

Ili mradi wanafuata sheria na ili mradi uwekezaji huu unaruhusu watu wote pamoja na wananchi waliopo hapa, mimi nadhani tuendelee na kuwakaribisha wawekezaji kwa kadri tuwezavyo na kuhakikisha kwamba sera yetu ya madini inaendelea kutekelezwa na pale kwenye marekebisho kama ambavyo tumekuwa tukizungumza wakati hadi wakati sasa masuala haya ni masuala ya kuzungumza kama ambavyo hivi karibuni tutakuwa hapa Bungeni na Semina ya kupitia taarifa ya Kamati iliyoundwa juu ya Madini.

Lakini Watanzania hawa hawajafanywa kuwa ni vibarua wa wazungu, sera ya Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake haijawafanya Watanzania wawe ni vibarua wa wazungu. Mwananchi yoyote ambaye anataka kuwekeza anakaribishwa na huo ndiyo msimamo wetu. (*Makofi*)

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa nini Serikali haiwafundishi wananchi wanaokaa katika sehemu za madini kufanya hisa na wazungu wanaokuja kufanya biashara hapo badala ya kuwapa hisa au kufanya *partnership* na wakazi wa sehemu hizo badala ya kuwalipa tu fidia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati najibu hapo awali nilizungumzia juu ya sera yetu ya madini na juu ya Sheria ya Madini ambayo tumeipitisha katika Bunge hili na katika Sheria hii na Sera hii yapo maeneo ambayo wawekezaji wanatakiwa waende wafanye

ubia na Watanzania na wengine katika wawekezaji hawa huuza hata baadhi ya hisa zao kwa wananchi wa Tanzania na tunayo mifano mingi tu katika Sekta hii ya Madini.

Lakini si sera yetu kulazimisha kwamba mwekezaji anayekuja kwa upande ambao anauzungumzia Mheshimiwa Mbunge kwamba lazima awe ameshirikiana na wananchi kwa maana ya kupewa hisa ya aina fulani isipokuwa katika maeneo yale tu kama yalivyoainishwa kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Na. 136

**Barabara ya Mwanangwa – Misasi -Busongo - Salawe**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:

Kwa kuwa, barabara za Wilayani Mwisungwi bado zinahitaji matengenezo ili zipitike kwa nyakati zote:-

(a) Je, barabara ya Mwanangwa – Misasi – Busongo hadi Salawe itakamilika lini hasa katika tuta lililopo kwenye eneo la Mto Mwame palipojengwa daraja jipya?

(b) Je, barabara ya kuunganisha Usagara – Kisesa – kupitia Fela inajengwa na nani, na ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

(c) Je, madaraja ya Mwamagembe kati ya Mwigiligili na Mwawile yatajengwa lini ili kuepusha ajali kama ilivyowahi kutokea?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kupitia wakala wa barabara (*TANROADS*) mkoa wa Mwanza tayari imefanya matengenezo makubwa ya barabara ya Mwanangwa – Misasi hadi Salawe ambapo jumla ya kilomita 38 za barabara hii zimefanyiwa ukarabati (*rehabilitation*) kwa kiwango cha changarawe pamoja na kukamilisha ujenzi wa daraja kubwa la kudumu lenye urefu wa mita 40 kwenye mto Mwame. Hali ya barabara hii kwa sasa ni nzuri.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Usagala – Fela hadi Kisesa hivi sasa inafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa msaada wa fedha za *Europena Union.* Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika karibuni ambapo itafuatiwa na hatua zingine za ujenzi.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005 Wizara yangu kupitia wakala wa barabara *TANROAD* Mkoa wa Mwanza imekamilisha pia

ujenzi wa madaraja Mwamagembe na Mwagiligili pamoja na ujenzi wa tuta la barabara iingiayo kwenye daraja jipya la Mwame.

Aidha Maandalizi ya daraja lingine dogo katika eneo hilo la Mwame unaendelea ili kuruhusu sehemu hiyo yote kupitika.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kabisa nimshukuru yeye Naibu Waziri na Waziri wake kwa ujumla kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya kwenye Jimbo la Msumgwi na ninawaombea kwa Mungu wakashinde ushindi wa kishindo kwenye majimbo yao. (*Makofi*)

Katika jibu ambalo amejibu kwamba Mwanangwa, Salawi ni barabara safi. Je, ana habari kwamba kutokana na malori mazito yanayopeleka vifaa vya ujenzi wa mradi wa maji kwenda Shinyanga yameharibu sana barabara hiyo hasa kutoka Mwanangwa hadi Misasi?

Kwa kuwa wana fungu la kuweza kukarabati barabara, Serikali inasemaje kuwashauri ili waweze kukarabati barabara hiyo ya kutoka Mwanangwa kwenda Misasi?

La pili, katika barabara ya Usagara - Kisesa hadi Fela upembuzi unaendelea na itajengwa kwa kiwango cha lami na ninashukuru sana. Lakini kumekuwa na tatizo kubwa sana baina ya Fela na Bujingwa, tumewahi kupata ajali na Mwalimu wetu akafa kwenye daraja hilo la Fela.

Je, Serikali inaonaje kutengeneza daraja la muda ili angalau wananchi wa Fela na Bujingwa waweze kuwasiliana? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacob Shibiliti kama ifuatavyo:-

Tunajua kwamba kuna tatizo la malori makubwa sana yanapita kwenye barabara hiyo na tumewasiliana na wawekezaji tuone ni kiasi gani tunaweza kushirikiana kuitengeneza upya barabara hiyo na wao wakishiriki.

Madaraja yale katika barabara ya Fela na Majingwa ni pamoja na taarifa niliyoitoa kwamba sasa hivi tunafanya hatua ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami na katika utafiti tunaoufanya upembuzi yakinifu tunaoufanya sasa hivi ni kuona jinsi gani tunaweza ama kuyakwepa madaraja haya ama kuyatengezena kwa kiwango kikubwa

kabisa ili barabara zipitike. Tukisema tujenge madaraja ya muda itakuwa aghali sana barabara hii, naomba wananchi wastahimili tu kwamba tutaijenga barabara hii pamoja na madaraja hayo.

Na. 137

**Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2004/2005 Waziri wa Elimu na Utamaduni alitoa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa kuboresha elimu ya sekondari kwa kufanya shughuli mbalimbali kama ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, maabara na pale inapobidi kujenga hosteli kwa kuchangia bidhaaa za viwandani:-

(a) Je, ni uwiano gani wa ujenzi wa madarasa na majengo mengine ulioandaliwa Kimkoa na Kitaifa?

(b) Je, Mkoa wa Ruvuma umepangiwa kusaidiwa majengo mangapi kwa wastan kwa kila Wilaya?

(c) Je, ni vigezo vipi Serikali itatumia ili kusaidia utoaji wa fedha za vifaa/bidhaa za viwandani kumalizia majengo hayo, na ni nani atakuwa msimamizi mkuu wa mpango huo Ki-wizara na Kijamii?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa MMEM 2004 – 2009 shule ya sekondari ya kawaida (O-*level*) iliyokamilika yenye mikondo 4, uwiano wa majengo unaohitajika ni kama ifuatavyo; vyumba vya madarasa 16, nyumba za Walimu 29, jengo la utawala 1, maktaba 1, maabara 3, ukumbi wa mikutano 1 na matundu ya vyoo 25 yakiwemo matundu 10 kwa wavulana, 12 kwa wasichana na 3 kwa Walimu na Watumishi wengine.

(b)Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma umepangiwa ruzuku ya maendeleo ya Shilingi milioni 856 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi mpya wa madarasa 76 na nyumba za Walimu 36. mgawanyo wa Ruzuku hiyo kiwilaya ni kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Tunduru yenye wanafunzi wa darasa la saba waliokuwepo mwaka 2004 ni 3133, madarasa hakuna, nyumba za walimu 7 na jumla ya ruzuku shilingi milioni 63.

Wilaya ya Mbinga wanafunzi wa darasa la saba mwaka 2004 ni 9596, madarasa 47, nyumba za walimu 12 kwa hiyo jumla ya ruzuku ni shilingi miliioni 437.

Wilaya ya Songea Mjini wanafunzi darasa la saba mwaka 2004 ni 2675, madarasa yaliyohitajika 9, nyumba za walimu 6. Jumla ya ruzuku milioni 117.

Wilaya ya Songea Vijijini wanafunzi darasa la saba 2004 ni 5255, madarasa yaliyohitajika ni 20, nyumba za walimu 11. Jumla ya Ruzuku ni shilingi milioni 236.

Jumla inakuwa wanafunzi wa darasa la saba 20,659, madarasa 76, nyumba za walimu 36 na jumla ya ruzuku kama nilivyokwisha sema shilingi milioni 856.

(c)Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa MMES vigezo vilivyotumika katika kupanga mgao wa ruzuku ya maendeleo kwa kila Wilaya ni kuwezesha Wilaya kufikia lengo la kitaifa la kupeleka asilimia 35 ya watahiniwa wa Darasa la Saba wa mwaka 2004 kuanza kidato cha kwanza mwaka 2005.

Majengo yanayohitajika kuongezwa ili kufikia kiwango hicho yanavutia ruzuku ya maendeleo ya shilingi milioni saba kwa darasa na shilingi milioni tisa kwa nyumba ya mwalimu.

Mheshimiwa Spika, msimamizi mkuu wa *MMES* ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kupitia Idara ya Elimu ya Sekondari, ambapo Mkuu wa shule akishirikiana na Bodi ya Shule na Kamati ya Ujenzi wa shule ni msimamizi mkuu katika kutekeleza mpango huu katika ngazi ya shule.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa, takribani katika kila Wilaya zimeshapelekwa fedha hizo za mpango wa MMES na kwa kuwa katika Wilaya ya Songea Vijijini kata ya Tanga, Litisha, Kilagano, Lilambo na Winu wameshaanza ujenzi wa majengo hayo kwa vigezo vinavyotakiwa na maeneo mengine wameshamaliza majengo hayo kwa nguvu za wananchi tu bila fedha hizo za mpango wa MMES.

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kupeleka fedha hizo katika Halmashauri hiyo ya Wilaya ya Songea kwa vigezo alivyovitaja kwenye jibu lake la msingi ili kusaidia nguvu za wananchi kuokoa majengo yaliyokwishajengwa na mengine kukamilika?

Mheshimiwa Spika, pili, ni kwa nini fedha hizo zimechelewa sana kufika katika Halmashauri hiyo ya Wilaya ya Songea mpaka sasa hivi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nafurahi kusikia kwamba sasa Kata alizozitaja wamekamilisha ujenzi wa majengo. Sasa ruzuku ya maendeleo katika Mpango huu wa Elimu ya Sekondari haiendi kwenye Halmashauri, ruzuku ya maendeleo inakwenda shuleni, tuliona Halmashauri za Wilaya zina mzigo mkubwa wa utekelezaji wa MMEM. MMEM fedha zinapitia Halmashauri ya Wilaya, lakini Mpango wa MMES fedha zinakwenda kwenye shule za sekondari na kama sekondari ile ni mpya haina Bodi ya Shule wala haina *Headmaster.* Kwa hiyo, hawana akaunti, tuna utaratibu wa kupitisha fedha hizo kwa shule mlezi.

Mheshimiwa Spika, fedha zilipelekwa kwa shule mlezi kulingana na mapendekezo yaliyoletwa na Wilaya kupitia Afisa Elimu wa Mkoa, ambayo yanasema katika eneo hili shule hizi mpya zinazojengwa, shule yao mlezi ni hii. Sasa ruzuku hii ya maendeleo ilitolewa kulingana na hatua ya majengo iliyofikiwa, kama kulikuwa na kuchelewa hawakuweza kukagua kuona utekelezaji, angalau boma limejengwa, shule hiyo haikuingia katika kupata ruzuku ya maendeleo katika mwaka huu. Lakini kama ilikuwa imekwishafikiwa, inabidi tuangalie ni shule ipi na ipi. Kama ilikuwa imekwishafikia hatua hiyo, basi fedha hizo zimekwishatumwa kwa shule mlezi. Tunaweza kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuangalia moja moja iko wapi na katika hatua gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, kwa nini fedha hizo hazikupelekwa katika Halmashauri ya Wilaya. Kwa kweli hili linafanana na maelezo ambayo tayari nimekwishayatoa. Tunaweza kuchambua moja moja tukajua tatizo liko wapi, lakini kama hizi ni shule ambazo haziku-*qualify,* yaani hazikufuzu kupata ruzuku ya maendeleo kwa mwaka huu tunaoumalizia sasa, maana yake ni kwamba *automatically* zinaingia sasa katika Bajeti mpya ambayo makisio yake nitayawasilisha hapa Bungeni mnamo tarehe 5 Julai, 2005.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, sasa tuendelee na shughuli nyingine tukianza na matangazo kama ifuatavyo:-

Kuna tangazo la kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Masoub, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 24 Juni, 2005 mara baada ya kipindi hiki cha maswali, wajumbe wa Kamati wakutane Chumba Na. 227, Ghorofa ya pili. Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Wabunge Wanawake anaomba wakutane hapo nje tu mara baada ya maswali kwa kazi fupi ya kupanga safari ya kwenda kwenye mazishi ya Mheshimiwa Margareth Bwana. Hali kadhalika, nilipotangaza uwakilishi wetu katika mazishi hayo nilikuwa sijakamilisha mawasiliano na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, sasa tumekamilisha mawasiliano na ameniambia kwamba Kambi hiyo ya Upinzani itawakilishwa kwenye mazishi ya Mheshimiwa Margareth Bwana na Mheshimiwa Mutamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara.

Mwisho wa matangazo tunaendelea na *Order Paper*, Katibu tuendelee.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2005 *(The Finance Bill, 2005)***

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Huo Muswada ndio utakamilisha shughuli za Bajeti hapo tutakapomaliza kujadili Wizara zote ndio unaoitwa *Finance Bill.* Tunausoma leo kwa sababu ndio umetimiza siku 21 zinazotakiwa na Kanuni. lakini utakuja kusomwa mara ya pili baada ya kukamilisha mjadala wa Bajeti za Wizara zote.

Tunaendelea na *agenda* inayofuata. Katibu, endelea na *Order Paper. (Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006

### Wizara ya Kilimo na Chakula

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya awali ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Lakini kabla ya kuanza kuchangia naomba kwa heshima na kwa huzuni kabisa nitoe pole kwa ndugu, familia, jamaa na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Margareth Bwana. Kwa kweli tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke pema roho yake. Sisi tunasema *Inna Lilahi waina ilaihi rajiuna*. Mungu ametoa na Mungu ametwaa, jina lake lihimidiwe.

Naomba pia nitoe pole kwa kifo cha Mheshimiwa Abuu Kiwanga wa Jimbo la Kilombero, kwa familia yake, jamaa na ndugu na pia naomba Mwenyezi Mungu aiweke pema roho ya marehemu huyu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba pia nichukue nafasi hii kwa heshima kabisa kuwapongeza ndugu zetu hasa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na CCM kwa ajili ya kugombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba pia nimpongeze mgombea mwenza Dr. Ali Mohammed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza na pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea Urais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa naomba nijielekeze katika hoja iliyopo mbele yetu ya kujadili bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Naomba niwapongeze pia Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa bajeti nzuri ambayo wameiwasilisha jana. Ni Bajeti nzuri ambayo kwa kweli tunaanza sasa kuona dhamira ya Serikali ikijionyesha ya kuanza kushughulikia kwa vitendo sekta hii ya kilimo. Ni muda mrefu tumekuwa tukizungumza na hasa tangu wakati wa uhuru, kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Maandiko mengi yamepita yakizungumzia kilimo lakini kwa kweli uzito unaostahili ulikuwa bado haujapewa katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunajua wazi kwamba kilimo kinaajiri asilimia sabini ya Watanzania wote. Sasa rasilimali tunayoiangalia ambayo inatakiwa iendane na asilimia sabini ya hawa Watanzania wote kwa kweli ilikuwa bado haijaanza kuwekwa hapo, inawezekana ni kwa sababu ya hali yetu ya kifedha, lakini hata hivyo ni lazima tunatakiwa kwa vyovyote vile hata tukiwa na hali ya namna gani kwa vile tunajua ndio uti wa mgongo, tunajua ndio mkombozi wa uchumi wetu, kwa kweli tunatakiwa tuipe sekta hii umuhimu mkubwa na kwa hiyo tuipe fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba kwa mwaka huu au kwa Bajeti hii, kilimo kimeweza kuongezewa asilimia 84.4 zaidi kuliko Bajeti ya miaka yote ambayo ilikuwa inapewa. Hilo ni ongezeko zuri na nasema naipongeza Serikali kwa ongezeko la namna hiyo.

Lakini bado na-*appeal* kwa Serikali kwamba kwa kweli pamoja na kwamba ongezeko ni zuri bado ongezeko hili si zuri kiasi cha kuweza kukisaidia kilimo kiweze kuinuka. Maana yake tunaona wakulima hasa wadogo wadogo ambao bado wanalima au wanaifanya kazi hii kwa hali ngumu. Sasa tutawakomboaje hawa wakulima? Jinsi tutakavyoweza kuwakomboa ni kuwasaidia nao wajisikie kwamba ongezeko hilo ambalo limeongezeka katika sekta hii ya kilimo linawafikia na liwafikie wakulima wote ukiacha wale ambao pengine sasa hivi wanaanza kujisikia kwa kupewa ruzuku ya mbolea. Sasa kwa sababu kilimo kipo karibu sehemu yote ya Tanzania, basi naomba ongezeko hili lianze kuwafikia wakulima wote.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kilimo tunasema ndio sekta pekee ambayo inaweza kuajiri watu wengi katika nchi hii. Ongezeko la kilimo ambalo tumeliona miaka

kuanzia mwaka 1994 mpaka mwaka 2004 kutoka asilimia 2.1 hadi asilimia 6.0, kwa kweli ni dogo ukilinganisha na jinsi tunavyokwenda. Tungependa kilimo kiongezeke kwa asilimia kubwa ili kiweze kuonekana kwa wananchi wote.

Lakini hata hivyo ongezeko hili la kilimo kwa asilimia sita ni ongezeko lisilo na uhimilivu. Maana yake ni nini? Yaani *is not sustainable*, tukiliangalia kwa sababu bado kilimo kinategemea ruzuku ya Mwenyezi Mungu yaani mvua. Mwaka ambao mvua zitanyesha vizuri, ongezeko linaweza kufika hata asilimia kumi au zaidi, mradi tu hali ya hewa ni nzuri.

Lakini hali ya hewa punde inapokuwa mbaya, basi unaweza kujikuta hata ukafika kwenye sifuri, ukaanza moja tena kutokana na hali ya hewa. Sasa hii bado haitupi hali nzuri, hatuwezi kuendelea katika karne ya leo kutegemea mvua ili tuweze kuona ongezeko linaendelea. Lazima sasa hivi tuje na mabadiliko kulingana na wakati, sayansi na teknolojia na inawezekana kwa sababu ya maendeleo haya Mungu naye ameanza kutusikia kwamba ni lazima tufanye kazi kwa bidii zaidi katika kuendeleza hiki kilimo kuliko kuendelea kumtegemea yeye kutupa mvua.

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii Mungu ametupa mito mingi na sehemu zingine mvua nyingi, lakini hata sehemu ambazo zina mito mingi au sehemu ambazo ni nzuri kwa kilimo, umwagiliaji bado ni tatizo, hatuwezi kufanya kazi hiyo kama inavyopaswa. Kwa hiyo. mimi ninachoishauri Serikali ni kwamba, ongezeko hili lingeweza likawa ongezeko zuri zaidi kama tungeweza kuweka miundombinu mizuri ya kilimo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima hawa kuendeleza kilimo chao. Miundombinu hiyo ni nini? Miundombinu hiyo ni maji, hakuna kitu kingine, maana sasa hivi ndio tunategemea mvua kama maji ya kuweza kuendeleza kilimo chetu. Lakini kama tutawatengenezea miundombinu kama malambo au mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji, kwa kweli tunaweza kujikomboa katika kilimo cha Tanzania na tukawa na ongezeko kubwa kuliko ongezeko hili ambalo sasa hivi ndio tunajisifu kwamba tumeongeza kilimo. Kwa hiyo, naomba Wizara iongeze juhudi zake katika kuangalia masuala ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika umwagiliaji lipo zoezi ambalo lilikuwa limefanyika nchi nzima kwa ajili ya kubaini katika kila Mkoa maeneo ambayo yanawezekana kwa ajili ya umwagiliaji. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amenakiri sehemu akisema kwamba katika Mikoa kama ya Singida, Dodoma, Tabora kila wakati kunatokea upungufu wa chakula na anasema labda anaangalia kuunda hata Tume na wataalam kwenda kuangalia ni sababu zipi zinazofanya upungufu huu uendelee kutokea kila wakati. Mimi nafikiri jibu lipo wazi, nalo ni kwamba, haya ni maeneo na ni Mikoa ya ukame ambayo mvua zake ni chache kila wakati na mvua zake ni za kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, sasa kama jibu hilo ni sahihi na ni maeneo ambayo ni ya ukame, kwa nini Mikoa hii sasa isielekezwe kwa kusaidiwa katika kutengenezewa malambo kwa ajili ya umwagiliaji kwa sababu njaa isingekuwepo katika maeneo hayo, ardhi tunayo kubwa na maji yanaweza kupatikana kwa mvua chache ambazo zinanyesha pamoja na maji ya chini. Tafadhalini tuisaidie hii Mikoa, tusingeweza kutafuta sababu

maana zinaeleweka. Unakwenda kutafuta sababu gani ambayo utasema Mikoa hii ya Shinyanga, Singida, Dodoma na Tabora kwamba inakuwa na upungufu wa chakula kila wakati. Sababu inaeleweka, sababu ni ukosefu wa maji. Kwa hiyo, tupatiwe maji kwani watu ni wakulima, watu wanafanya kazi katika Mikoa hii, tunaomba tupatiwe maji ili tuweze kufanya kazi na mtaona jinsi tutakavyoinua kilimo.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina zaidi ya hekari milioni 29.4 za umwagiliaji. Katika hekari hizo ni hekari 249,992 tu ambazo ndizo sasa tunasema zinamwagiliwa au tumefikia hapo miaka yote. Kutoka kwenye hekta 29.4 milioni, lakini sasa hivi tuna uwezo wa hekta 249.92. Naipongeza Serikali na Wizara kwa juhudi ambazo mmefanya maana kule nyuma tulikuwa tumeshapoteza hata zile hekari chache ambazo zilikuwa zinaweza kumwagiliwa.

Ninachokisema ni kwamba hizi hekari peke yake kama tunaweza kuziendeleza, hatuna sababu ya wakulima wengine hasa wale wadogo wadogo kulima. Nchi hii inaweza kujitegemea kupata chakula pamoja na kuuza na kupata mazao mengine kwa hekari hizi, kwa nini Serikali isijielekeze kwa kasi kabisa kuliko jinsi inavyofanya sasa hivi katika kuhangaikia kilimo hiki?

Mheshimiwa Spika, mimi ningeishauri Serikali kwa kweli tuna watu wengi sasa hivi ambao hawafanyi kazi na hawafanyi kazi kwa nini? Kwa sababu kilimo hiki cha kujikimu, kilimo cha jadi, wananchi hasa vijana sasa hivi hawawezi kwenda kulima kwa sababu hakina uhakika. Hebu tuwatengenezee vijana hawa ajira ya uhakika katika maeneo haya ili waweze kujiajiri.

Tuna vijana zaidi ya milioni mbili na kila mwaka wanaoingia kwenye ajira ni zaidi ya 650,000 mpaka 750,000. Hivi tunategemea ni ajira gani itakayowaajiri hawa vijana pamoja na hawa tulionao. Sasa hivi wanaolima Vijijini ni wazee, hakuna vijana. Bila kuwarudisha hawa kwa kuwawekea mazingira mazuri kwa kweli hatuwezi kuwapata, wote wataingia Mijini kutafuta ajira ambayo haipo.

Mheshimiwa Spika, hili la Mijini tunajidanganya. Kila siku wanapoingia Mijini hawa vijana eti tunawatengenezea sehemu za kufanyia biashara, wanajengewa mabanda na kadhalika. Kwa mfano, kama Dar es Salaam, tunaambiwa sasa hivi tuna watu milioni tatu na kitu kwa sensa iliyofanyika lakini zaidi ya asilimia 46, ni watu ambao hawana kazi, hivi ni wangapi utakaowatengenezea hawa wapate biashara ya kufanya waweze kuishi katika Mji. Hakuna, haiwezekani hata nusu ya hawa, hata robo ya hawa kuweza kuwapatia mahali pa kufanya biashara. Biashara pekee tunayoweza kuwapatia ni katika kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunaona biashara nzuri ni katika kilimo, kwa nini tuendelee kupoteza fedha kidogo ambazo tunazo kwa kuweka mazingira Mijini, kutoa mikopo ya shilingi elfu hamsini hamsini, sijui kufanya nini, kwa ajili ya vijana, kwa nini fedha hizi zote tusiziweke zikaenda kwenye kilimo, tukawatengenezea katika hekari hizi ambazo tumeshazibaini. Tukawapeleka katika *schemes* hizi, vijana wakafanya kazi,

tukawapa na nyenzo. Nina uhakika tukifanya hivyo tutakuwa tumeokoa idadi kubwa ya kila mwaka ya vijana ambao wanaingia katika ajira ya laki sita mpaka saba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo ambayo nilikuwa nayo, naomba sasa Serikali ijielekeze katika kutatua matatizo ya wakulima. Ijielekeze angalau kuboresha kule Vijijini kwa wakulima hawa wadogo wadogo, waboreshe basi namna ya kupata pembejeo, wahakikishe pembejeo pamoja na zana za kilimo zinapungua bei, haiwezekani ukasema unataka uwaondoe wananchi katika kilimo cha jembe la mkono wakati plau sasa hivi inakwenda kwenye laki moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilisahau kufafanua mwanzoni kwamba kwa kuwa kazi ya Mungu haina makosa, basi ratiba yetu itaendelea kama ilivyopangwa yaani mjadala wa Wizara hii utakamilika leo. Jumatatu tutaendelea na Wizara ya Ujenzi kama ilivyo kwenye ratiba.

Kwa hiyo, tujue hivyo kwamba wengine walioomba kuchangia watakosa nafasi na ndio maana nawahamasisha wachangie kwa maandishi.

Tunamwita sasa Mheshimiwa Dr. William Shija, atafuatiwa na Mheshimiwa Halimenshi Mayonga.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu mdogo katika hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Kabla ya kufanya hivyo, naomba na mimi niwape pole ndugu zetu wa Jimbo la Kilombero kwa kifo cha Marehemu Abuu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge mwenzetu na Mbunge wao.

Vile vile, niwape pole sana ndugu zetu wa Mkoa wa Rukwa kwa kifo cha marehemu Ndugu yetu Margareth Bwana, aliyetutoka jana na alikuwa anawakilisha Viti Maalum CCM Mkoa wa Rukwa. Kwa kweli tuna masikitiko makubwa. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, napenda niwape pole sana ndugu zetu wafiwa pamoja na jamaa wote pamoja na Bunge hili Tukufu na namwomba Mwenyezi Mungu ajalie roho za Marehemu hawa wakae mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, pili, na mimi napenda niungane na wenzangu kuwapa pongezi nyingi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambaye aliteuliwa na Chama chetu cha Mapinduzi (CCM) kuwa ndiye mgombea urais wa nchi yetu ya Tanzania. Vile vile nampa pongezi Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, kwa kuteuliwa na Chama chetu cha Mapinduzi kuwa mgombea mwenza na tunawaombea afya njema, maisha marefu na amani moyoni waweze kushiriki katika uchaguzi na sisi tutawasaidia hatimaye waibuke katika ushindi mkubwa, mzuri na wa amani.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampa pongezi Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa kiti cha Urais kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Viongozi hawa ambao Chama cha Mapinduzi kimewaamini mimi nadhani tutaungana wana CCM na wananchi kwa ujumla tuweze kuwasaidia na wao watusaidie vile vile kuongoza nchi yetu baada ya Uchaguzi Mkuu unaofanyika mwezi Oktoba.

Mimi nasema hivyo kwa moyo wa dhati kabisa, kwa sababu na mimi nilishiriki katika kinyang'anyiro hicho na baada ya kushiriki kwa moyo wa dhati kabisa na nguvu zote sina kinyongo chochote kabisa na kuteuliwa kwa viongozi hawa na badala yake naahidi kuwasaidia kwa namna yoyote ile ambayo Mwenyezi Mungu atatujalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nizungumzie mambo machache juu ya hoja ya Waziri wa Kilimo. Kwanza nampongeza sana Waziri wa Kilimo, msaidizi wake Naibu Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Kilimo ambao ni wengi, wazuri, wamesoma, wamebobea katika nchi yetu, kwa kweli tunawapongeza sana kwa kazi zote ambazo wamejitahidi kuzifanya katika kipindi kirefu baada ya uhuru wetu. Ndio maana tunajua kwamba sekta ya kilimo kwa kweli ni nzito, ni sekta nyeti na ni sekta ambayo Mheshimiwa Hamis Nguli aliyenitangulia amesema ni sekta inayotoa matumaini ya ajira kubwa.

Lakini ajira kubwa katika kilimo ni ile ambayo lazima iendane na teknolojia za kisasa ili iweze kuwachukua vijana wengi kushiriki katika kilimo cha kisasa na hatimaye tuwe na tija katika sekta nzima ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa nishauri mapema kabisa kwamba mimi nafikiri nchi yoyote inapokuwa inashughulika na mambo ya maendeleo ya uchumi inatazama rasilimali zake na rasilimali zetu zipo katika kilimo.

Ningependa nipendekeze kwamba Rais ajaye namwomba aunde vizuri hii Wizara, ikiwezekana aunde upya iwe na mfumo ambao utaweza kutegemeana vizuri na kufanya uratibu unaoweza kutoa tija na kutupa mawasiliano yanayotakiwa katika sekta ya kilimo, kwa mfano, mfumo nilikuwa nafikiri uwe ni ule wa kilimo, mifugo, ushirika na masoko. Vikae pamoja ili kuweka wataalam kuelewana wanafanya nini.

Hilo jambo naliona ni kubwa kwa sababu ukiweka Wizara mbili unaweza ukarahisisha, lakini mawasiliano tuliyonayo katika sekta ya umma mara nyingi huwa yanaweza kuleta migogoro kama ambavyo tumeona katika sekta ya masoko kuhusiana na mazao mbalimbali kwamba inaleta matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uratibu mwingine ambao naupendekeza ni ule baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametaja

katika ukurasa wa 63 mpaka 64 kwamba, wataangalia namna ya kuachia majukumu katika Serikali za Mitaa au katika Halmashauri.

Sasa kitendo hicho lazima kiangaliwe kwa makini, tunaweza kufika mahali tukafanya kitendo kama kile tulichokifanya cha kuondoa kazi fulani fulani Mikoani na kuzipeleka katika Halmashauri bila maandalizi kamili na hatimaye wakulima watapwaya, watapata matatizo na wakati huo huo sisi tutapata hasara kama Taifa katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo naomba sana tuliangalie kwa makini sana, Halmashauri zetu nyingi bado ni hafifu katika utaalam na kwa hiyo lazima tuzisaidie kwa namna ya pekee ili jukumu hili liweze kutekelezwa vizuri.

Kwa hiyo, uratibu huo nauomba ufanywe vizuri na kwa msingi kwamba sekta ya kilimo inasimamiwa hasa na ugani. Ugani katika nchi yoyote ile inayoendesha kilimo vizuri iwe ni Marekani, India, China au maeneo mengine ambayo yameendesha kilimo vizuri, sehemu au kitengo cha ugani ni muhimu sana.

Sisi Tanzania lazima tuendelee kujiuliza. Je, tunaendeshaji huduma ya ugani ukilinganisha na huduma ya ugani iliyokuwa inafanywa hata kabla hatujapata uhuru. Je, tunafikia kiwango hicho au tunapwaya?

Mheshimiwa Spika, ninavyoangalia katika Vijiji vyetu naona tunapwaya katika eneo la ugani na ndio maana hata kilimo cha umwagiliaji maji kinakawia kutekelezwa kwa sababu baadhi ya wataalam wetu kwa kweli utakuta hawana utashi ule wa kumfuatilia mkulima vizuri kila atakapoanza kilimo chake cha zao lolote lile kuanzia wakati anatayarisha shamba lake, wakati anatafuta mbegu, wakati anafanya mambo mengine ya madawa na kadhalika, ili kuona kama je, anapata huduma ile anayostahili ili kuendeleza kilimo chake?

Mimi naona tuko hafifu kweli katika huduma ya ugani na naomba suala hilo sasa tujielekeze, tujiimarishe, kama Maafisa Kilimo wetu walio katika Vijiji vyetu na Kata zetu wanaonekana basi hawahudumiwi vizuri, basi Serikali iangalie namna ya kuwahudumia vizuri ili nao wawahudumie vizuri hao wakulima katika eneo la ugani.

Bila Ugani kilimo chetu kitaendelea kuwa duni na wakulima watakata tamaa, baadhi kwa kweli wameishakata tamaa, lakini hawana sababu ya kukata tamaa kwa sababu ardhi ipo, mbolea inapatikana, katika maeneo mengine kama maeneo ya Mikoa yetu ya Mwanza, Shinyanga na kadhalika mbolea ya samadi ni nyingi inatumika, lakini Huduma ya Ugani inakuwa ni hafifu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo. Sasa napenda nijielekeze kwenye kilimo cha zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria namba 2 ya mwaka 2001 ambayo ilijielekeza katika maendeleo ya zao la Pamba. Katika sheria hiyo kuna vipengele vingi vilivyozungumzwa, lakini pamoja na kuwa na Bodi, Wasimamizi na Watafiti na kadhalika. Ilitupa matumaini Sheria hiyo kwamba zao la pamba baadaye lingeweza kuimarika. Lakini kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula ni kwamba mwaka hadi mwaka zao la pamba linaonekana linayumba kwa sababu au bei ya Kimataifa inakuwa ndogo au mvua inakuwa kidogo. Lakini mimi naona kilimo cha pamba kinakuwa hafifu kwa sababu ya kutofuatilia vizuri.

Mheshimiwa Spika, sheria hii mimi nina mashaka kwamba hatujaifuatilia vizuri. Nimejikumbusha katika vipengele mbalimbali vya Sheria hiyo na nimeona kwamba kuna maeneo mengi ambayo bado hatujayatekeleza kwa maana ya kuimarisha zao la pamba. Matokeo yake kuna kero chungu mzima kwa wakulima, mwaka juzi nilileta kero hapa ya mbegu ambazo hazikuota. Nilimshukuru Mheshimiwa Waziri na baadaye tulimshukuru wengi wakulima wa pamba kwa sababu alifuatilia mpaka kwenye Mikoa yetu akaona kwamba ilikuwa kweli kuna mbegu zilizotawanywa lakini hazikuweza kuota baada ya kupandwa. Sasa kero hiyo je, imekwishakwisha sasa na hatutapata tatizo hilo tena? Ningependa nihakikishiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini kero nyingine ni juu ya ununuzi wa pamba. Baadhi yetu katika maeneo yanayolima pamba tuna mawazo kwamba zao la pamba lingeweza kuwekewa wanunuzi mahsusi badala ya kuachiwa huria tu wakati wowote wanaingia wanunuzi wachache au wanaingia wanunuzi wengi. Wakiingia wanunuzi wachache basi wanabana bei na wanaelekea kuwapunja wakulima, wakiingia wengi ndiyo bei inafunguka. Sasa hivi nilikuwa nazungumza na ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Kabisa, hapo nje amesema kwamba kwa bei ilivyo katika soko la dunia sasa hivi inawezekana kabisa bei ya pamba ikaongezeka kwa jinsi msimu huu ulivyoingia umeingia na bei ya shilingi 170 na 180 kwa kilo, kitu ambacho ni mapunjo makubwa kutokana na jinsi mkulima alivyowekeza kwenye kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanyaje ili bei hizi zisiwakatishe tamaa wakulima hawa na kwa jinsi bei ilivyo sasa katika soko la dunia naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula atuhakikisha je, wakulima sasa bei itaongezeka kwa mpango gani, kwa usimamizi gani na kwa matumaini gani kwa kuwa wakulima wa zao la pamba wanasubiri huko Vijijini kwetu ili waweze kujua kwamba kuna matumaini na waweze kuendelea kulima zao la pamba na kwa maana hiyo kuweza kujikimu na umaskini kutokana na mpango wetu wa MKUKUTA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa vilevile kuna kero ya madawa. Kuna baadhi ya madawa yanauzwa lakini si madawa ya kweli. Ni madawa ambayo watu wameyachanganya na maji na wameyachanganya na vitu vingine sasa usimamizi wake ni upi ili mkulima asiweze kupata hasara ya madawa ambapo atakuwa amepata madawa hafifu wakati anasimamia pamba yake.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna kero ya miundombinu. Zamani kulikuwa na fedha ambazo zinahudumia miundombinu katika maeneo yanayolima pamba fedha hizo zimekwenda wapi? Tungependa tuelezwe ili kusudi miundombinu hii ikiwepo kama barabara zinatengenezwa Vijijini katika maeneo yanayolima pamba basi tujue kwamba wakulima watakuwa na urahisi wa kuweza kupeleka mazao yao wakati wa kuuza.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kumekuwa na kero ya uchafu wa pamba. Sasa nataka niiulize Serikali yenyewe inafanyaje kumsaidia mkulima asiwe na tatizo la uchafu wa pamba kwa nchi yetu ili tuweze kupata bei nzuri ya pamba na tunafanya nini tusiwe na uchafu wa pamba na tusiendelee kumsingizia mkulima kwamba ndiye anayesababisha uchafu huo.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda niseme kwamba katika mambo ya bei nikisisitiza nasema kwamba inatushangaza wakati mwingine katika mwaka 2004/2005 msimu huo, baadhi ya wakulima wapunjwa bei na mpaka Serikali ikaingilia kati na hapa Waheshimiwa Wabunge kutoka Mikoa inayolima pamba tukakutanishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu akasimamia juu ya kurekebisha bei badala ya shilingi 275 ikawa sasa 300, mapunjo hayo mengine baadhi ya wakulima hawajafidiwa.

Nasema katika Kata zangu kwa mfano, za Tabaruka, Igalula, Busisi, Kaguga, Buzirasoga, Sima, Nyamazungo, Kasugamire na hata Kata zingine nyingi katika Jimbo la Buchosa na hata katika Mkoa wa Mwanza kwa ujumla na Mkoa wa Shinyanga baadhi ya wakulima waliopunjwa hawakufidiwa. Kwa nini Serikali haikufuatilia ili kusudi wakulima hao waliopunjwa waweze kufidiwa na wasiwe na kinyongo tena juu ya harakati zao za kujikimu na zao la Pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nimalizie kwa sababu kengele ya pili, inakaribia. Niseme tu kwamba kutokana na sheria hii ya pamba ya mwaka 2001 kwa nini usianzishwe mfuko wa kukinga bei ya zao la pamba. Tunaweza kabisa pale pameandikwa *Cotton Development Fund* katika Ibara nafikiri ya 48. Lakini mbali na *Cotton Development Fund*, Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba kwa nini tusiwe vilevile na Mfuko wa kukinga bei ili mkulima aziweze kuyumba mwaka hadi mwaka katika mapato ambayo yanatokana na bei ya dunia na sisi ni sehemu ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba bado kuna kazi kubwa kwa kilimo cha zao la pamba nchini na tusingependa kuwakatisha tamaa. Naomba Serikali isimamie na ninaomba zao la pamba lionekane kwamba ni zao letu. Mwenyezi Mungu ametupa hali ya hewa tuliyonayo kwa ajili ya kuzalisha pamba na ikiwezekana tuweze kuimarisha hata viwanda vyetu na hatimaye tupunguze umaskini ambao tumeuwekea mpango maalum.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa nafikiri wa 54 Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula amezungumza vizuri sana kwenye hotuba yake juu ya Mpango wa Wizara wa kutekeleza Programu ya Sekta ya Kilimo. Hayo maelezo ni mazuri sana, wasiwasi wangu ni kwamba je, tutatekeleza kikamilifu programu hiyo, tutasimamiaje, tutapanga

nani asimamie maana huo ndiyo udhaifu wetu kwa kadri ninavyofahamu. Sasa udhaifu huo tuuondoe tunaenda sasa kwenye Serikali ya Awamu ya Nne wako watendaji wazuri tu wanaoweza kusimamia mambo haya. Mheshimiwa Waziri tuungane kwa pamoja Watanzania tuweze kuinua kilimo kwa ujumla ikiwa pamoja na umwagiliaji maji, lakini vilevile zao la pamba tuhakikishe kwamba linakwenda vizuri kwa muda wote.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na Serikali na ninawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya asubuhi niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu Waheshimiwa Wabunge ambao wameaga dunia katika kipindi hiki tukianzia na Mheshimiwa marehemu Abu Kiwanga na hatimaye Mheshimiwa marehemu Margareth Bwana ambaye alifariki siku ya jana. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwanza ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa asilimia mia moja ili iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongea mambo machache kwa sababu muda wa dakika 15 huu ni kama *breakfast* hautoshelezi. Nimekuwa Mbunge tangu mwaka 1990 tulikuwa na utaratibu Mheshimiwa Mbunge alikuwa anaongea kwa muda wa nusu saa, mimi nafikiri tukirudi itabidi tuurudishe wa kuongea kwa zaidi ya nusu saa kwa sababu mambo ya kuzungumza yapo mengi kweli. Tunafanya haraka kwa sababu tunaenda kwenye uchaguzi, lakini taratibu na kanuni tukirudi hapa tutafanya marekebisho ya hilo, maana sisi ni wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi salamu kama utakuwa umerudi hapa nafikiri wewe ni mtu maarufu sana utatekeleza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza, mazao ya biashara yana gharama kubwa kubwa hayana mfano na hao wanayoyalima hayo mazao ya biashara inaonekana wanaendelea kupata hasara. Ukichukua zao la kahawa ile gharama ambayo anatumia mpaka anavuna kahawa hailingani na ile bei ya sasa hivi anayouza kahawa. Sasa hayo mazao yanaweza yakapotea kwa muda mfupi. Kuna mkakati gani katika bajeti hii tuliyoileta ili kulinda bei kwa wale wanaolima yale mazao ya kahawa, pamba, pareto, korosho kwa sababu yana gharama kubwa. Sijui kama mmeishafanya utafiti na kuona kwamba mtu wanayelima mazao hayo anapata faida kwa kiwango gani kwa eka moja. Sasa hapa tuwainue wakulima.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka juzi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema anaanzisha Benki ya Wakulima na Wavuvi, nimekaa nikisubiri utaratibu huo wa Benki ya Wakulima mpaka leo sijaiona. Lakini kwenye bajeti yake alielezea Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Hiyo Benki ya Wavuvi mpaka leo hakuna. Kule tuna Ziwa Tanganyika wangeweza wakavua samaki kwa kutumia mikopo ya Benki hiyo ya Wavuvi lakini hawana mikopo Ziwa lipo na samaki ni wengi, lakini umaskini ni mwingi.

Sasa hii MKUKUTA sijui mtaunda jina lingine si mbali tu na itakuwepo MKUKUTA na mingine ni uundaji wa majina lakini hatujaona kasi ya mabadiliko ya watu ambao kweli wanalengwa halafu wanabadilika kimaisha maneno ni mengi tu.

Mheshimiwa Spika, sasa sielewi kama kweli tutafika huko tunakoelekea kwa kuondoa umaskini. Unaondoaje umaskini wakati watu hauwawezeshi mfukoni haiwezekani. Kwa hiyo, watu wengi wanataendelea kulundikana Mijini, Wamachinga watazajana katika Jiji la Dar es Salaam na hakuna njia nyingine ya kuepusha suala hilo na hakuna utaratibu unaopangwa na hakuna majibu sahihi.

Mheshimiwa Spika, sasa wakulima hao wenye umri wa miaka 60 na 70 ndiyo bado wanatumia jembe la mkono wanalima kweli wanaweza wakaondoa umaskini hata hii bajeti sijui kama kweli inawalenga wao. Tunafanyaje utaratibu, sasa nguvu mpya ya kizazi wanakimbia suala la kilimo, wanataka kufanya biashara ya kubeba vyombo mkononi, wanabeba *radio* mkononi na mikanda wanatembeza. Ukiwahesabu kwa kila Mkoa wale ni wengi sana. Sasa hawana malengo na hawana mwelekeo na mimi nafikiri kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula pamoja na kwamba inapewa fedha nyingi ndiyo Wizara inayohusika kwa sababu kote duniani huanzi na kutayarisha viwanda bila kilimo huwezi hata uende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu msingi wa kwanza hata mtoto mdogo anapoanza kukaa, unaona amelelewa ameanza kutembea, unaona anaanza kutafuta kulima kama ana mti unaona anachimba chini anapanda, kwa maana msingi wa kwanza ni kilimo. Sasa tumeimba sana kilimo tangu mwaka 1990 kilimo ni uti wa mgongo, sasa nafikiri tugeuze isiwe uti wa mgongo tulime tu. Hili neno uti wa mgongo ni nadharia na wanaanza kuchoka nalo.

Sasa mimi naomba kwamba kweli gharama ya mazao ni kubwa na kama ni hivyo ni kubwa. Sasa tupendekeza basi kama soko la dunia la kahawa linaonekana katika nchi jirani kwa nini tusiwaruhusu hao wakulima wakauza mazao yao huko, Serikali inazuia nini? Hivi mkulima wa Marekani akisikia soko la kahawa au pamba yake Tanzania akataka kuleta ile Serikali ya Marekani inamzuia kuileta Tanzania. Sasa Serikali yetu bado ina vikwazo vya vizuizi waacheni watu wauze mazao yao katika nchi jirani, kama watu wa Arusha wamelima mahindi yao wanataka kuyauza Kenya bado mnawazuia, mnawazuia kwa misingi gani waache wakauze huko.

Mheshimiwa Spika, leo gharama ya kuzalisha mahindi hayo tulikuwa tunaongea hapa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe akanionyesha kwenye kitabu akasema hapa wanatengeneza hasara tu. Kwa sababu unapofanya *irrigation* kwenye

mahindi, afadhali hiyo *irrigation* ingekuwa inafanyika kwenye maharage, njegere na haya mambo ya *hot culture* ni nafuu. Lakini unaweza kusema kabisa umebeba gunia la mahindi ni hasara labda huyo anayebeba mahindi sasa hivi ya kuchoma akayachukua huko Dar es Salaam akayafikisha hapa kwa sababu mhindi mmoja ni shilingi 200/= hata hapo anaweza akapata faida kuliko sasa hivi kilimo cha mahindi ambacho unazalisha halafu ule ugali una gharama siyo ya kawaida. Hebu tuwasaidie hao wakulima kweli mimi naona kuna hali ngumu.

Mheshimiwa Spika, lingine niombe tu kwamba hivi suala la ruzuku tuliyoweka, hivi hiyo Mikoa tuliyosema kwamba watapewa ruzuku ya mbolea wanafika wapi. Mimi Kigoma sijaiona hiyo mbolea na watu ambao mimi nilifika kule nikawashawishi wafanye taratibu zote kule Halmashauri wakafanya, wakaja Wizarani mpaka leo hawajapata. Bahati nzuri huu ni mwezi Juni, Julai, Agosti, mwezi Septemba Mkoa wa Kigoma tunapokea mvua, mwezi wa Septemba, Oktoba, Novemba, Desemba mpaka mwezi wa Mei, mwaka kesho mvua iacha kunyesha hivi kama mwezi Juni, mwaka kesho, sasa hivi kama hatuwezi kupata mbolea hiyo ya ruzuku hivi maelezo ni yapi?

Hiyo mbolea naomba Mheshimiwa Waziri unipe sasa yaani nikiondoka hapa unipe mbolea mimi niibebe maana wataalam wako huko sijui ni Mkurugenzi wa namna gani, wana matatizo sijui wanataka rushwa tuwapelekee huko. Mheshimiwa Waziri ni mtu wa kura hawezi kuomba rushwa siyo rahisi kuomba rushwa nasema hili kwa uchungu kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, kitu tumekipitisha hapa Bungeni na tumekubaliana, kwa sababu mwanzoni walikuwa wametangaza Mikoa ile maarufu, lakini na ile Mikoa yenye kupata mvua ya kutosheleza ni maarufu. Sasa watawezaje kusubiria kipindi chote hicho hakuna mbolea kuna jibu la namna gani. Sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula tunaheshimiana sana na yeye amewahi kukaa Kigoma. Kwa hiyo, Mkoa wa Kigoma kama anausahau atuambie, anieleze hapa hapa na mimi niende niwambie kwamba ameusahau pamoja na kwamba alikaa muda mrefu na alipata na watoto pale pale na wengine tuliwapa majina ya Waha lakini ameusahau. Naomba kupata jibu katika hilo kwamba ananipa tani ngapi za mbolea wale watu wana fedha zao tayari. Wale watendaji wake Mheshimiwa Waziri ndiyo hawamsaidii na hawana majibu sahihi kwa sababu walikuja pale wanagonga mwamba. Sasa walipokuja wakasema mbolea imeisha ni majibu tu ya kuweza kueleza kwamba mbolea imeisha wewe ukakubaliana nao. Hilo siliungi mkono. Nisipopata maelezo ya kina basi mimi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula humu ndani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la barabara za wakulima. Hizi barabara za wakulima hao wanaozalisha mazao kule Vijijini wanabeba mazao yao kwa baiskeli. Hivi mawasiliano ya hizi barabara ukitazama kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi inakuwa imeandika hizi barabara hakuna mawasiliano. Mimi ningetoa ushauri kwamba kuwepo mawasiliano kati ya Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Kilimo na Chakula huwezi kulima mazao porini halafu akayabeba kichwani huyo mtu anachoka. Wakati kuna *Pla*n Halmashauri wamechora ramani za barabara za kwenda huko kwa wakulima, lakini

hawawezi kupata hizo fedha za kutengeneza barabara na hatuna barabara za namna hiyo wanakuwa wameeleza tu pale.

Mheshimiwa Spika, sasa tuwasaidie hao ili waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi wanalalamika sana kwenye Jimbo langu wale wakulima wanapata tatizo la kutosha kweli kweli na halina dawa. Sasa ningeomba labda kama kuna maelezo yaliyosahihi hilo litiliwe mkazo mzuri vinginevyo tutazidi tu kuimba kilimo ni uti wa mgongo, tutawaongezea barabara, barabara watasubiri hazionekani watu wengi wanazidi kukimbilia Mijini basi tuwashawishi vijana wote waje walundikane Mjini, jambo ambalo si sahihi kabisa. Kipindi fulani vijana wale wamachinga walijitolea kwenda Morogoro walikosea nyenzo tu, walikosa nguvu ya kuweza kuwasaidia na Serikali ikawaacha. Sasa leo ukisema kwamba Serikali ni soko huria wajitegemee bila watu kwenda kuwafuatilia siyo utaratibu.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Waheshimiwa Wabunge wa Uganda tunawauliza hapa, je nyie wale wanaoanzisha kilimo huko Vijijini mnafanyaje? Wakasema kuna wataalam maalum wa kwenda kuleta ripoti. Sasa hapa nchini wote wanakaa ofisini tu hili jambo lazima lifanyiwe mabadiliko.

Sasa sisi ndiyo tumeshinikiza kwamba nguvu kubwa ihame kutoka Wizarani na Mkoani iende Wilayani na ikienda Wilayani iende kwenye Kata, ikitoka kwenye Kata iende Vijijini sasa hao wataalam wanafanya nini?

Lakini tangu zamani kwenye ukoloni mimi nilikuwa naona tu watu wanatembea Mbwana Mashamba walikuwa wa kutosha, unamwona tu anavamia mashamba humfahamu anatoka wapi, pengine unasema kwamba ni mtu anayeenda kutaka kufanya uhalifu, lakini unakuta anatayarisha vizuri, lakini leo hakuna kitu. Haya mambo tunayasahau wapi? Watu wanadai nyongeza za mishahara tu bila utendaji maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba jambo hili litiliwe maanani kwa sababu muda ni kidogo narudia tena kusema kwamba hatukupata mbolea ya ruzuku kwenye Jimbo langu la Kigoma Kaskazini na wale wananchi kweli wanahitaji na sisi tunahitaji mbolea mapema kwa sababu kama kutapatikana uwezekano huo basi kwenye mwezi huu wa Juni na mwezi Julai iwe imeishawafikia.

Tunajua usafiri wa kule Kigoma ni ngumu vilevile kwa sababu hayo yote yanahitaji maandalizi. Mkoa wa Kigoma usafiri una ratiba zake kwa sababu treni siyo kila siku, ndege ni kila siku lakini sijui kama tunaweza kubeba mbolea kwa ndege, kwa hiyo ni Mkoa unaohitaji uangalifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa mara nyingine tena. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya hii ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kutoa pole sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Misungwi kwa familia za ndugu zetu wote wawili Mheshimiwa marehemu Margareth Bwana na Mheshimiwa marehemu Abu Kiwanga kwa vifo vyao vyenye masikitiko makubwa sana. Tunaomba sana Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao wote wawili mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya majonzi hayo. Nitoe pongezi za aina ya pekee kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi uliofanyika Chimwaga kwa kazi nzuri sana waliyoifanya ya kuweza kumchagua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kura nyingi sana tunapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri. Lakini pia tunampongeza yeye mwenyewe Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete tuna imani naye na pia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kwake naye ili aungane katika shughuli nzito hiyo ya kuweza kuliongoza Taifa hili pamoja na ndugu yetu Mheshimiwa Rais Amani Abeid Karume katika nchi yetu upande wa Zanzibar. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Misungwi kwa kweli kutokana na kazi hii iliyofanyika Chimwaga wao walifikiri kwamba kama wamemaliza kazi kwa niaba yao, wamejiridhisha kabisa kwamba Rais ameshapatikana, Makamu wa Rais yupo na Rais wa Zanzibar ameshapatikana. Tayari wananchi wa maeneo ya Misungwi huko wanaimba nyimbo nzuri tu na wamepanga mambo yanaendelea. Kwa hiyo, hii naona kwamba kazi huenda imeishaisha na tutaungana nao katika utaratibu huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula imepangiliwa vizuri, ina maana kuna watu ambao wamekaa na kuifanyia kazi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu ndugu Ngirwa na Wakurugenzi wote wameshirikiana vizuri na wameileta hotuba hii kwa wakati ambao kweli imepangiliwa kwa maana kwamba watu mnakaa kwa pamoja. Kwa hiyo, mimi inaniwia vigumu kuinyima *marks* za asilimia mia moja. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kazi imefanyika vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana na inagusa watu wengi hasa wakulima asilimia 80. Watanzania walio wengi wanategemea kilimo. lakini zimekuwepo lawama inasukumiwa Wizara hii ya Kilimo na Chakula. Sikatai zipo kweli ambazo ni za moja kwa moja zinawahusu Wizara ya Kilimo na Chakula, lakini zingine haziwahusu. Kwa hiyo, yale yasiyowahusu ambayo wanayabeba Wizara ninawapa pole sana kwa kuyabeba.

La kwanza, mvua kutonyesha siyo suala la Wizara ya Kilimo na Chakula, mkulima anakuwa tayari ameshaanda na amepanda na amefanya palizi, matokeo yake mvua hainyeshi lawama kwa Waziri wa Kilimo na Chakula na wahusika na wengine.

Kwa hiyo, hili ni nzito sana lakini halikwepeki inabidi walibebe na baadaye kuhangaika nalo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubovu wa barabara mkulima amelima mazao yake ameshapata tayari namna ya kuyapeleka kwenye soko siyo suala la Mheshimiwa George Kahama tena anahangaika ni Wizara zingine zipo hapo katikati, lakini lawama hii mtu amekaa na mazao yake ameyafikisha kwenye soko lakini bei imekuwa ni ya chini lawama inakuja kwenye Wizara mbili hizo Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara ya Kilimo na Chakula haliwahusu inabidi Serikali kwa ujumla ifikirie suala la barabara vijijini, wananchi wanateseka sana na mazao yao, yanakosa bei lawama zinakuja kwa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa hiyo nawapeni pole sana.

Mheshimiwa Spika, yapo yanayoihusu Wizara moja kwa moja suala la mbolea kuifikisha kwa wakulima ni wajibu wa Wizara ya Kilimo na Chakula, tunawapongeza sana angalau sasa hivi mnajitahidi sana kwenye Mikoa ya Kusini mnapeleka mbolea kwa wakati, Mikoa ya Kusini wanalima na kupata mazao mengi ambayo yanatutosheleza sisi Watanzania. Tunawapongeza sana watu wa Kusini kwa kweli mmekuwa mkitulea katika kutupatia chakula. Naomba muongeze juhudi katika kilimo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, safari hii zimetengwa bilioni 7.2 kwa ajili ya ruzuku katika Mikoa hiyo ya Kusini kuwapa mbolea wanasaidiwa namna ya kusafirishaji kwa hiyo tunapunguza gharama za usafirishaji wa madawa hayo ambayo ilimhusu mkulima agharamie yeye, hili wamefanya vizuri kwa Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, nikirejea kama wenzangu waliomalizia kuzungumzia sasa hivi zao la pamba lina gharama kubwa sana. Shilingi 300 hata kama ingekuwepo leo kwa mkulima wa zao la pamba haitoshi, gharama ya kuzalisha zao la pamba ni kubwa mno, unyunyiziaji wa yale madawa ni zaidi ya mara tano.

Lakini sijasikia kwamba kuna ruzuku ipi imewekwa kwenye zao la pamba kwa ajili ya madawa hayo ya kunyunyizia ili impunguzie gharama huyo mkulima wa zao la pamba naye angalau aweze kufikia hata hiyo bei. Wakulima walio wengi sasa hivi hawanyunyizii dawa matokeo yake wanapata mavuno kidogo. Kwa hiyo, hata kama ungelimpa shilingi 400 kwa kilo kwenye ekari kwa sababu amepata kilo wakati mwingine 50 kwa ekari hailipi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ifikirie namna ya kupunguza gharama za madawa, madawa ya kunyunyizia ni aghali sana yapunguzwe bei ili mwananchi aweze kunyunyizia shambani ili aweze kupata mavuno mengi na baadaye bei hata kama itakuwa ni ya shilingi 300 mara kilo nyingi kwa hiyo faida atakuwa ameishapata. Naiomba Serikali ilishughulikie hilo na katika majumuisho waone angalau watamsaidiaje Mheshimiwa Peter Kabisa mtu wa Bodi ya Pamba na jinsi ya kumpa ruzuku ili angalau huyu mkulima naye apunguze bei ya madawa ya pamba.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiria labda Serikali ijaribu kuangalia kuwa na kinga ya bei. Nchi nyingine kama India nilienda huko, nikambiwa mpaka Tume ya Bei bado ipo. Mfano kama zao la Pamba inapangwa bei ya shilingi 500, kwa hiyo mkulima analima zao akitegemea kupata shilingi 500, kama itaanguka kwenye soko la dunia ule mfuko au ile kinga ya bei kama ipo basi inakinga pale, kwa hiyo mkulima anaendelea kupata ile shilingi 500, kama itapanda kwenye soko la dunia basi ile ya juu itatolewa itaenda kuwekwa kwenye mfuko ule ili mkulima anakuwa na analima kwa lengo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli bado ni matatizo makubwa sana. Naomba Serikali ilione hilo. Mkulima wa pamba sasa hivi analima bila kuelewa atauza kwa bei gani, alitegemea shilingi 300 kama mwaka jana na sasa hivi ni shilingi 170 anateseka kweli. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kulifanyia kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi ni kame, ina matatizo makubwa sana ya mvua za wasiwasi. Lakini Waziri ameshaliona hilo na kutuweka kwenye programu husishi ya kilimo cha umwagiliaji. Waziri, watu wa Igongwa katika Kijiji cha Mabuki wanakupongeza sana kwa skimu yao ya mwanzo ambayo ni ya mfano inaendelea vizuri na wamepata mpunga wa kutosha. Tunakupongeza sana. Lakini pia bado umetufikiria umetuongezea mradi huo mwingine wa Kijiji cha Lubuga sehemu ya Nyambeho ekta 180 mradi unamalizika kujengwa, ni mkombozi badala ya mvua sasa tunatumia kukinga maji hayo ambayo yanaporomoka kwenda ziwani baadaye waweze kuwahudumia. Niendelee kushukuru kwa skimu zingine mbili za Ilujamate Hekta 200 na Nyashidala kati ya Kijiji cha Kasololo na Nduha hekta 370 ambazo umeahidi Mheshimiwa Waziri kuwa utazimalizia katika mwaka huu wa fedha Nakushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Misungwi ahsante sana kwa kazi yako nzuri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwenye Chuo cha Utafiti Ukiruguru. Kama nilivyosema kwamba Misungwi ni kame ina matatizo makubwa sana ya maji ya kunywa binadamu pamoja na mifugo. Limekuwepo tatizo kwenye taasisi hii ya Ukiruguru. Naibu Waziri alifika pale, Waziri Mkuu alifika na kuna mradi mwingine unaoendelea pale ukaahidi kwamba, kwanza kwenye swali langu la mwanzo kabisa ambalo niliwauliza hapa namna ya kutatua tatizo hilo. Serikali ililivalia njuga na zaidi ya shilingi milioni 120 kwa ajili ya kulipia umeme uliokuwa umekatwa kwenye chuo chetu cha Ukiruguru Serikali ilitekeleza hilo, nawapongeza sana. Lakini baadaye mmetafuta watu ambao watakuja kuwaletea maji wananchi wa maeneo ya Mwalo, njoo hapa Buganda Nyang'olongo mpaka ndani ya chuo chetu cha Ukiruguru ikiwemo Kijiji cha jirani cha Ngudama kumekuwa na ucheleweshho ambayo nadhani mnayafahamu tumeshazungumza Mheshimiwa Waziri pamoja na Katibu Mkuu. Sasa hivi nimepigiwa simu wananchi wanafukua yale mabomba wameanza sasa kutandaza kwenda kwenye mradi wa kuchukuliwa maji Nyakasanga pale. Mheshimiwa Naibu Waziri tulikwenda pale tukakuta *transformer* inaunguruma kwa hiyo nina imani kabisa kwa juhudi zako Katibu Mkuu na wenzako ndani ya miezi hii miwili wananchi wa Ukiruguru watakuwa wamepata maji, utakuwa umenisaidia sana, lifanyie kazi hilo. (*Makofi)*

Maana yamekuwepo malalamiko mengi, Mkuu wa Chuo analalamika kule upande wa mafunzo. Lakini lingine nijaribu kuzungumzia suala la Nane Nane. Nane Nane kwa

kweli ni chombo cha wakulima, kusherehekea sherehe yao. Zamani kilikuwa kinashughulikiwa na Wizara ya Ushirika kupitia wanaushirika ambao ni asasi yao.Baadaye ikaingiliana na siku ya kuzaliwa kwa Chama cha *TANU*, Saba Saba. Lakini baadaye imekuwa ikishughulikiwa na *TASO* ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo. Sasa ningependa tu niulize swali hivi hii *TASO* imeundwa na nani na kwa maslahi ya nani angalau niweze kupata hilo na kimesajiliwa lini na uhalali wake ukoje nielezwe hiyo *TASO.* Uongozi wake Kitaifa ukoje na akina nani wako pale kwenye ile *TASO*, nipate majibu hayo. Wanawajibika kwa nani na wanatoa taarifa kwa nani. Umma wa wakulima na wanaushirika vipi na chombo hicho kabla na baada ya sherehe za Nane Nane ambazo zitafanyika mwaka huu na zimekuwa zikifanyika hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie mradi wa mbarika. Lengo lilikuwa ni ekta 35. Lakini badala yake wananchi wamekuwa wakilalamika kwamba mradi huu kwa kweli umekuwa na matatizo mengi, hauna fedha. Mashine iliyonunuliwa ni ndogo haiwezi ku-*supply* maji kwenye ekta hizo 35. Badala yake kweli ile mashine imekuwa na uwezo wa kuhudumia ekta 8 tu. Sasa wananchi au wana kikundi wale walikuwa wametegemea ekta 35 wagawane kule kumekuwa na mvutano ekta 8 hizi watagawana vipi. Ile mashine kweli iligundulika kwamba haina uwezo wa ku-*supply* ekta hizo 35. Sasa niiombe Serikali waungalie mradi huu wafikirie namna ya kuweza kuwapa fedha ili angalau waweze kufikia lengo hilo na eneo lote kwa ujumla ni ekta 150.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nirudie tena kumpongeza Waziri, Naibu Waziri najua kwamba mna kazi ngumu kwenye majimbo yenu. Mimi kwa kweli dua yangu bado ipo pale pale Mheshimiwa Keenja, Mheshimiwa Mbawala urudipo jimboni kwako nina imani kabisa wananchi wa majimbo yenu wanaona yale mnayoyafanya. Wawajalie sana wawape kura mrudi tena hapa Bungeni tufanya kazi. Baada ya maelezo hayo naunga mkono tena hoja hii nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niongee machache katika sekta hii muhimu kwa Taifa letu. Kwanza kabisa kabla sijaanza kuchangia natoa pole kwa familia na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kupotolewa na mpendwa wao Mheshimiwa Margareth Bwana.

Mheshimiwa Spika, mimi hapa kwanza kabisa ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri pamoja na vielelezo vyote alivyovitoa kama takwimu katika hotuba hii lakini nitakayoongelea ni suala la *strategy* ni suala la sera. Hatumpendezi mtu yoyote tunapoongelea kuwa kilimo kimekua na kinaendelea kukua mwaka hadi mwaka. Ukweli kuwa katika hali halisi kilimo kama kitakua kitahitaji mageuzi makubwa katika maeneo mawili. Moja ni suala la kuvuna maji kusudi shughuli ya kilimo iwe ya miezi 12 sio ya msimu mmoja. Suala hili sioni kwa nini Serikali ina kigugumizi kwa sababu sio kuwa sisi tunaanzisha hili suala la kuvuna maji hapa katika Bunge hili lako Tukufu.

Nchi nyingi pamoja na zile ambazo zinapata mvua nyingi sana lakini maji yanavunwa kwa mpango. Lakini sisi tunalohitaji sasa ni kuanza maandalizi na kukubali hiyo *concept* ya kuvuna maji lakini hapa haijakubalika kabisa. Tunapoongelea inakuwa

tu kujihami na kujitetea, sasa hapa sio Mahakama. Taifa hili litaendelea kilimo kitapokuwa kimeboreka kimepata mageuzi ya kutosha. Kwa hiyo mimi ninavyoiona suala la kilimo ni suala la kufa na kupona kama walivyosema zamani. Kwa sababu kilimo ndicho ambacho wananchi asilimia 70 mpaka 80 ambao wanajihusisha na maisha yao na umaskini wetu utaondokana tu au utapungua kama kilimo kitaboreshwa. Mimi nadiriki kusema kuwa kama tusipokubali dhana nzima ya kuvuna maji ambapo maji yale yatatumika kwa kilimo kwa kweli hatutaendelea. Tunaweza kuja na takwimu za kila namna hapa tukaremba hotuba zetu lakini itakuwa tunajidanganya tu.

Mheshimiwa Spika, tumeongelea suala la uwekezaji kama hatutajenga mazingira ya Mapinduzi katika kilimo na kujenga miundombinu inayoweza kuwavutia wawekezaji waje kuzalisha itakuwa vigumu sana kuwapata wawekezaji. Kama tutakuwa tumeweka mazingira ya kujenga miundombinu kama kujenga mabwawa, mifereji, kupeleka umeme vijijini nina uhakika tunaweza kupata wawekezaji wadogo na wakubwa ambao wanaweza kuwekeza kwenye kilimo. Ardhi yetu asilimia kubwa sana inafaa kwa kilimo. Iwe kwenye mikoa ya ukame au kwenye mikoa yenye mvua nyingi lakini inalimika na inaweza kuzalisha mazao ya kutosha. Sasa hili hatujaanza tunaongelea tu vitu vidogo vidogo vya kuendeleza. Mimi katika mkoa wangu na Wilaya yangu ya Iramba pametajwa miradi mbalimbali ambayo inaendelea katika skimu za kumwagilia. Miradi hiyo ni Masimba hekta 400, Mlandala ekta 300, Kilondatale hekta 100, Tyeme/Masagi hekta 200. Ukweli ni kuwa sijaona kilimo cha kumwagilia katika maeneo hayo. Labda katika maeneo kama Tyeme/Masagi umwagiliaji unapatikana kidogo wakati wa mvua na mvua ikikatika baada ya wiki moja kilimo kile hakiendelei tena. Sasa sijui ni kilimo gani cha kumwagilia ambacho Mheshimiwa Waziri ametuletea takwimu hizi kuwa kuna kilimo katika Wilaya ya Iramba ambacho kinaendelea. Skimu ya Kirondatali tunaambiwa hapa ni hekta 100. Mto huu wa Kirondatali kwanza kabisa ni korongo tu na kwa kuwa hakuna bwawa maji hayawezi yenyewe yakaondoka kutoka bondeni yaende kwenye vilima mashamba. Kwa hiyo, hakuna bwawa, hakuna chochote na mwaka 2001 wakati wa Bajeti Mheshimiwa Waziri aliniahidi kuwa atajaribu kuona uwezekano wa kujenga bwawa dogo katika Mto huu wa Kilondatale, lakini mpaka leo hata maandalizi hayajaanza. Lakini hapa pameandikwa kwamba kuna hekta 100. zinamwagili kwenye mashamba.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo cha kumwagilia au kilimo vijijini wahisani wengi sana hasa Taasisi za Kimataifa za fedha zinaweza zikaitikia na kutusaidia. *African Development Bank* ambayo kuna kitengo chake cha *ADF* kinatoa misaada au mikopo ya masharti nafuu sana wanaweza wakasaidia kutayarisha *road map* ya kupanga na kufanya *survey* na kupata maeneo ambayo yanafaa kwa kumwagilia katika Taifa zima. Sasa kwa nini Wizara haijapeleka maombi kwenye Benki ya Maendeleo ya Afrika kusudi itusaidie? Mradi huu au skimu hizi za kumwagilia ni skimu ambazo zitagharimu sana. Tutahitaji misaada na taasisi kama Benki ya Afrika na Benki ya Dunia zinapendelea sana miradi hii lakini tungepeleka maombi yetu nina hakika suala hili tungeanza katika mipangilio inayofaa. Sio tu kuamka kesho tunafanya hapa lakini pasipo mipangilio. Tunalohitaji ni kuwa na *strategic long term planning* katika maeneo ambayo tunaweza tukasema kuwa Wilaya hii na hii maeneo yake yanafaa katika kilimo cha kumwagilia na mahali pa kuvuna maji.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe naongelea kwa uchungu suala la kuvuna maji ya mvua kama mtaalamu ambaye nilisimamia miradi hii miaka mingi sana katika nchi mbalimbali za Afrika. Mimi baada ya kuongelea sana suala hili la kuvuna maji nimepata kuandika mradi mmoja ambao ni mradi wa kuvuna maji katika Wilaya yangu ya Iramba kwenye milima ya Sekenke. Mradi huu ambao nimekwishaupeleka tayari kwenye Wizara ya Fedha tangu mwaka jana utajumuisha kata saba. Kata ya Uruchu, Mtekente, Cheme, Mtoa, Shelui, Tuike, Tulia na Kidaru. Nusu ya Iramba kama maji yatakuwa kuvunwa kwenye milima ya Sekenke nusu ya Iramba itakuwa katika hali ya kumwagilia mashamba. Ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wajaribu kufuatilia mradi huu ambao nasikia wamekwisha upeleka tayari kuuombea msaada Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki *(ADB)*ya Nchi za Kiarabu *(BADEA)* na pia nasikia na Serikali ya Ubelgiji na Italia imeomba mradi huu. Sasa mradi kama huu unaonekana unaweza ukawa unafaa ni mahali pa kuanzia. Mimi ningeiomba Wizara ya Kilimo ione umuhimu wa kufuatilia miradi ambayo tunaitajataja katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba pia niongelee suala moja ambalo nasema kuwa sisi sio wa kwanza kubuni na kuleta mawazo ya kuvuna maji. Nchi ambazo ziko kwenye ukanda wa majangwa hazina njaa wala ukame. Sasa sisi hapa Taifa letu linapokuwa linagubikwa na matatizo ya njaa na ukame na hatuchukui hatua yoyote ya kusema kuwa miaka ijayo tujihami na matatizo haya sasa nani atatuhurumia zaidi au kujihurumia sisi wenyewe. Mimi ningeomba na ningeshauri kuwa suala la njaa sasa tuanze kulishughulikia kikamilifu. Ni fedhea kwa wananchi wetu mara kwa mara wanagubikwa na njaa kwa sababu tatizo la mvua ambalo halipo chini ya uwezo wetu lakini mvua hizi ndogo ambazo zinaonyesha ndizo tungezitumia katika kuyavuna maji yake na kuyatumia kuondoa tatizo la njaa.

Miaka mitatu mfululizo tumekuwa aidha katika Wilaya mbalimbali kuna njaa au upungufu wa chakula. Lakini sisi tunaona kuwa tumefanya vya kutosha tunapoanza kushughulika kutafuta chakula cha njaa. Suala la kutafuta chakula cha njaa hili lingekuwe labda ni *the last resort*. Kwanza ni kufanya tahadhari kwamba tatizo hili lisitokee.Mwaka huu tunajiona kuwa mvua ilikuwa ndogo mahali pengi hata mahali ambapo panakuwa na mvua nyingi hapakuwa na mvua ya kutosha.

Lakini takwimu tunazopewa hapa zinaeleza tunajitosheleza kwa chakula. Mimi sielewi kama tunapozungumzia suala hili la njaa ambalo ni la aibu sana kwani ardhi nzuri tunayo, mvua ipo kuliko hata katika nchi zingine hata nchi za jirani lakini hatujafanya vya kutosha kuhakikisha kuwa kilimo kiwe cha mazao ya chakula au ya biashara tunazalisha ya kutosha. Kilimo kiwe ni shughuli ya wakati wote sio wa msimu mmoja kubahatisha mvua. Hili suala la kubahatisha mvua hivi tunalionaje? Wakulima wetu baada ya msimu wanaweka majembe yao uvunguni, kilimo kinakuwa ni cha kujikimu. Kilimo maana yake unapovuna mara moja mwananchi atatumia na familia yake mpaka mavuno ya mwaka ujao. Sasa umaskini utapunguaje kama kweli hali kama hii inaendelea kwa sababu katika mavuno ya msimu mmoja ndiyo yatatumika kuhudumia

familia.Kilimo cha sasa at best ni kutumikia tumbo, hakuna cha ziada kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, lakini kama tungekuwa tunavuna mara mbili au tatu kwa mwaka na kilimo kiwe kama ni shughuli ya kila siku kama tunavyokuwa na shughuli za kila siku katika maduka yetu. Je, kweli tungekuwa tunasema leo tunazungumzia kuwa kuna takwimu tunazozipata kuwa mwaka 2004 mavuno mchanganyiko yalikuwa tani 13,000 ingekuwa mara tatu sio tani 39,000 kama tungevuna mara tatu. Leo Kitaifa tuna hekta zaidi ya 29 milioni ambazo zinafaa katika kilimo cha kumwagilia na leo Mheshimiwa Waziri ametuletea ekari laki 2 za skimu za umwagiliaji mashamba.

Skimu zingine ni mashamba madogo madogo ya familia moja moja lakini hekta 200,000 kwa hekta 29 milioni hivi tunaweza kujivuna tukasema kuwa tunaendelea katika kilimo cha kumwagilia? Uwezo wa kumwagulia hekta 29 milioni. Kwa sasa tumefikia 200,000. Mimi ningeona hili suala likubalike na Serikali. Wizara ya Kilimo haina uwezo ninavyoiona ni Serikali nzima itoe tamko wazi wazi kuwa tutaanzaje katika maandalizi ya kuleta mageuzi kwenye kilimo? Mageuzi maana yake ni kuanza kuvuna maji ya mvua na kumwagilia Mashamba. Pasipokuwa na maji hujalima hata ukitoa mikopo midogo midogo. Ndiyo maana mimi sizungumzii mikopo ama pembejeo kwa sababu kama utakuwa na maji ni ya msingi sana baada ya hapo mengine yanaweza yakapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeiomba bajeti hii ione umuhimu wa kuja na *long term planning and programming strategy* katika kuleta mabadiliko kwenye kilimo. Hii ndiyo itakuwa ufumbuzi wetu katika maendeleo iwe ya kiuchumi au ya kijamii kwa sababu wananchi walio wengi wamezamia katika shughuli za kilimo, lakini matokeo yake tunaona kuwa inakuwa vigumu sana kuendelea kwao kwa sababu ya matatizo ya hali ya hewa ambayo inabadilika mwaka hadi mwaka hayapo chini ya uwezo wao. Serikali iwajengee miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo.Kabla sijapigiwa kengele ya pili nasisitiza kuwa naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba aangalie suala la kuleta *Long Term Planning Strategy,* katika kuleta mapinduzi halisi katika kilimo. Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba niungane na wenzangu wote katika majonzi makubwa ambayo yametufika ya kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Margareth Bwana. Mimi alikuwa ni jirani yangu tunakaa naye kwenye msitari mmoja hapa kwa hiyo, *I can feel it.*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo ni Wizara ambayo mara nyingi sana inabeba mzigo mkubwa sana wa lawama. Kwa bahati mbaya sana Naibu Waziri wa Wizara hii huwa ukimgusa kidogo anakasirika. Hata jana tulikuwa pale nje amenuna kwamba juzi nilimsema anamwambia Mawaziri wake unaona Chegeni akisema hivi Bungeni. Namwambia Mheshimiwa tusalimiane, aah hapana, ulitusema ibaya sana Bungeni. Mheshimiwa Prof. Mbawala ndiyo kazi. Kusema, kusemwa au kukosolewa ni sehemu ya wajibu wako katika kutimiza majukumu yako vizuri zaidi. Kwa hiyo na mimi nitaanza kukusema tena leo. Lakini nakusema kwa nia nzuri tu na kukupongeza pale ambapo umefanya kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ambayo kwa kweli inastahili tuiangalie kwa mtazamo tofauti. Unaposema Wizara ya Kilimo ambayo Watanzania zaidi ya asilimia 80 wanategemea. Lakini Wizara hii leo unaipangia bajeti ya shilingi bilioni 63 eti ifanikishe majukumu yake hivi kweli si mwanzo wa kuanza kumlaumu Prof. Mbawala hapa na anachukia.

Lakini nadhani hatujakuwa *serious* upande wa kilimo. Hii Wizara fedha inazopata hazihusiani na majukumu ya Wizara hii labda vinginevyo tukubaliane ni kwamba ina majukumu mengine sera ambayo Watanzania wote wanalitegemea.

Lakini kama kuitegemea kwa majukumu hayo kwa kweli Mheshimiwa Keenja na Prof. Mbawala mtani wangu mmefanya kazi nzuri. Tunawapongeza kwa hiyo mmefanya kazi nzuri. Uwezo wenu ulikuwa ni mdogo mtafanyaje. Nchi hii ni kubwa mno na bahati nzuri Wizara hii ni Wizara ambayo ina wasomi wengi zaidi nadhani. Kuna Ma-*doctors* wengi, Ma-*reserchers* wengi kila aina wako kule ndani lakini jinsi gani wanatumika sielewi. Kwa sababu *impact on the ground* ni ndogo hatuioni pengine kwa sababu hawana uwezo, hawana *resources* ambazo wanaweza kuzitumia ku-*deploy* na kuonyesha kwamba kweli wanazitumia kikamilifu kuleta mafanikio. Sasa mtani wangu hapa bwana mimi nikisema kidogo anachukia. Profesa usichukie tukusaidie upate fedha nyingi na utimize majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, juzi juzi nilikuwa ziarani Misri. Nilipofika kule Misri wanasema hivi wao kwamba wanamtambua sana Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Kambarage Nyerere. Yeye anajulikana sana kule Misri. Pili, wanalitambua zaidi Jiji la Dar es Salaam na tatu wanasema tunaitambua sana *Simba Sports Club*. Lakini nne na hasa sasa wanasema sasa wanamtambua zaidi sana Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifungo, Mheshimiwa Edward N. Lowassa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Na Raphael vile vile?

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Ahaa sio mambo ya ushabiki Mheshimiwa Spika.

Hapa nasema ambayo nimeyasikia kule. Nasema mambo ambayo nimeyasikia kule. Kwa hiyo, kwa hili nasema kwa sababu gani wamemtambua Edward Lowassa kwa sababu ya msimamo juu ya matumizi ya maji ya Mto Nile.

Mlheshimiwa Spika, imekuwa ni *event* ambayo kwa Misri wanamkumbuka sasa hivi. Amechukua *deliberate move* na Serikali ika-*make up* vizuri zaidi, sasa ningesema hivi na sisi sasa sio Misri watambue Dar es Salaam, Mwalimu Nyerere, *Simba Sports Club* na Edward Lowassa hapana. Tutambue sasa kilimo. Tukitambue kilimo hiyo ndiyo *drive* yangu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ndugu zangu wa Bodi ya Pamba siku zote nagombana nao. Unaposema kwamba Bodi ya Pamba iko Makao Makuu Dar es Salaam,

pamba inalimwa ukanda wa magharibi. Nikimtaka leo Mkurugenzi Mkuu kwa shida yoyote ya pamba itabidi apande ndege aje Mwanza kutatua matatizo ya Bodi ya Pamba au yanayowahusu wakulima wa pamba.

Kuna maamuzi ambayo ni vyema tuyaangalie kwa nini Ofisi kama hii tusingeihamisha kutoka Dar es Salaam ikae karibu na mahali panapozalishwa pamba tupunguze gharama kwa mkulima. Mimi hainiingii vizuri tunaweza tukabaki na *Liason* ofisi Dar es Salaam pale *fine* lakini ile *centre* ofisi kubwa iwe katika ukanda ambao tunazalisha zao hili tumpunguzie gharama mkulima.

Mheshimiwa Spika, siku zote tunasema kwamba kilimo ni kipana. Lakini sasa mimi naomba nijielekeze zaidi katika kilimo cha pamba. Kwa sababu kwangu pamba ni siasa na wataalamu mtanisamehe mimi nakula kwa sababu nazungumza masuala ya pamba. Niko Bungeni kwa sababu nawakilisha *interests* za wakulima wangu na wapiga kura wangu kwa sababu ya pamba. Mwanri atazungumzia kahawa kwa sababu wakulima wake wanalima kahawa. Mimi nitazungumzia pamba. Katika hili mkulima wa pamba bado hajasaidiwa vya kutosha kila mwaka yeye yuko taabani tu. Analima pamba vizuri sana Msukuma huyu lakini ikifika wakati wa kuuza pamba unaambiwa mara bei imeshuka, anaambiwa mara utakopwa, mara pembejeo utaletewa hapati kwa muda unaotakiwa na kadhalika.

Sasa hayo matatizo madogo madogo tungependa yaboreshwe. Nyinyi mnaohusika na mambo kama haya muyaboreshe. Hivi mkulima anapoanza kulima anahitaji pembejeo kama madawa ya kuulia wadudu hayapati kwa muda unaotakiwa. Anapewa pasi na anaambiwa kwamba sasa unapouza pamba yako tunakukata fedha fulani ziongezwe kwenye kitabu chako. Ikifika muda wa kutaka kumlipa ile fedha apate pembejeo hawezi kupata.

Mheshimiwa Spika, sasa mkulima siku zote awe ni mtu wa kusumbuka tu. Anasumbuka sumbuka ningeiomba haya Mheshimiwa Keenja wakati ulipokuwa Tume ya Jiji kazi yako ilionekana pale Dar es Salaam. Najua Ubungo hakuna wakulima wa pamba, lakini kule kwangu kuna wakulima wa pamba. Ebu ona namna gani tuwasaidie wakulima wa pamba ili wauondoe umaskini walio nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kinga la bei ya pamba. Sote tunajua kwamba bei ya pamba katika soko la dunia inabadilika kila wakati. Inabadilika badilika lakini mkulima huyu hana kinga yoyote ile ya mazao yake. Kwa nini huu mkakati wa kupata kinga ya bei ya mazao tusiuweke bayana ili mkulima anapolima pamba yake ajue mwaka huu nitalima pamba yangu kama ni kwa shilingi 300/= nitauza kwa shilingi 300/= *short of that* atafidiwa na mfuko ule.

Lakini bei ya pamba sasa hivi ni shilingi 230/= wakati mkulima alipolima pamba alijua atauza angalau kwa shilingi zaidi ya 300 sasa yote hii ni matatizo. Ukiangalia kuna mlolongo mkubwa sana wa makato. Kuna Mfuko wa Uendelezaji wa Zao la Pamba *CDF* anakatwa shilingi 21/=, Mfuko wa Elimu shilingi 7 na kitu, Halmashauri ya Wilaya inakata shilingi 13/= Bodi shilingi 7/50, kuna ile *Association* ni shilingi 2/50 yote hiyo

inaingia kwenye bei ambayo mkulima ameiuzia pamba yake. Hayo ni makato sasa karibu shilingi 60 hapa zinapungua kwa sababu ya makato. Mimi ningeshauri sana tujaribu kuangalia namna gani kuweza kumsaidia mkulima kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine *very funny* ni kwamba, kuna hii fedha ya ruzuku ya usafirishaji wa mbolea. Mwaka huu tumetenga Shilingi bilioni 7.2, inakwenda Mikoa ambayo inapata mbolea. Lakini Mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga na Kagera tunatumia mbolea ya samadi au ya wanyama tunaowafuga. Sasa kwanini wakulima hawa na wenyewe wasipate angalau fungu fulani liwasaidie kusomba ile mbolea kutoka majumbani kwao na kupeleka mashambani kwao? Kama wengine wanapata ruzuku na wenyewe wapate ruzuku ya namna hiyo, wasombe kutoka majumbani kwao wapeleke mashambani si ni ruzuku jamani!

Mheshimiwa Spika, ningeomba hili suala, Mheshimiwa aliangalie, hizi pesa zinavyokwenda wanafaidika upande mmoja tu na sisi tunalima vilevile. Lakini kingine cha zaidi ni kwamba anayeingiza mbolea ndiyo anayepeleka mpaka kule kwa wakulima, sasa sielewi *control* ziko wapi. Huyu bwana akiingiza makaratasi akapeleka halafu akarudi akapata ruzuku hiyo, inakuwaje? *Where are checks and balances?* Ziko wapi?

Mimi nashawishika kusema kwamba kuna baadhi ya Mashirika kama lile la *RTC* Dar es Salaam, wanajitahidi sana na nampongeza Mheshimiwa Keenja, kuna wakati aliamua kuwapatia kazi maalum, nilifurahi nilipofika pale wanafanya kazi moja nzuri sana. Ni Shirika tu la watu wafanyakazi wameji- *mobilize* vizuri lakini wanaliendesha. Tuwasaidie, wale wanapofanya biashara tunaamini hela inabaki hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengine wanafanya biashara *at the end of the day* hela inahama nje ya nchi. Sasa hawa watu wanavyowapendelea, mimi naona kuna haja ya kuangalia, ni sawa sawa na Benki. Mimi ukisema kwamba mnaipa *EXIM Bank* Mfuko mkubwa zaidi wa ku-*manage* wakulima mkaacha *CRDB*, hizo *logistic* sizielewi vizuri. *(Makofi)*

Mimi ningeamani bora kuisaidia *CRDB* ambayo tunaamini kwamba tuna hisa mle ndani na tuna *interest* yetu humo ndani. Hali ya *EXIM Bank* mimi sielewi, ukienda hata kuomba mkopo pale, bwana kama huna rangi fulani huwezi ukapatata mkopo. Sasa hizi Benki ambazo bado zinakuwa zina zile *sentiments* hazitufai kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu bado Serikali inawekeza pesa nyingi kule, pesa yetu ya Walipakodi inawekezwa kule. Tuzipe Benki ambazo kweli zinakuwa na mtandao wa kuwasaidia watu ambao kweli wanahusika na pesa hizi. Lakini bado naipongeza Wizara ya Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Keenja na Mheshimiwa Profesa Mbawala nawapongeza kwa mradi wa umwagiliaji wa Kalemela katika Jimboni langu. Hapo nawapongeza kwa kweli. Nilisema nitasema mabaya lakini nitawapongeza vilivile, isipokuwa sasa pale Kalemela na pale Mwamanyili, miradi imeanza lakini haijakamilika, miaka miwili imepita sasa.

Hebu sasa sukuma basi na mimi nichekelee, sasa miradi imeanzishwa lakini haijakamilika mpaka leo hii, tunapoongea hapa tuongee kwa lugha inayostahili na Wataalam wakisikiliza kule. Naomba msaidie miradi ikamilike. Mradi ule wa Kalemela tumejenga *tank*, tumeweka *infrastructure*, nyingine za mabomba lakini mpaka leo hii haujakamilika, *simply windmill* haijapatikana. Sasa hii tunaanzisha miradi, inakuwa kama *white elephant* inakaa pale tu, matokeo yake haiwasaidii hata wananchi na sisi tunataka tumwagilie, tuvune mpunga wetu vizuri zaidi. Ndiyo ukanda wenye neema kwa sababu Ukanda wa Ziwa, tunataka tufanye *green belt*, sasa miaka miwili mitatu inapita sasa hivi tunasema hadithi tu. Hakuna ambacho kimeshatekelezwa kwamba kinaonekana sasa kimeshaanza.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Keenja katika Bajeti hii atusaidie kutekeleza mara moja miradi hii; Mradi wa kumwagilia maji Mwamanyili na pale Kalemela au Lukungu, ili sasa tunaposema *green belt* katika Kanda ya Ziwa, basi tuone tumeanza. Kuna miradi ya kule Nyatwali, kwa Mheshimiwa Tembe Nyaburi, kuna miradi ya pale Magu, tuikamilishe ile ili Ukanda ule uweze sasa kuwa kamili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya, bado ningependa tu kusema kwamba, Wizara hii imefanya kazi kwa mazingira magumu, lakini tukubaliane kwamba kama hatuwapi pesa, kweli itakuwa ni kitendawili. Ningeshauri kwamba, katika pesa ambayo tutakuwa tumesamehewa madeni, hatulipi pesa, hebu tujaribu kuchukua mkakati wa makusudi kabisa tuwekeze katika kilimo, hii pesa tuiweke katika kilimo na kuweza kuandaa miundombinu ambayo ingesaidia kilimo sasa kiweze kuwa na matokeo mazuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi, utakuta kuna wimbi kubwa sana la watu wanaanza kuona kilimo hakina faida. Lakini nchi yetu ina raslimali kubwa sana ya ardhi na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, hapa yupo anathibitisha hili kwamba nchi hii ndiyo ina ardhi nzuri yenye rutuba na bado inaweza ikafanya kilimo kizuri kabisa. Ni aibu kwa Tanzania kuwa na njaa, ni fedheha na ni aibu kubwa sana, eti tunakwenda kutafuta chakula Kenya na Waziri anasema nilikwenda kutafuta chakula Kenya. Hivi kweli Tanzania iuziwe chakula na Kenya kweli!

Mheshimiwa Spika, hii nadhani ni kutokuwa na mpangilio mzuri tu, ningeomba sana sana tujaribu kuweka mkakati na kuiomba Serikali tuelekeze fedha nyingi upande wa kilimo, hawa Mawaziri wamefanya kazi yao nzuri na Wataalam wao lakini tuwaongezee fedha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kwa Waziri wa Ushirika na Masoko. Bahati nzuri Mheshimiwa George Kahama yupo ni shemeji yangu, lakini nitakusema kidogo, Wizara ya Ushirika na Masoko kwa sababu wana uhusiano wa karibu sana na Kilimo, hauwezi ukamsema wa Kilimo usimseme wa Ushirika na Masoko.

Tunaomba hii dhana ya bei ya mazao ya wakulima, kuwe na *indication* basi, mkulima anapolima ajue kwamba mazao yetu tutayauza kwa namna hii. Angalau tuwe

tunatangaza bei hizo ambazo zitawasaidia wakulima zaidi, wajulishwe kwamba wanapolima zao fulani, lina faida hii, linauzwa kwa bei hii. Wakulima hawajui haya.

Mheshimiwa Spika, kuna mitandao mingi, kuna Redio, kuna *TV* mpaka Vijijini siku hizi wanasikiliza na wanaona. Hebu tujaribu kuwa na programu zinazoweza kuwasaidia wakulima wajue mwenendo wa bei za mazao. Itasaidia sana mara kwa mara kuweza kufanya wakulima wachague kwamba leo nalima nini na nitapata nini katika zao hili.

Meshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda tena niunge mkono hoja hii na kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na kwamba si kwamba tunawasema kwa nia mbaya, hapana. Tunawesema kwa nia njema ili kuboresha shughuli zao na Mheshimiwa Mbawala mtani wangu, usiwe unakasirika kasirika unaposemwa, ndiyo majukumu hayo Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono hoja hii *(Makofi)*

**MHE: KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Lakini niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa wa Marehemu, Mheshimiwa Margareth Bwana na Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Waziri wa Kilimo na Chakula, lakini pia na Naibu wake na Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote kwa kukamilisha hoja hii ya Makadirio ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa uzuri na imezingatia mambo ya msingi kabisa. Narudia, nasema nawapa hongera sana kwa kazi nzuri waliyoifanya na ndiyo maana na sisi tumepata mambo ya kuchangia zaidi na kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza zaidi katika suala hili muhimu la kilimo na katika kujielekeza katika suala hili la kilimo nimechagua *points* za muhimu ambazo ningependa Serikali izingatie ziko *points* zinazoimarisha kilimo, lakini pia zipo *points* ambazo ni kikwazo cha kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, *point* ya kwanza, naomba kilimo kikue kwa asilimia 8.5 mpaka asilimia 10 ndicho kinaweza kikachangia mambo muhimu yafuatayo:- Lakini chini ya hapo, kinyume cha hapo tutaendelea kuzungumza habari ya kilimo na uchumi wetu hautasimama imara. Jambo la kwanza kwa kuimarisha kilimo katika asilimia hiyo 8.5 mpaka 10 tutaondoa umaskini kwa uhakika. Tumeanzisha MKUKUTA na vitu vingine, lakini msingi wake hasa ni kilimo.

Lakini jambo la pili, kitakuwa kimekuza uchumi kwa kiwango cha juu zaidi. Kwa sababu sekta zote pia zinategemea kilimo, lakini pia tutakuwa tumeharakisha maendeleo ya watu na hasa wa Vijijini na wa Mijini na pia kitaondoa njaa katika nchi hii. Hayo ni mambo ya msingi sana.

Kwa hiyo, kilimo kisimamiwe kikue kwa haraka kwa asilimia hizo na kuendelea badala ya asilimia sita.

Mheshimiwa Spika, *point* ya pili, ili kilimo kikue kwa kasi kubwa kinahitaji lazima kipatiwe mahitaji muhimu yafuatayo:- maana huwezi kuzungumza tu habari ya kilimo bila kuwa na mahitaji yake muhimu. Hitaji la kwanza ni pembejeo makini na zinazopatikana kwa muda muafaka. Kilimo bora ni pembejeo, kama hakuna pembejeo hakuna kilimo bora.

Kwa hiyo, naomba suala hili lizingatiwe sana na Serikali. Lakini pia zana za kileo za kilimo, zana za kisayansi, sio zana zile za kutumia mitulinga. Hizo zana za kisayansi ndizo ambazo zitaimarisha na kukuza kilimo na kiweze kuleta tija na maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini sehemu nyingine ni utaalam wa ugani ulioko karibu na wananchi. Wataalam wa ugani walio wengi huko wanafanya shughuli zao tu, hawapo karibu na wananchi. Kwa hiyo, wananchi kilimo hiki tunachokiona na uchumi huu tunaoujenga unajengwa kwa taabu, kwa jasho la wananchi wanyonge bila utaalam wowote. Kwa hiyo, tunaomba hao Wataalam wa ugani wawe karibu na wananchi wawasaidie. Wakifanya hivyo tutapiga hatua, lakini pia lazima kuwe na uwekezaji wa masoko ya uhakika nje na hata ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mkulima anapolima, anakuwa na uhakika kwamba atauza ndani ya nchi hata akitaka nje ya nchi atauza. Kwa misingi hiyo, ndio tutakuza kilimo, kitaendelea kukua, lakini pia nguvu kazi mpya ya vijana ambayo ndio tegemeo kubwa tunaitumiaje? Hapo ni suala la msingi kweli kweli! Vijana wetu walio wengi kabisa kwa sababu hakuna sayansi inayotumika katika kilimo, hakuna zana za kisasa wanatoroka wanakwenda Mijini. *(Makofi)*

Kwa hiyo tuwawezeshe kwa njia mbalimbali, aidha mitaji na zana za kisasa za kuzalishia mali. Tukifanya hivyo, vijana wetu watatulia na watachangia katika kilimo, tutafanikiwa na uchumi utakua. *Program* zote katika Wizara mbalimbali vile vile zilenge vijana, vijana hao ndio wachumi, vijana hao ndio watakaoondoa umaskini na kuondoa njaa nchini. Kwa hiyo, tuhakikishe kabisa tunakuwa karibu nao ili tuweze kuwatumia kwa ajili ya kilimo cha kisasa chenye zana za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *point* yangu ya tatu kilimo chetu kina vikwazo vingi ambavyo sharti Serikali iviondoe. Kama Serikali haiwezi kuondoa hivyo vikwazo hatutapiga hatua kubwa katika kilimo. Kikwazo cha kwanza na kilimo chenye misingi ya ujima kiondolewe kabisa, yaani tuwe na kilimo cha kisasa sio kile cha ujima, jembe lile la mkono na vitu vingine hatuwezi kufika mbali.

Tanzania watu wanaongezeka, kilimo kinazidi kudidimia, hicho cha ujima hakitatufikisha mbali. Hicho ni kikwazo cha kilimo katika nchi yetu, kiondolewe! Waziri Keenja na mwenzie ni makini kabisa, wanaweza wakaweka mikakati ya kuondoa hicho ili wananchi watumie jembe la kukokotwa na ng'ombe, matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia zana za kilimo zenye msingi wa mitulinga lazima ziondolewe kabisa, zifutwe! Haziwezi kutufikisha mbali. Lakini jambo lingine ni kwamba wananchi wetu ambao wanajenga uchumi ni wale ambao wana mashamba madogo madogo, mashamba makubwa ni machache. Lakini haya mashamba madogo, basi yajengewe hoja yalimwe kwa misingi ya kanuni za kilimo na waweze kupata pembejeo ili wazalishe zaidi katika maeneo yale.

Lakini pia, vijana wetu kama nilivyoeleza ambao ni zaidi ya asilimia 75, wapo zaidi ya milioni tatu ambao wana nguvu, hawa tuwalenge, tuwabane ili tushirikiane nao waweze kuingia katika eneo la kilimo. Eneo la kilimo linaendelea kubaki tu na watu wazee na kadhalika, vijana hawajashiriki vizuri kwa sababu hakuna zana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikwazo kingine ni kile cha barabara mbovu Vijijini ambazo hazichochei kabisa wananchi kulima kwa sababu watasafirishaje ama watasafiri vipi wao? Kwa hiyo, tunaomba Serikali iondoe kikwazo hiki cha barabara mbovu Vijijini zitengenezwe katika mkakati huu wa MKUKUTA, basi suala la barabara za Vijijini lizingatiwe. *(Makofi)*

Barabara za Vijijini zikiwa bora, wananchi watavutika kabisa katika suala la kilimo na uzalishaji utaongezeka. Lakini pia uwekezaji katika kusindika, wananchi wanakata tamaa kwa sababu mazao yao wanayauza yakiwa hivyo hivyo. Mazao yanatakiwa yauzwe yakiwa yamesindikwa huko Vijijini. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye hivyo, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeimarisha kilimo chetu na tutakuza uchumi wetu.

Kwa hiyo, Serikali iwejibike basi kuweka mikakati ambayo itaondoa vikwazo hivyo na kilimo kipewe fedha nyingi zaidi kama walivyosema wenzangu. Fedha zilizotengwa katika Wizara hii ni chache, kama ningekuwa ni mimi ningetoa fedha za

kutosha kabisa kwa sababu ndio kiini cha maendeleo yetu hapa katika kilimo. Lakini pia wakulima Vijijini, kwa kweli lazima tuwaangalie tumewaambia tu walime lakini hatupo karibu nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *point* ya nne, nizungumzie kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Kule Kondoa katika Jimbo la Kondoa Kaskazini ziko *scheme* za umwagiliaji ambazo zinahitaji kuboreshwa zaidi, kukarabatiwa zaidi, zikiachwa hivyo zitachakaa na hazitaleta ufanisi hata kidogo. *Scheme* ya kwanza iko Kikoye katika Kata ya Kikole ni ya siku nyingi inahitaji kuboreshwa ili hata maeneo yale ya kumwagilia yaongezeke.

Scheme nyingine ya Mnenia halikadhalika inahitaji kuboreshwa ili maeneo ya uzalishaji yaongezeke. Lakini pia eneo la Hurui, *scheme* ya Huruhi ambayo iko katika Kata ya Kikoye nayo inahitajika kukarabatiwa na kuboreshwa ili maeneo yale ya uzalishaji yaongezeke na kule kwa madebe katika Kata ya Sawi panahitaji uboreshaji.

Lakini pia kuna mradi mpya wa Kisese ambao bado haujakamilika. Naibu Waziri anajua kwa sababu amefika mara nyingi sana kule, mradi huo bado haujakamilika. Huo unatakiwa ukamilike, wadau wake ni Vijiji vinne; Kijiji cha Mapinduzi, Sauna, Madisa na Disa hekta nyingi kabisa. Sasa tunaomba huu mradi ukamilike. Hizi *scheme* zikiimarishwa zitazalisha. Kwa sababu tumepania kuondoa umaskini, sasa kuondoa umaskini kwa kupitia umwagiliaji ni rahisi zaidi kwa sababu kilimo kitakuwa cha muda wote.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kama nilivyoeleza kwamba kule Kisese kuna mradi huu mpya ambao haujakamilika na ninashangaa kwa nini unachelewa. Naomba ukamilishwe haraka kabisa. Wapo wananchi waliofanya kazi pale walikuwa wameajiriwa katika shughuli mbalimbali wakati wanajenga *tank.* Wakati wanajenga *tank* wanadai zaidi ya Shilingi milioni sita, Serikali ipeleke fedha ili walipwe. Tena kila siku wananisumbua, hata jana na niliwaambia nikipata nafasi nitakumbusha Serikali kuwaombea, maana wenyewe hawawezi kuja wote kuomba.

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri hili lifuatiliwe na wataalam nafikiri wanajua, kule fedha hizi zipelekwe na mradi huo ukamilike.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie habari ya mpango wa mikopo. Mikopo ya matrekta kama walivyoeleza wenzangu, kule Kondoa kuna watu wamehitaji sana matrekta, lakini mpaka leo hawajapewa, wametimiza masharti yote wanazungushwa tu. Msimu umekwisha, sasa sijui watalima nini? Huo MKUKUTA tunaouhimiza sijui utatengenezwa!, Utafanywa na nani? Hao ndio tunataka wachangie ili tuondokane na tatizo hili.

Kwa hiyo tunaomba sana, nini hasa kinafanya kuchelewa? Kama wana mashaka na mali yake, waende waangalie nyumba, hati na kadhalika watoe mkopo ili wachangie kilimo haraka. Kwa hiyo, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, yako mabonde ambayo ningependa yakafanyiwe utafiti. Liko Bonde la Mto Bubu katika Kijiji cha Munguri na Mungoroma lifanyiwe utafiti ili tuweze kufanya kazi ya kumwagilia pale. Lakini liko Bonde vile vile la Mto Bubu katika Kijiji cha Berebera lifanyiwe utafiti ili tuweze kumwagilia. Bonde lingine ni la Kingale katika Kijiji cha Kingale nalo lifanyiwe utafiti tulime. Shabaha yetu ni ile kubwa ya kuondoa umaskini kupitia MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, lakini nasema kwamba naunga mkono hoja, sina tatizo. Lakini naomba yale niliyosema yazingatiwe ili yafanyiwe kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kukupongeza sana kwamba kwa miaka hii ambayo tumekuwa wote hapa Bungeni umeweza kuendesha vizuri Bunge letu kwa umahiri. Nami nakuombea Mwenyezi Mungu akurudishe na ushinde kwa kishindo cha kimbunga. Mimi nataka nikuhakikishie kwamba nitakuwa Kampeni Meneja wako, nimejitolea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nianze kwa kutoa pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge mwenzetu ambaye ametutoka jana. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Sasa nianze kwa kupongeza Wizara ya Kilimo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Charles Keenja pamoja na Mheshimiwa Mbawala pamoja na wataalam wote. Kwa kweli, kazi wameifanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini nianze tu kwa kusema kwamba niulize swali moja tu na lazima swali hili tujiulize siku zote kwamba kwa nini Tanzania bado maskini miaka 40 baada ya uhuru? Nchi yetu tuliamua kuweka kilimo kiwe ndiyo uti wa mgongo, lakini nafikiri hili nalo ni sababu mojawapo ambayo imetufanya tukaendelea kuwa maskini. Sasa tungeamua tukasema kwamba kilimo sasa kiwe uso wa maendeleo yetu ili kiwe kinaonekana kwa sababu kimesahaulika kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, leo pesa ambayo kwa kweli wamepata wenzetu wa Kilimo ni ndogo sana, haitatosha. Kwa hiyo, ningefikiri, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Fedha yupo hapa, aangalie kama tutaendelea kusamehewa, basi Mheshimiwa Keenja akileta hesabu zake nyingine tumfikirie ili aendeshe kilimo, kwa sababu lawama zote

zinakwenda kwenye Wizara ya Kilimo, maana Wizara ya kilimo ndiyo ambayo tunaitegemea.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba mkulima hawezi kutoka kwenye lindi la umaskini pasipo kutumia kilimo cha kisasa kikiwemo kilimo cha umwagiliaji. Lakini mkulima mdogo ataweza vipi kulima kilimo cha kisasa kama hawezi hata kupata mkopo? Kama gharama za kununua jembe la mkono tu yeye inakuwa ni tatizo, atawezaje kumudu gharama ya kununua jembe la kukokotwa kwa ng'ombe? Kwa hiyo, mimi nafikiri suala la kuanzisha Benki ya mkulima, inaweza kuwa ndiyo ukombozi mkubwa. Kwa sababu leo hii ukienda kukopa pesa, unatakiwa urejeshe baada ya mwaka mmoja. Sasa kilimo kwa mwaka mmoja huwezi kurejesha. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Benki hiyo ikaanza mapema ili itusaidie kuboresha kilimo.

Leo tunaingia kwenye karne ya 21 ya Sayansi na teknolojia kwa jembe la mkono, ni aibu. Kama walivyozungumza Wabunge wenzangu kwamba katika Wizara yenye wasomi wazuri, basi Wizara ya Kilimo inaongoza. Sasa kitu cha kufanya leo hii ungekwenda Kilolo, ukakae na watu wa Kilolo hawa ambao tunawajadili kwa sababu hao wakulima ambao tunawajadili wako kule Vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaojadili tuko sisi ambao tunakaa huku Mjini. Lakini ukikaa na mtu wa Kijijini, kwa mfano mtu wa kule Kilolo ukamwambia, tuambie kwa nini tuko maskini? Angekwambia kwamba cha kwanza ambacho tunatakiwa tufanye, tuboreshe barabara, kwa sababu leo hii mbolea ile ambayo Mheshimiwa Keenja alituuzia kwa ruzuku ni kwamba mazao yamelimwa lakini yameshindwa kufikishwa Sokoni, yameshindwa kufikishwa hata Kata nyingine, kwa sababu barabara hakuna. Sasa sisi tungeweza kupanga mipango mizuri, Wizara ya Kilimo na hizo pesa ambazo mmepata tukaboresha zile barabara za Vijijini, tukafumba macho, baada ya mwaka mmoja pato la Serikali lingekua, kwa sababu yule mkulima angeweza moja kwa moja kufikisha mazao yake kutoka shambani kwenda Sokoni.

Mheshimiwa Spika, mazao yakishafika Sokoni, Keenja ameshamaliza kazi yake, tunakwenda kwa Mheshimiwa Sir George Kahama kwamba soko vipi sasa! Tungeboresha soko. Lakini sasa hivi tunakamatakamata hapa hapa na ukiangalia tunakwenda kama kisiasa, kwamba lazima tupeleke ruzuku kwa Mheshimiwa Chibulunje, lazima tupeleke ruzuku kwa Mwanri bila kuangalia kitu gani wananchi wanataka.

Mheshimiwa Spika, sisi kule Kilolo, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliahidi kwamba yuko tayari, sisi ambao tumepata Wilaya mpya tukae chini tuangalie jinsi ambavyo wanaweza kutusaidia kwenye mpango wa barabara. Mimi nafikiri boresheni barabara, kilimo kitakwenda tu.

Mheshimiwa, ninapozungumza sasa hivi kuna baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Kilolo, Mahenge, Ruaha Mbuyuni, tunategemea kupata njaa kubwa sana. Sasa ni kitu cha aibu wakati sehemu nyingine Wilaya ya Kilolo mazao yanaharibika kwa kukosa

kufikishwa sehemu ambayo yanatakiwa. Nafikiri tuangalie uwezekanao wa kuona tutafikaje.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa nizungumze ni suala hili la wataalam na wanasiasa kuingiliana. Sisi wanasiasa tukizungumza kisiasa, wataalam mara nyingi wanatuelewa na wataalam wakizungumza kitaalam, sisi wanasiasa tunawaelewa. Lakini mtaalam akianza kuingiza siasa, ndipo tatizo linapoanza kutokea na sisi wanasiasa tukianza kuingiza utaalam ndipo tatizo linapotokea.

Kwa hiyo, mimi ningefikiri wataalam mambo ya siasa mtuachie na sisi mambo ya utaalam tutawaachia ili twende mbele. Bila kufanya hivyo, wataalam wanaweza wakaanza kumlaumu Mheshimiwa Keenja, wakamlaumu Mbawala bure, wakamlaumu Mwamoto, lakini wewe fanya kazi yako kiutalaam. Si umesomea! Fanya kiutaalam.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie kwamba kuna wataalam ambao hawajakwenda Shule kabisa lakini ni wataalam Vijijini kule. Kama wale wangesikilizwa, mambo mengi sana yangeweza kwenda. Hawajasoma lakini wana utaalam wa kujua mambo mengi sana. Sasa mimi ningewashauri wataalam msiwadharau wale, mkipata nafasi mzungumze nao. Hawezi kuharibu utaalam wake! Zungumza naye utapata faida kubwa kuliko kuweka malumbano mbele.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli niwashukuru sana Wizara ya Kilimo, nimshukuru sana Mheshimiwa Keenja na Wizara yake kwa ujumla kwamba tulipiga kelele sana kuhusu suala la kilimo cha umwagiliaji kwenye maeneo ya Nyanzwa, Ilindi, Magana na Ruaha Mbuyuni. Ile miradi imekamilika na wananchi wameishaanza kuona manufaa yake.

Lakini tatizo ambalo lipo mpaka sasa hivi ni kwamba mimi nafikiri kwa sababu ile miradi haijafunguliwa na kabla ya kufunguliwa Mheshimiwa Keenja alishaniambia kwamba yuko tayari kufungua kabla hatujaaga Bunge, wataalam waende wakaangalie ile miradi imetumia fedha nyingi sana. Kuna matatizo madogo madogo sana ya mifereji ambayo yanaweza kuharibu maana nzima ya miradi ile ambayo imegharimu fedha nyingi. Kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri atume wataalam waende kwa sababu uharibifu unaoweza kutokea ni mkubwa na kuna watu ambao wameng’ang’ania kwenye vyanzo vya maji yale ambayo yanakwenda kwenye ile mifereji. Sasa kwa kupitia Wizara hii, ukiwaagiza watu wake Mikoani kule Iringa watusaidie ili tuweze kuwaondoa wale watu ambao wameng’ang’ania kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la mbolea. Suala la ruzuku ya mbolea ni suala zuri sana, lakini sasa tatizo ambalo lipo kuna baadhi ya mbolea ambayo ruzuku yake haijapungua sana, wala haijaondolewa. Kwa mfano *CAN*, kule kwetu kuna maeneo ya ukanda wa nyanda za juu na ukanda wa nyanda za chini. Kwa hiyo, utakuta mbolea iliyoondolewa ruzuku ni ile ambayo wa nyanda za juu wanalima kwa mfano *DAP* na *UREA*. Kwa hiyo, kwa sababu Bajeti imeshapita, siyo rahisi kupunguza lakini sisi tungefikiri mngefanya *balance* tu kwamba kwenye ile mbole ya *NPK* na *CAN*

mkapunguza asilimia angalau 25, wenye *UREA* asilimia 75 mambo yaka-*balance* nao wakapata kidogo ahueni.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ni ngependa kuzungumza ni suala la shamba la chai Dabaga. Mimi naomba Mheshimwa Waziri atusaidie, bahati nzuri pia yeye ni mpigakura wangu kule Kilolo kwa sababu kuna shamba ambalo analima.

Sasa ungetusaidia Mheshimiwa kuhakikisha kwamba lile shamba la Dabaga linabinafsishwa vizuri kwa sababu sasa hivi ni muda mrefu na wananchi wamekata tamaa. Wako tayari sasa hivi wanangoja wapate uhakika kutoka kwenye hii Bajeti kwamba ile miche waifyeke wafanye kitu kingine, kwa sababu sasa hivi ni karibu miaka minne wananchi hawaoni maendeleo ya kile kiwanda. Ulikipeleka kikabinafsishwe, lakini hakuna chochote kilichoendelea. Tumehamasisha watu wamelima chai, mimi ni mmojawapo na ninalima chai pale, kuna wakulima wadogo wadogo, lakini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa, ningekuomba sana ulizungumze hilo kwa kina, kwa sababu mimi nina hakika kabisa ukiamua kutokugombea kule Ubungo, baada ya miaka 10 ijayo unaweza kuja kule Kilolo watu wakakupa kura kwa sababu wanakufahamu. Kwa hiyo, ningeomba ulishughulike hilo ili utakapokuja, basi uweze kulizungumza kwamba na wewe ulilifanyia kazi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ambalo ningependa kulizungumza ni suala la masoko. Nirudie tena, “masoko,” kwamba kuna mazao ambayo yanalimwa kule Kilolo, lakini bado hayana soko la kutosha. Kwa mfano paplika, tungeomba utusaidie kuhakikisha kwamba unapozungumza na Mheshimiwa Waziri wa Masoko ili tuwe na soko la uhakika kwa sababu waliopo pale wanaonunua kwa kweli ni tofauti na jinsi walivyotueleza. Wakulima wanalima, lakini yale mazao yanaharibika yakiwa mikononi mwao. Kwa hiyo, hiyo nayo ni tatizo.

Mwisho, naomba niunge mkono hoja na kuomba uongezewe tena Bajeti yako. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, napenda nikushukuru sana kwa nafasi hii na kwa kweli napenda nieleze masikitiko yangu makubwa na majonzi makubwa kwa kifo cha Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Margareth Bwana. Nilikuwa nasoma hotuba yake aliyoitoa hapa mwisho kama ilivyoandikwa kwenye Gazeti la Mwananchi na kuona kuwa alikuwa na ari kubwa naye apate nafasi ya kwenda kwenye eneo lake la uchaguzi agombee ili aweze kurudi kwenye Bunge lijalo. Hivyo, tumwombe Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema Peponi na kwamba maneno yake aliyosema hapa hayakwenda bure.

Mheshimiwa Spika, pia napenda niipongeze sana Serikali; kwa kweli zamu hii Bajeti ni kubwa. Mimi nimeona watu wanasema Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula ni ndogo. Nimekuwa nafuatilia Bajeti za Wizara ya Kilimo na Chakula kwa karibu sana. Mwaka huu Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula, kama alivyosema hapa Mheshimiwa Mtoa Hoja kwamba leo alikuwa anaomba aidhinishiwe Shilingi bilioni 118. Kwa hiyo, Bajeti hii ni kubwa sana. Mkitaka kujua ukubwa wake, mnaweza kufikiria Mashirika makubwa kama *UNESCO*, Bajeti yake ya mwaka kama ni Shilingi bilioni 250, Bajeti inayoshughulikia dunia nzima. Sasa hii Bajeti ya Wizara ni karibu nusu hivi ya *UNESCO*. Sasa hii ni Wizara moja tu! Hivyo hii Bajeti kubwa kinachotakiwa hapa ni ni usimamizi mzuri ili itoe matokeo. Hii ndiyo inayotakiwa, lakini Bajeti hii ni kubwa kweli kweli. (*Makofi*)

Mwaka jana, Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula ilikuwa kama Shilingi bilioni 64 na Bajeti ya maendeleo ilikuwa kama Shilingi bilioni 32. Mwaka huu Bajeti ya Maendeleo peke yake ni Shilingi bilioni 64.5, hii ni Bajeti kubwa sana. Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba ndugu zangu hebu tuchangie tuone kwa jinsi gani tunaweza kupata mafanikio kwenye kazi kubwa hii ambayo imefanya na Serikali. Kama Serikali imefanya kazi hii kubwa mpaka wakaruka kutoka Shilingi bilioni 64 mwaka jana 2004 na kufika mara mbili yake mwaka huu 2005, kwa kweli hii si haba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri - Profesa Pius Mbawala. Mheshimiwa Profesa hongera. Nilimsikia rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Chegeni akisema ulichukia jana. Pole Profesa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwapongeze sana wataalam wa Wizara ya Kilimo na Chakula, chini ya Katibu Mkuu Wilfred Ngirwa. Wakati ninapowapongeza, napenda niwashukuru sana kwa juhudi kubwa waliyofanya ya kujaribu kulianzisha zao la viazi mviringo katika Jimbo langu la uchaguzi. Katika mwaka 2003/2004 walipeleka wataalam kule ili waweze kuangalia uwezekano wa kuanzisha zao la viazi mviringo katika Jimbo la Mwanga. Wakaenda kule mlimani wakakuta panafaa, kama kuna maji ya umwagiliaji na wakapeleka mbegu kule mwaka jana 2004. Lakini mbegu ile ikakutana na uhaba wa mvua na viazi vilipozalishwa ilifanya vizuri sana wakati wa njaa ikawa chakula. Maana wakati wa njaa unakula kila kitu. *(Makofi)*

Nikawaomba tena kwamba watusaidie mbegu tani tano ili tuweze kupanda katika vuli ya mwaka huu, bahati mbaya na wenyewe walikuwa na uhaba wakatupatia tani moja. Mbegu ile imezalishwa lakini kama mnavyojua katika eneo lile kumekuwa na uhaba mkubwa wa chakula kwa sababu ya ukame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawaomba kwa dhati kabisa maana mwaka huu kuna ahueni kidogo, hebu wafanye juhudi kabisa na walichukulie kama suala la Wizara, watusaidie kuanzisha mazao haya ili yashike yawe sehemu ya kilimo cha eneo lile. Viazi mviringo, mpunga, nitaelezea baadaye kwa nini ninaomba mpunga uwe zao kule, paprika, fiwi, mikunde na mazao mengine ambayo ninyi wataalam mnajua zaidi ya sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukame umeikumba Wilaya ya Mwanga kwa zaidi ya miaka mitano mfululizo sasa. Wananchi wamekuwa wanajaribu kulima mahindi na hayakuwezekana. Kumekuwa na nguvu ya kusukuma hata muhogo. Lakini nilikuwa nataka nishauri kwa kitaalam kwamba muhogo ni zao la maeneo yenye mvua nyingi. Muhogo wenyewe ukikua kwenye eneo lenye mvua nyingi ni mzuri kwa kula kwa sababu hauwi na sumu. Lakini katika maeneo ambayo mvua ni kidogo ule muhogo (*tuber*) unakusanya sumu nyingi ya *cyanogenic glucocide* ambayo siku moja Waziri wa Afya alitoa athari ambazo ziliwapata wananchi wa Wilaya za Kusini ambao walikula muhogo uliokuzwa kwenye eneo la ukame.

Kwa hiyo, kwa Wilaya ya Mwanga na ukame ulioko pale, muhogo japo unaweza kukua kwenye ukame lakini haufai kula ukishakua kwa sababu unakuwa na *glucocide* za *cyanide* ambazo ni nyingi kuzidi inavyowezekana mtu kuula bila madhara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo lile, pamoja na ukame, mvua ndogo huwa inakuja. Kwa hiyo, tunaomba sana wataalam wa Idara ya Umwagiliaji iende kule itusaidie kupima maeneo ambayo tunaweza kuvuna maji. Wakati wa mvua, maji hayo yanakuwepo yanapita kwenye makorongo na kwenye mito yanakwenda Mtoni na yanaondoka. Kwa hiyo, tunaomba sana watusaidie kutengeneze makinga maji ili tuweze kuvuna maji wakati mvua inaponyesha. Wakati mvua inapokuwa hafifu tunapokuwa na vipindi vya ukame, basi maji yale tuyapeleke shambani hasa katika majaruba ili tuweze kukuza mpunga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunayo mabonde mengi na mimi napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wiki iliyopita alituma wataalam kule kwenda kuyaangalia maeneo haya ili kuangalia ni jinsi gani wanaweza kutusaidia kuepukana na upungufu wa chakula kila mwaka. Kwa hiyo, nawashukuru sana. Lakini napenda hapa ni-*emphasis,* nilikuwa nimekosa nafasi ya kuzungumza hapa leo. Kwa hiyo, nimeandika kama mchango wa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji sana tupate makinga maji katika Kata ya Kileo katika eneo la Kifaru, Kituli, Mforo na Kileo yenyewe. Mkurugenzi wa Umwagiliaji alikuwa ndiye mtaalam wa kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yale, kwa hiyo, anafahamu sana.

Mwaka jana walituahidi kwamba katika eneo waliloliita *Butu system* ambapo kuna miradi ya Mwanjo, Kirurumo, Kwakihindi, Kwakoa na Mabashula walituahidi kwamba wangeweza kusaidia kuendeleza mabonde yale. Nimewaambia kwamba kulikuwa na matatizo ya Bajeti na kwa hiyo, kazi ile haikufanywa. Lakini mwaka huu sioni matatizo yanaweza kutokea maana hela tuliyonayo hapa ya *development* alhamdulillah! Kwa hiyo, ninawaomba sana baada ya kufanya tathmini ya awali, basi mwende kule mtusaidie kuendeleza mabonde haya ili tuepukane na upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa sana nitoe rai katika miradi mikubwa ya umwagiliaji ambayo imejengwa kule kama Mradi wa Kivulini. Kwa kweli Mradi wa

Kivulini ambao ni mradi wenye hekta 1500 kwa kweli haukutekelezwa vizuri. Yule mkandarasi hakufuata *specifications* ambazo zilikuwepo. Mradi umetengenezwa, hakuna maeneo ya kupeleka trekta shambani, hakuna eneo ambalo wakulima wanaweza kuruka ile mifereji ya umwagiliji wakaenda kwenye mashamba yao. Kwa hiyo, kuna wakulima, mama mmoja na mtoto wake wamekufa wakijaribu kuruka kwenye mifereji hiyo kwa sababu hakuna eneo la kuingiza trekta, hakuna eneo la kuingiza maksai na watu. Maana yake umejengwa uwe wa kulima kwa jembe tu. Kwa hiyo, tunawaomba Wizara waukamilishe mradi huu ikiwa ni pamoja na kuweka maeneo ambayo wanyama watakunywa maji.

Mradi wa pili ni Mradi wa Kiria ambao ni wa zamani sana. Tulikuwa tunaomba Serikali itusaidie kuukarabati kwa sababu asilimia 60 ya maji ya mradi huu yanapotea bure badala ya kuingia shambani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, basi niseme anglau neno moja linalogusa kilimo kwa ujumla. Nilipokuwa nasoma hotuba ya Bajeti, niliangalia sana yale maeneo ambayo mimi nadhani ni maeneo nyeti sana. Ili kuendeleza kilimo, ni lazima kufuata masharti ya kilimo bora na masharti ya kilimo bora yanahusu kutumia mbegu bora, kutumia mbolea na kupanda mimea mingi kama inavyokuwa *recommended* na wataalam wetu. Kwa mfano mkulima anayelima mahindi anashauriwa kupanda mimea kama 45,000 kwa hekta moja. Sasa kama kule kwetu tunavyopanda kwa Kipare, basi mkulima anapanda kwenye hekta moja anapanda mimea 17,000 kwa hiyo, ameshapunguza uzalishaji kwa nusu nzima. Kama hakutumia mbegu bora, basi amepunguza kwa zaidi.

Kwa hiyo, kwa mazao yetu mengi hapa Tanzania uzalishaji wetu uko kwenye kiwango cha asilimia 10 mpaka 20. Pale tungetakiwa kupata kilo 100 tunapata kilo 10. Pale tungetakiwa kupata kilo 1000 tunapata labda kilo 90 za zao hilo. Yote hii inatokana na kutofuata masharti ya kilimo bora. *(Makofi)*

Sasa katika Bajeti, tumeambiwa tunahitaji tani 12,000 za mbegu. Lakini mwaka jana tuliambiwa tunahitaji tani 32,000 za mbegu. Kwa hiyo, nadhani kuna ka-*variation* kidogo hapa. Kwa nini? Lakini ninachotaka kusema ni kwamba mbegu nyingi zinatoka nje kuliko zile tunazozalisha wenyewe. Kwa kweli mbegu tunazonunua kutoka nchi za nje hazikidhi mahitaji kwa sababu hazikuzalishwa kulingana na mazingira yetu. Kwa hiyo, tunaomba sana mbegu bora kwa asilimia 90 kwa 100 *at least* zizalishwe hapa nchini na zipewe ruzuku kama mbolea. Mbegu ni ghali sana. (*Makofi*)

Pia, mbolea ni ghali sana lakini Serikali imechukua hatua kubwa sana ya kuweka ruzuku. Nilikuwa napiga hesabu hapa juu ya bahasha nikaona kila kilo ya mbolea inapewa ruzuku karibu Sh.90/= hivi. Sasa kama mbolea yenyewe gunia moja linanunuliwa Sh.7,000/= halafu na Serikali inalipia Sh.4,500/= kwa gunia la kilo 50, basi mbolea ingemfikia mkulima chini ya Sh. 10,000/= kwa gunia la kilo 50. Sasa bado mbolea pamoja na kupewa ruzuku, inauzwa Sh.16,000/= mpaka Sh.25,000/=. Suala hili tuliangalie kwa makini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbolea hii itoke Dubai ije Dar es Salaam, ipelekwe kwa gari la Lori mpaka Lusaka halafu iuzwe Sh.12,000/= kwa gunia moja, haiwezekani pale Dar es Salaam iuzwe kwa Sh.16,000/=. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo tunatakiwa tulifanyie utafiti na tujue ni tatizo gani na tulisahihishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine la msingi ambalo ni vyema tukaanza kulijadili ni matumizi ya maji. Lazima tufike mahali tuseme, hivi maji yetu tuyatumie kufanya nini? Hivi sasa kipaumbele cha kwanza ni kuzalisha umeme. Hivi kweli tumefikia hapo? Kwa nini kipaumbele cha maji kisiwe kunywa, kumwagilia halafu umeme? Umeme tukazalisha kutokana na makaa ya mawe. Tukazalisha kutokana na gesi na tukazalisha kutokana na *geothermal sources* nyingine badala ya kutumia maji haya ambayo tunataka kunywa, kumwagilia mashamba. Tupunguze matumizi ya maji kwa ajili ya kuzalisha umeme kama ndiyo kipaumbele chetu cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naungana na wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Arumeru Mashariki. Natoa pole za dhati sana kwa kufiwa na mwenzetu Mheshimiwa Margareth Bwana. Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, kiafya kwa kweli sikuwa *fit* sana wakati huu, lakini tangu jana nimekuwa nikipigiwa simu kila baada ya masaa kadhaa kwa ajili ya hoja inayotolewa leo ya Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa sababu muhimu, hasa kwa sababu ya *interest* ambayo wananchi wa Jimbo langu la Arumeru Mashariki wanayo kwenye hii Sekta ya Kilimo na Chakula na hasa salamu ambazo walipenda nizifikishe kwa Wizara hii kupitia kwa Mheshimiwa Waziri na waandamizi wote wa Wizara hii. Naomba nipewe hiyo fursa kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Mheshimiwa Katibu Mkuu na Viongozi wote wengine kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya katika Wizara hii na inaonyesha katika hotuba hii ambayo imetolewa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, salamu ambazo nimetumwa na ambazo wananchi wangu wa Arumeru Mashariki wanaikumbuka, kwa muda mrefu Wana-Arumeru Mashariki ambao wanatufahamu, tumekuwa kidogo na matatizo ya kiardhi kwa muda mrefu na wengi wakidhani kwamba huenda sisi ni wagumu kwenda kwenye maeneo mengine au kuanza maeneo mapya. Samahani kutumia hilo neno geni, wakadhania kwamba sisi ni *conservative*. Ni ukweli lakini hatukudhania kwamba kuna mtu ambaye angeweza kutuhamasisha tukaweza kubadilika na kuanza maisha mengine mapya.

Tunaomba kutoa taarifa kwamba kwa kupitia hamasa tuliyopata kupitia uwezeshwaji wa Wizara ya Kilimo na Chakula na hasa Mheshimiwa Waziri, Charles Keenja na timu ya Wizara nzima, Wana- Arumeru Mashariki wamehamasika kuanzisha vikundi ambavyo viko tayari. Wameshahamasika na wako sasa hivi katika makazi mapya wakiwa na lengo la kilimo cha biashara na kuendeleza kilimo cha kahawa bora.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi wameniambia nifikishe hizo salamu zao, lengo lao liko pale pale, karibu 3000 mpaka 4000 tayari wako kwenye makazi mapya. Matatizo makubwa ni makazi pamoja na hali ya hewa kwa sasa hivi pamoja na uwezeshwaji kwa maana ya mazingira yaliyopo sasa hivi, bado hayajawaruhusu kuanzisha makazi ambayo ni ya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanachoomba ni kupewa utalaam na kuweza kuanzishiwa utaratibu wa kukweza kupata uwezeshwaji wa kuendeleza makazi hayo. Walipofika Wizarani, waliona kwamba wana uwezekano na huo uwezekano imekuwa matatizo katika kufuatilia kwa sababu ya hali ilivyokuwa. Lakini kwa kweli wameona matumaini makubwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mengine yanayohusu hili suala ambalo limejitokeza la mbolea. Tuna taarifa tatu katika Jimbo langu, Tarafa ya Poli, King'ori na Mbuguni. Tarafa ya Mbuguni na King'ori pamoja na Poli zina misimu miwili tofauti. Tarafa ya Poli msimu wake wa mazao ya chakula unaanza wakati huu. Sasa hivi ninavyozungumza wako shambani wanalima. Mahitaji yao ya mbolea ni wakati huu.

Ukanda huu mwingine wa chini wa Tarafa ya Mbuguni na King'ole, wanangojea sasa kuvuna. Kwa hiyo, mahitaji ya mbolea pamoja na pembejeo nyingine yanakuwa ni kwa nyakati tofauti. Bahati mbaya wakati ambapo wale wa Tarafa ya Poli wakati wanahitaji mbolea, haulingani na wakati ambao mbolea ya ruzuku inatolewa. Kwa hiyo, hawafaidiki na ile mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Spika, ombi ni kwamba, mara nyingi wanapotaka kupata mbolea hii, ni lazima waende Mjini Arusha au waende *Usa River,* napo ni umbali wa si chini ya Kilometa 15 mpaka 20. Ni mbali! Mara nyingi, isipokuwa kwa mwaka huu ambapo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ilisaidia katika kutoa uratibu kwa kiasi fulani lakini kwa kweli wengi kwanza inakuwa vigumu kupata taarifa kwamba pembejeio hizi zipo au mbolea hii ipo. Wanaouza hawafahamiki mara kwa mara hawapati taarifa, wanapokuja taarifa zinakuwa zimekwisha, zinanunuliwa na watu binafsi na watu binafsi wanauza kwa bei za kawaida.

Mheshimiwa Spika, ombi ni kwamba tungependelea kwamba kwenye Tarafa ya Poli, zipitie kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi. Vyama vya Msingi vya Ushirika ambavyo viko na wananchi pale pale karibu nao, vinaweza vikatoa huduma nzuri zaidi katika kusambanza pembejeo kuliko ambavyo sasa hivi mpango huu upo. Ndiyo mpango ambao unaweza ukafaa wananchi wa karibu Tarafa zote. Tarafa ya Poli na King'ori, Tafafa ya Mbuguni si yote lakini hata nayo pia inaweza ikafikiriwa mpango mwingine kwa sababu haina zao ambalo linafanana na Tarafa hizi nyingine mbili, Tarafa ya Poli na King'ori.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu hali ya hewa. Mara nyingi hali ya hewa inatutatanisha na taarifa tunazopata kuhusu hali ya hewa zinatutatanisha, tunapata taarifa kutoka kwa watu wengi na inatoka kwa Viongozi wengine wa siasa, wengine Viongozi wa jamii, wengine Serikalini na wakati wa hewa mara nyingi tunapopata taarifa

ya hali ya hewa inakuwa vigumu kuweza kutabiri kwamba kweli mvua ipo ya kutosha na kwa hiyo, uweze kuweka mipango yako ya kilimo kufuatana na taarifa tunayopata ya hali ya hewa.

Hatujui ni nani wa kukubaliana naye umfuate, mara panda mapema au wengine wanakwambia huu ndio wakati wa kuanza kulima, wakati wa kuanza kupanda, panda mazao ya muda mfupi, wakati mwingine inayokuja kutokea inakuwa tofauti na unavyoelezwa. Pendekezo langu kwenye hii sasa hivi, wengi tunafahamu kwamba teknolojia iliyopo ya hali ya hewa inatosha na ninavyoona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri inayoonyesha waziwazi kwamba kwa kweli kazi inavyofanyika na Wizara ni nzuri na utaalam upo. Lakini sijui kama *early warning system* katika Wizara itapatikana ya kuweza kutoa utabiri wa muda mrefu na ukawa sahihi! Ni gharama, lakini nina imani kwamba tunaweza tukaondokana na hili suala la kupewa utabiri wa hali ya hewa ambao unatoa *messages* ambazo zinakuwa *confusing* kwa wakulima. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, nafahamu masuala ya hali ya hewa yako kwenye Wizara nyingine pia, lakini ningependekeza kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula iwe na *unit* yake yenyewe ambayo inajitoesheleza kitaalam na kiteknolojia. Sio vizuri sana kutegemea *unit* iliyo chini ya Wizara nyingine, nadhani kama ilivyo sasa hivi, sijui. Kwa jinsi mlivyo, nina imani kwamba *in terms of expertise* kwa kweli mnajitosheleza. Nina imani inawezekana kuongeza jitihada katika hili.

Masuala mengine yanahusu mambo ya utafiti. Kama ambavyo inaonyesha kabisa kwenye taarifa ya kwenye hotuba ya Bajeti ni suala la *research*. Kuna masuala kama mawili hivi ambayo yanaanza kujitokeza kwenye tafiti zinazotokeza karibu kwenye nchi nyingi zinazoendelea. Kuna suala ambalo sijaliona na ningependelea kulisikia kwamba ni suala ambalo linaanza ku-*creep in,* baada ya muda si mrefu huenda litaingia kikweli kweli na litakuwa na *effect* kubwa katika nchi yetu na nchi nyingine za aina yetu. *Empathetically* nadhani ndiyo mwelekeo kwamba liingie. Mimi nadhani lisitukute hatujajiandaa na Wizara peke inayoweza kutuongoza katika hili ni hii Wizara ya Kilimo na Chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naona Wizara sahihi ndiyo hii Wizara na tungeomba hili suala litazamwe kwa undani zaidi na tuandaliwe kupokea masuala kama haya. Niliona pia kwenye gazeti kwamba wanaanza kututishia kwamba eti ukitumia soya kama ni mwanamke, huenda usipate mtoto kama ni nyakati zake. Lakini masuala kama hayo ni vizuri kwa Wizara ikatupa mwongozo. Mimi pendekezo langu ni kwamba, Wizara iwe na *consultative relations* za mara kwa mara na Bunge kulieleza kwamba tafiti zinazoendelea ziko wapi? *Status* yake iko wapi? Mwelekeo wetu ukoje? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Arumeru Mashariki wanamwombea sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na Watendaji wake Wakuu wote kwa ujumla, wanawatakiwa mema. Wanataka waone kwamba Awamu ya Nne ione Uongozi huu huu na nguvu hii hii na ari hii hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Ahsante Mheshimiwa Spika nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu. Sisi wananchi wa Jimbo la Siha tumepokea tena kwa masikito makubwa taarifa uliyoitoa hapa Bungeni ya kuondokewa na Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Dada yetu mpendwa, linatutia hofu, linaweka *tension* kwa sababu kumekuwa na mfululizo wa vifo.

Lakini ninadhani ni vizuri pia tukaweka vizuri masuala ya vifo haya, kwamba maisha hayana maana kama hakuna kifo, kama vile ambavyo kifo hakina maana kama hakuna maisha. Kifo kinaweka *value* katika maisha. Kama tungekuwa tunaishi milele, maisha yasingekuwa na maana. Ni pana sana, tukiingia huko tutachukua muda.

Lakini kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha nawapa pole sana ndugu na jamaa wa Mheshimiwa Margareth J. Bwana. Nakupa pole Mheshimiwa Spika na ndugu Wabunge wenzangu. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Margareth J. Bwana mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimekwenda Kilimani pale, lakini nilirudi haraka kwa sababu niliomba nichangie Wizara hii, kwa sababu ni Wizara ambayo inatuhusu Watanzania tulio wengi. Asilimia 87 ya Watanzania ni wakulima. Tunaposema kwamba nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi, 87 *percent* ni ya wakulima na chakula tunacholima hapa kinalimwa na wakulima wadogo wadogo ndiyo wanaitwa ma-*peasant* na sisi tunaozungumza humu ndani ni *voice* ya hao ma-*peasant.* Kwa hiyo, hii ndiyo Wizara yetu inayotuhusu sisi Wabunge wengi tulioko humu ndani. *(Makofi)*

Lakini tunapoizungumzia Wizara hii ni vizuri tukaweka *concept* hii vizuri ikaeleweka. Uchumi tulionao katika Tanzania na katika nchi nyingi za Kiafrika *in developing countries,* ni uchumi ambao unaitwa ni uchumi wa nyuma, duni na wa kikoloni mamboleo ndiyo *characteristic* yake. Lazima tuelewane hilo, uchumi ulio nyuma, duni na wa kikoloni mamboleo ndiyo uchumi huu unavyoitwa, ndiyo tulio nao.

Uchumi wa namna hiyo, ni uchumi ambao huwezi ukauita ni mpango wala huwezi ukauita ni programu. Hiki kinachoendelea katika nchi yetu kinaitwa shughuli. Hizi ni shughuli tu unazoziona. Ni harakati tu. Lakini huwezi ukaziita ni programu. Kwa sababu programu, lazima iwe na kitu kinapangwa. Unakiona kabisa hiki kama mvua hazikunyesha nitamwagilia. Lakini ama unamwaga mbegu unaweka hapo chini, unabaki unamwomba Mungu, unasema Mungu uliyeko juu mbinguni nakuomba mvua zinyeshe. Zisiponyesha umekwenda. Sasa huo uchumi ni uchumi wa ajabu ajabu sana! Ni shughuli tu hii! *(Kicheko)*

Huwezi ukasema uchumi huu unajua ni uchumi ambao uko *programmed.* Mheshimiwa Keenja uchumi wetu huu ni uchumi wa nyuma, duni na wa kikoloni mamboleo. *The basic contradiction* unayoipata katika uchumi wa namna hiyo ni kati ya *labour* na *level of the productive forces.* Naomba nieleze kwa Kiswahili. Ni kati ya nguvukazi na kiwango cha vitendea kazi. Ni kilimo ambacho watu wanaendelea kubeba

mzigo kichwani. Ni kilimo ambacho watu wanachukua mbegu wanarusha kwa mkono hivi, wanapanda.

Mheshimiwa Spika, kilimo kile ni kilimo cha kujikimu tu Mzee wangu. Unakaa tu unamwona ni mkulima mdogo mdogo anakuambia mimi usinibabaishe, mimi sili kwako. Ukimvuruga atakula karanga zake, atakula ndizi, atakaa, ataishi. Anakwenda hivyo hivyo, hakina mapinduzi ndani yake, hakuna maendeleo ndani yake. Yeye anaishi hamna ziada, akimaliza kulipa *school fees,* amevaa nguo, amekula amelala, amejenga nyumba, habari imekwisha. Hakuna ziada na *development* ni ziada, ndicho kilimo tulicho nacho hapa.

Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, usipokuwa na kitu kinachoitwa *surplus, there is no development.* Sasa kama tunakula, tunakunywa, tunalala, kimekwisha, unapelekaje watoto Shule? Unanunuaje petroli na unajengaje madarasa? Wenzetu wanachofanya duniani sasa hivi ni kuondoa huo mgongano tunaouzungumza kati ya maendeleo ya binadamu kwa maana ya nguvukazi na *level* ya vitendea kazi. Ndiyo maana Sam Nujoma pale kwao Namibia alipokuwa anaondoka *investment* yao kwa elimu ilikuwa *33 percent.* Akawaachia usia, katika *handing over note* yake kwa yule anayekuja, akawaambia: "Hakikisheni kwamba mna-*invest 50 percent* katika elimu."

*Fifty percent! Can you imagine!* Hiyo tunazungumza *Windhoek* si ya kwetu sisi. Ndiyo maana hapa kwetu tulipoanza habari ya kufikiria namna ya ku-*develop science and technology* tunaanza na Lyamungo. Mimi nilisema sawa sawa kabisa. Kuna matatizo yake pale, kuna mambo ya *STABEX*.

Lakini kwanza *address* suala la utafiti. Unaondokanaje na kilimo cha ajabu ajabu hiki kama hukufanya *researc*? Kazi kubwa imefanyika Lyamungo na watu wa Lyamungo, Profesa Terry mimi nampongeza kwa kazi nzuri na Wizara naipongeza kwa kazi nzuri. Wazo lile lilikuwa ni wazo zuri. Kwa sababu huwezi kuondokana na huu uchumi duni, nyuma wa kikoloni mamboleo. Huu unaitwa shughuli kama hufanyi utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima ufanye utafiti! Kama hufanyi utafiti hakuna uchumi! Tukapeleka hela pale mabilioni, tukataka sisi zifanye kazi hiyo na kazi inafanyika pale. Nimekwenda nataka ni-*appreciate* hapa kwamba *TACRI* wamenipokea tumezungumza, nikamwambia tumepitisha mambo haya, tumekubaliana. Nataka twende sasa Hai, Jimbo la Siha. Twende tukaweke sawa *pilots* chache. Twende tukafanye pale katika maeneo ambayo yatakuwa ni ya mfano kwa ajili ya wakulima wetu na wewe anza kufanya hivyo katika Jimbo langu la Siha.

Nataka tuwaonyeshe wakulima wetu wadogo namna ya kulima kahawa kisasa. Ile kahawa ya zamani tunaanza kuiondoa kidogo kidogo na Lyamungo wanafanya kazi nzuri. *It is my responsibility Mr. Speaker Sir, as a Member of Parliament* kusema hapa kwamba kazi inayofanywa na Lyamungo ni kazi nzuri na ninawatia moyo waendelee hivyo hivyo. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, kilimo hicho duni na cha kikoloni mamboleo, hicho ninachokiita shughuli, ni kilimo ambacho kinakaa kinamwomba Mungu mvua inyeshe.

Mheshimiwa Spika, ukienda Zimbabwe, ukitaka wakuwekee *insurance* katika kilimo chako watakuuliza kwanza, mabwawa yako yako wapi? Watakuuliza kwanza mfereji wako uko wapi? Hakuna *insurance agency* itakayokubali ikuwekee wewe *insurance* katika shamba lako kama unategemea mvua maana wanajua utaliwa.

Alikuwa anazungumza Profesa hapa, kule Zimbabwe wao wakati wa mvua ndiyo wakati wa kwenda likizo, hawalimi. Kilimo duni na cha nyuma na cha kikoloni mamboleo ni kilimo ambacho kinategemea mvua. Ukitaka kujua *characteristics* zake, ona jinsi unavyotegemea mvua, kila siku unategemea mvua, hivyo ujue basi Mzee wangu wewe ni mtu wa kumwomba Mungu. Maana ni *primitive!* Mahali pa kushikilia ni kwamba nenda kwenye kitu kinachoitwa *irrigation,* mwagilia! *(Makofi)*

Kila mtu atakuja ataku-*support.* Sisitiza hilo. Katika Jimbo langu la Siha nataka nitoe ushuhuda kupitia Wizara hii, walisikia, nikawaomba. Sasa nilikuja hapa na swali langu linaitwa Mfongo wa Mzungu na ndiyo maana wananiita Mzee wa *Mfongo* *Mfongo* ni mfereji, hicho ni Kichaga. Nikawaomba nisaidieni kuu-*revival,* kufufua mfongo wa mzungu tuondokane na shughuli, tufanye kilimo cha kisasa. Wizara kupitia Japanese *Aid* tukapata milioni 150 kwa ajili ya kusaidia ule mfereji. Mimi siwezi kukaa hapa nikasema Keenja hajafanya kazi bwana.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanyika kazi. Tumekwenda kule tumefufua huu mfereji na sasa tunapozungumza tukienda pale kazi inafanyika. Ndiyo nikajua kwamba sasa tunaanza kuondokana na kilimo duni. Nimekuja hapa kutoa ushuhuda kwamba Serikali imefanya kazi nzuri na wananchi wa Jimbo langu la Siha wana-*salute* kwa kazi hiyo iliyofanyika. *(Makofi)*

*Mfongo* wa Mae sasa hivi unatengenezwa. *Mfongo* wa Wanri sasa unatengenezwa, *Mfongo* wa Ndabo sasa unatengenezwa, Namgwiriri unatengenezwa na Lima unatengenezwa. Hiyo ni mifereji siyo Vijiji. Nimehama huko ni mifereji tu. Ina majina yake, *Mfongo.* Mimi nafikiri tufanye kazi hii. Ukitaka kuondokana na kilimo hiki cha ajabu ajabu imarisha *extension services,* waambie Maafisa wetu wa Kilimo waondoke pale Bomang'ombe waondoke katika Makao Makuu ya Wilaya waende Vijijini wakaonyeshe watu wetu namna ya kulima kilimo cha kisasa. Mimi hapo sitaki niendeleze kwa sababu wenzangu wamezungumzia. Nataka nizungumzie hii habari ya *STABEX* ambayo imezungumzwa hapa. *(Makofi)*

Iko ile pesa ambayo tumesema kwamba itakwenda sasa kwa maana yake habari ya kitochi Serikali ilishakataa. Hii tumelia hapa jamani wananchi wapewe hela kidogo na wao waendelee, wakaimarishe zao lile, imeshindikana. Sitaki kuingia kwenye hiyo *debate.* Hiyo barabara sasa iko wapi? Hiyo barabara tunayoambiwa kwamba itatengenezwa, kahawa kule kwangu inalimwa, Vijiji vya Lawate, Mae, Wanri, Sumu, Kashashi, Kitahema, hakuna barabara inayokwenda kule. Barabara zote tumeambiwa hela hizi zinakwenda kwenye *TANROADS*.

Nafikiri pale tuko *off target.* Peleka basi hiyo barabara, sasa tuachache na ile habari ya kusema kwamba wananchi wanapelekewa pesa, tumeshakubali. Mimi nimekubali, wakienda kunilalamikia sawa. Nitawaeleza, hiyo barabara, mimi Jimbo langu la Siha, *Kibong'oto Co-operative Society* ya kwanza katika Afrika inazalisha kitu kinachoitwa kahawa iko pale Siha na *yet* Jimbo la Siha halina *allocation* yoyote iliyopata ya barabara. Ni wakulima wa kahawa ya *Arabica*, lakini hakuna kipande cha barabara kimekwenda kule. Hapa naomba kutofautiana na Serikali. Haiwezekani kabisa! Patakuwapo na tatizo la msingi katika mipango yetu kwamba hatukuelekeza zile barabara zikaenda kule kwa wakulima wadogo wadogo wanaolima kahawa, wapelekewe. Ni hivyo hivyo, ukienda Mbinga, Kagera na maeneo yote yanayolima kahawa kuna *problem* kwamba tumepeleka barabara zile za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wa mawazo yangu katika hii Wizara ya Kilimo na Chakula. Lakini kabla sijaendelea na mchango wa mawazo yangu, niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Margareth J. Bwana. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli ameeleza kwa kirefu jitihada za Wizara yenyewe na sisi tunaafiki na tunamuunga mkono kwa kazi yake nzuri. Kwa hiyo, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nataka nizungumze machache tu kwa kweli, mengi yameongelewa na wenzangu na mengi kayaongelea Mheshimiwa Waziri. Ni mazur,. Lakini nataka nizungumze na mimi yale ambayo yanalingana na eneo na hali ya mazingira. Nataka nizungumzie hasa juu ya barabara hizi za mazao ya biashara na nataka nizungumzie hasa juu ya zao la pamba. Wenzangu waliotangulia wamezungumzia, kwa mfano zao la kahawa huchagiwa fedha kwa ajili ya barabara, zao la chai hutengewa hela kwa ajili ya barabara. Lakini nataka nizungumzie juu ya zao la pamba ambalo ni muhimu sana katika nchi yetu na linatoa mchango mkubwa kwa kutungizia pato letu la Taifa. Nataka nianze kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Zao hili la pamba mwaka 2004 thamani ya mauzo ya pamba iliongezeka kwa asilimia 60.4. Ukisoma katika hiki kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa mwaka 2004, mwaka 2004 thamani ya mauzo ya pamba iliongezeka kwa asilimia 60.4 hadi Dola milioni 74.6 kutoka Dola milioni 46.5 kwa mwaka 2003. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya pamba kwa asilimia 52 kutoka tani 46,900 mwaka 2003 hadi tani 71,300 mwaka 2004. Sasa ukiangalia pato ambalo zao hili huingiza ukilinganisha na mazao mengine kwa mfano kahawa 2004 iliingiza Dola milioni 49.8, halafu katani iliingiza Dola milioni 7.3, ukija chai iliingiza Dola milioni 24.7. Sasa ukiangalia hapa zao ambalo linatoa mchango mkubwa kwa Taifa ni zao la pamba. Lakini

huduma za usafiri kwa wakulima ni mbaya. Nataka nitoe mfano mzuri kwa eneo ninalotoka. Nina Kata zisizopungua kama mbili. Moja, Mwadiluhumbo nyingine Somagedi. Ni maeneo ambayo yanalima pamba kwa wingi, lakini tangu nchi ipate uhuru hawajaona barabara na ndiyo wazalishaji. *(Makofi)*

Naishauri Serikali, moja ya motisha ya kuwasaidia wakulima wetu ni kuwawekea mazingira mazuri hata ya usafirishaji pamoja na kilimo. Ni kweli kwamba Serikali imekuwa ikisisitiza suala la mbolea. Hiyo mbolea itafikaje kama hali ya usafiri ni mbovu? Kwa hiyo, naiomba Serikali kama inavyofanya kwa mazao mengine, basi itoe uzito vile vile kwa zao la pamba, wakulima watengenezewe barabara ili waweze kusafirisha mazao yao vizuri.

Vile vile iwe kama ni motisha, walime vizuri wakijua Serikali inawatambua. *Imagine* kama nilivyotoa mfano, tangu mwaka 1961, watu wanalima pamba, hawajajengewa barabara. Lakini Taifa linawategemea watu hao walime zaidi, watoe mchango mzuri kwa Taifa ili Taifa liendelee.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wakati sasa umefika tujaribu kuangalia suala hili la kuangalia usafiri hasa maeneo haya ambayo yanalima pamba, tuweze kutoa motisha kwa wakulima wetu walime vizuri, wasafirishe mazao yao kuchangia pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni mazao haya ambayo tulishauriwa na Serikali kulima katika maeneo ya ukame. Kwa mfano Shinyanga, Dodoma na maeneo mengine. Tumeshauriwa kulima mazao ambayo yanavumilia ukame kama vile mtama na uwele. Nataka kuzungumzia kwamba wananchi wameitikia wito kulima mazao hayo. Tatizo linalowakabili ni ndege aina ya kweleakwelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kukamilisha shughuli za kilimo na mazao haya yakianza kuiva, kweleakwelea huvamia mashamba haya na kuleta usumbufu mkubwa sana. Hivi ninavyosema ni kwamba, juzi nilikuwa Kishapu pamoja na hali mbaya ya hewa, bado wananchi wanaendelea kusumbuliwa na ndege hawa kweleakwelea. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali ijaribu kutusaidia kutoa huduma mara kwa mara pindi wananchi wanapopatwa na tatizo hili la kweleakwelea ili tuepushe nchi yetu kukabiliwa na tatizo la njaa. Vinginevyo itakuwa hakuna faida kama wananchi wameitikia wito, wanalima halafu wanalimia ndege, Serikali haitoi huduma au huduma yenyewe inakuwa ya urasimu. Ndege wanashambulia leo, ndege ya kunyunyizia inakuja baada ya wiki moja, inakuta mazao yalishaharibika kabisa.

Kwa hiyo, mimi naomba Serikali ijaribu kutusaidia kutupa huduma hii na mara matatizo yanapotokea, basi huduma hii itolewe mapema iweze kusaidia wananchi waondokane na tatizo hili. Nadhani hilo litakuwa nimeeleweka.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia, kama walivyozungumzia wenzangu, kwa kweli tusidanganyane. Serikali kama haitatilia mkazo suala la umwagiliaji maji mashambani, hatutaondokana na tatizo la njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wameeleza, pamoja na Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza sasa hivi, Mheshimiwa Mwanri amezungumza vizuri tu kwamba kwa kweli kama tutaendelea kutegemea kilimo cha mvua, hatutabadilisha hali ya maisha yetu. Nimejaribu kuangalia katika kitabu cha Waziri, ni kweli kimeonyesha baadhi ya maeneo *schemes* ambazo zinatekelezwa na Serikali kwa ajili ya umwagiliaji. Lakini haijatosha, bado kidogo sana.

Yako maeneo mengi ambayo yanafaa kwa zao hili la umwagiliaji, kwa mfano maeneo ya Kanda ya Ziwa, kuna hii sehemu ambayo inatoka Mto Manonga hadi bonde la Wembere Singida. Ni eneo ambalo ni zuri kabisa kwa kilimo cha umwagiliaji na utafiti huu ulishafanywa miaka ya nyuma tangu mwaka 1920, ulifanywa utafiti na Wakoloni na wakaonyesha nia kwamba ni eneo ambalo linafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ili nchi yetu iondokane na tatizo la njaa, tutilie mkazo zaidi suala la umwagiliaji maji. *(Makofi)*

Kuna Mbunge mmoja alikuwa anasema kwamba, unajua kila baada ya miaka 10 inapopita hutokea njaa na mimi nadhani inawezekana kuwa ni kweli. Kwa sababu mwaka 1964 tulikuwa na njaa, mwaka 1974, mwaka 1984, mwaka 1994 na mwaka 2004 pia tulikuwa na njaa. Kwa hiyo, tumekuwa na mazingira hayo ya njaa njaa tu, yaani eneo lenye njaa njaa tu na hata juzi mimi katika mchango nilizungumzia Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu suala hili la njaa. Kwa kweli ni jambo la aibu kuongelea njaa. Lakini kama una tatizo ufanye nini? Ni lazima useme. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali itilie mkazo sana suala la kilimo cha umwagiliaji ili nchi yetu iondokane na tatizo la kuagiza chakula nje. Tunatumia gharama kubwa sana kuagiza chakula nje badala ya kulima na kupata chakula chetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka niliseme kabla sijamalizia ni juu ya watumishi wa Wizara hii ya Kilimo wanaostaafu kupata maslahi yao. Kwa kweli wanasumbuka sana. Nina mpigakura wangu mmoja, leo sijui ana miaka mingapi, nimekwenda pale Wizarani na makaratasi sijapata msaada wa aina yoyote. Badala ya kuidai Wizara, yule mtumishi kaamua kunichukia mimi kwamba simshughulikii kupata maslahi yake. Hatusalimiani kwa sababu ya maslahi yake. Namwambia mimi siyo Wizara. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kuangalia pale Wizarani pana matatizo makubwa. Nafikiri si mtu mmoja tu, wako wengi wanaodai maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui kuna nini pale! Mimi sijaelewa. Mtu anapostaafu si apewe haki yake, akajenge maisha yake! Sasa kwa nini tubebe lawama? Kwa nini tusisalimiane kwa ajili ya haki ya mtu? Nisisalimiwe kwa sababu ya pensheni ya mtu! Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ajaribu kuangalia pale, pana matatizo. Jaribuni kuweka mazingira mazuri ili mtu anapofanya kazi yake, basi apate haki yake akaishi vizuri kule badala ya kuendelea kupata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze vile vile Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Tunamtakia kila la kheri na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii. Kwa hali hiyo, napenda kutoa maoni au ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001/2002 Halmashauri ya Manyoni ikishirikiana na Bodi ya Korosho na Kituo cha Utafiti cha Naliendele walianzisha majaribio ya kilimo cha zao la korosho Wilayani Manyoni. Miche ya Mikorosho ya kisasa ilisambazwa kwa wakulima na mashambani. Mikorosho hii baada ya miaka mitatu imeanza kuzaa. Lakini ufuatiliaji wa wataalam haupo. Waje waone maendeleo ya jaribio hili, waendelee kuleta miche kwa wakulima wengine. Kwa kifupi zoezi hili tunashauri liwe endelevu. Hivi sasa limesimama.

Mheshimiwa Spika, Skimu za Umwagiliaji *(IFAD),* tunashukuru Wizara kwa Skimu za umwagiliaji za Chukuyu, Umbka, Msemembo, Udimaa na Serunda. Hata hivyo, tunashauri skimu hizi sasa zingekuwa mabwawa hatua kwa hatua ili kilimo hiki kifanyike bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pongezi kwa kazi nzuri.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo na Chakula. Naomba Wizara itoe malengo ya upandaji mikorosho mipya katika kila Wilaya inayolima korosho.

Mheshimiwa Spika, katika *paragraph* ya 24 ya kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, korosho zinabanguliwa, siyo kusindika.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, aliyefariki jana. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu wake na wataalamu wote pale Wizarani. Nawatakia juhudi na ufanisi mkubwa katika kazi zao. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Bukumbi na Shitage katika Jimbo la Tabora Kaskazini zimeingia katika kilimo cha pamba kwa mara ya kwanza kabisa mwaka jana 2004. Pamoja na furaha ya wakulima kupata fursa ya kujipunguzia umaskini/kujiongezea kipato cha njia ya zao hili, bado mioyo yao imeingiwa simanzi kwa kutokulipwa fedha za pamba yao ya mwaka jana, 2004. Hadi hivi sasa tunavyoongea, wakulima hawa wanajisikia wamesalitiwa kwa kukopwa tena bila kuwa wameonywa na isitoshe kwa

kuendelea kuachwa gizani bila taarifa za kuaminika kuhusu namna na lini watalipwa mamilioni wanayodai. Kampuni ya *KACU* ambayo ndiyo ilipewa ruksa kununua pamba yao, imekuwa tapeli mkubwa. Wamekaa kimya, hawasomi kabisa wala kuleta matumaini kwa wakulima wetu kwamba, ni lini watalipa huku tayari msimu mwingine ukiwa umeanza!

Mheshimiwa Spika, jambo hili linafahamika katika Bodi ya Pamba na Serikalini. Je, Wizara ina msaada gani katika kuhakikisha wakulima wetu wanalipwa na kwamba hawakatishwi tamaa na vitendo vya *KACU* kiasi cha kuathiri juhudi zao za kulima pamba kwa kuongeza kipato chao? Ni muda mwafaka sasa Serikali ikatoa tamko lake juu ya *KACU* kuwatapeli wakulima hawa. Tamko tunalohitaji hapa, ni lini fedha hizo zitalipwa?

Mheshimiwa Spika, mazingira ya ufanisi katika zao la tumbaku yameendelea kuwa mazuri tangu sheria mpya ya tumbaku ya mwaka 2001 ilipoanza kutekelezwa. Lakini pia kumeendelea kuwepo matatizo ambayo mimi nilidhani yanatatuliwa na sheria hiyo. Tatizo mojawapo la namna hiyo, ni kuendelea kuwepo kwa *ATTT* na kuendelea kwake kujihusisha kikamilifu katika biashara ya tumbaku pamoja na kuwa hawana leseni ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo ambalo naona limeondoshwa na sheria. Swali ni kwamba, kwa nini basi *ATTT* bado wanaendelea kuwepo na isitoshe wanaendelea kufanya biashara ya tumbaku huku hawana leseni? Mimi binafsi nimeuliza mara kadhaa hapa Bungeni juu ya uhalali wa *ATTT* kuendelea ku-*function* baada ya sheria ya mwaka 2001 kuanza kufanya kazi, lakini nasikitika kusema kuwa Serikali haijatoa kauli yenye urahisi wa kueleweka juu ya uhalali au kutokuwa halali kwa *ATTT* kuendelea kuwepo na kuendelea kujihusisha kikamilifu na biashara ya tumbaku.

Mheshimiwa Spika, *ATTT* ni tatzizo na kwa kweli ni kikwazo kwa wakulima wetu kufaidika na soko la ushindani. Ni tatizo kwa wakulima wetu katika utaratibu wa kupokea malipo yao. Ni tatizo kwa wananchi kwa ongezeko la *overheads* kwa ajili ya kuendesha hiyo *ATTT*. Kwa nini Serikali haioni haya na mengine mengi na haitaki kulimaliza tatizo hili ambalo kimsingi limemaliza na vifungu vya sheria ya tumbaku ya mwaka 2001 kwa upande mmoja na baadhi ya vifungu katika *Articles of Association* za *ATTT* ambazo zinapingana bayana na sheria? Ni kwa nini hali hii inaruhusiwa kuendelea? Nini basi maana ya kuwa na sheria na kuwepo kwa Idara za Serikali ambazo zinatakiwa kutekeleza sheria, ikiwemo Sheria ya Tumbaku, katika kutekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wakulima wetu wa tumbaku baadhi wamefanya juhudi za kufikiria mikopo *CRDB* kwa ajili ya kuimarisha/kuendeleza kilimo cha tumbaku. Lakini wanapambana na matatizo kweli kweli na yanasababishwa na hawa matajiri. Wanaona tonge lao kupitia kukopesha pembejeo linawaponyoka. Hawataki kumwacha mkulima wetu awe na mahusiano na *CRDB*. Kwa nini wanathubutu kufanya hivyo? Siyo kwa sababu wanazoea kuachwa tu waendelee kufanya wanavyotaka hata kama sheria hairuhusu? Siyo kwa sababu ya jeuri yao ya fedha?

Mheshimia Spika, naomba maelezo ya kina hapa. Naunga mkono hoja.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapa pole familia, rafiki na ndugu wa Marehemu Margareth Bwana aliyetutoroka jana tu na kwa majonzi makubwa tunawapa pole wananchi wa Mkoa wa Rukwa na pia Jumuiya ya *UWT*.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu inajadiliwa wakati wa hali ya hewa ya nchi nzima ni mbaya na ya kutisha, siyo tu mwaka huu ila kwa miaka minne mfululizo, mvua imekuwa sio ya kutabirika. Matokeo yake Taifa hili linaendelea kukumbwa na janga la njaa na ukame, upungufu wa chakula, kukithiri kwa umaskini kwa wananchi walio wengi hasa wakulima wadogo Vijijini (asilimia 80 ya idadi ya watu).

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo katika Taifa letu linahitaji mapinduzi makubwa na sio kuendelea kuimba kuwa kilimo kinaendelea, kinakua. Mapinduzi kitaifa katika kilimo yatatokea tu kama Serikali itaachana na tabia ya kujihami mara agenda ya kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo inapoletwa mbele ya Bunge au mbele ya wananchi. Kuvuna maji ya mvua maana yake ni Serikali ikubali waziwazi sera ya mtazamo wa muda mrefu wa maandalizi ya kutosha (*long term planning strategy in rain water harvest strategy for agricultural transformation*). Sasa Serikali itayarishe maeneo yanayofaa kwa kuvuna maji, ujenzi wa miundombinu za mabwawa/malambo na maeneo ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, tukijikita katika sera ya kuvuna maji, tutakiletea mageuzi makubwa kilimo na kukifanya kuwa ni shughuli ya kudumu ya misimu yote miezi 12 badala ya sasa kilimo cha msimu mmoja, shughuli za kubahatisha mvua. Kama wakulima wataweza kuvuna mazao zaidi ya mara mbili au mara tatu kwa sababu ya kuwepo na maji ya kutosha kwa kumwagilia mashamba basi kilimo kitachangia kwa kiwango kikubwa katika kupunguza umaskini.

Kilimo cha leo cha kutegemea mvua kinacholetea kuvuna mara moja ni kilimo cha kujikimu matumbo na hakuna mavuno ya ziada ambayo yatachangia kwenye kutokomeza umaskini. Pasipo maji, hakuna kilimo na kwa leo tuelewe au tujifanye kutokuelewa njaa na ukame katika Taifa letu ni suala la kujitakia, kwani tukikubali mapinduzi makubwa kwenye Sekta ya Kilimo njaa na ukame itakuwa historia kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tabia ya Wizara ya Kilimo kuokoteza au kupika takwimu za kukua kwa kilimo, kuongeza kukuwa kwa kilimo cha umwagiliaji ni kuwadanganya wananchi. Kwa miaka mingi mchango wa kilimo katika Taifa letu haujaonyesha kukua au kuboreka kabisa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula imerembwa na vitakwimu vingi vya uongo na kweli, lakini hali halisi kilimo kinaendelea kudidimia. Tunalohitaji hapa ni mapinduzi (*about turn*) na siyo kuendesha kilimo cha kutegemea mvua. Katika Wilaya ya Iramba pametajwa kuwa kuna skimu zifuatazo za kilimo cha umwagiliaji. Mlandala hekta 300, masimba hekta 400 Korondatali hekta 100, Tyeme/Masagi hekta 200.

Cha kushangaza sana, maendeleo haya hakuna kilimo cha kumwagilia. Skimu ya Kirondatali mpaka leo haijaanzishwa. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Kilimo basi ikashughulikie skimu za Masimba Tyeme/ Masagi na Mlandala, Wizara ione umuhimu kutenga fedha za kutosha kujenga mabwawa ya maji kusudi skimu hizi ziwe mahali ambapo wananchi, wakulima katika Vijiji hivi waweze kuongeza juhudi za kuongeza kuzalisha mazao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na Serikali ione umuhimu wa kuleta mapinduzi kwenye kilimo sasa.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii awali kabisa kutoa pole na rambirambi kwa ndugu, jamaa na wananchi wa Mikoa ya Rukwa na Mara kutokana na kifo cha Mheshimiwa Margreth Bwana.

Pongezi nyingi nazitoa kwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wote Wizarani kwa jitihada nzuri zinazofanyika.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kukumbusha Wizara juu ya mradi wa uchimbaji wa bwawa la kumwagilia katika mashamba ya mpunga ya Nduguti katika Kata ya Itwangi Wilayani Shinyanga Vijijini.

Ni mwaka wa pili sasa tangu Wizara kupitia, Naibu Waziri alipofanya ziara Wilayani petu na kupokea hoja yangu mbele ya wananchi juu ya kuboresha kilimo hicho kwa kujenga bwawa badala ya kutumia mifereji kwa kutumia mto Manonga ambapo maji yanapita tu baada ya mvua kuonyesha. Kimsingi napenda kufahamu tatizo liko wapi na hatua gani zimechukuliwa hadi sasa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo Bodi ya Mazao, kama ilivyo Bodi ya Pamba, nashauri kuwa, kwa kipindi kilichopo ni vyema kutazama upya sheria ya uundwaji wake, kwani bado wananchi na wakulima hawapati msaada wa kutosha kupitia Bodi. Mimi nadhani wakulima tumewatwisha mzigo ambao unafanya bei ya mazao iwe ndogo kutokana na gharama za uendeshaji wake. Pengine tutumie Ushirika pekee ufanye majukumu ya Bodi ya Kilimo cha Umwagiliaji. Ni ufumbuzi wa uhakika kwa wananchi wetu.

Kwa hiyo, naishauri Serikali yetu ilipe kipaumbele suala hili hasa katika Mikoa yote inayozunguka Ziwa Victoria. Kwa kuanzia, napenda kuelekeza Jimbo la Solwa katika Bonde la Salawe ambako mkondo wa Ziwa Victoria humwaga maji. Ni eneo zuri sana la umwagiliaji. Kama watalaamu wako wakiendeleza mradi wa umwagiliaji utakuwa ukombozi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pole na rambirambi zangu kwako, Bunge na familia ya Marehemu Margareth Bwana kwa

kuondokewa na Mheshimiwa Mbunge huyo. Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri Keenja pamoja na Naibu Waziri Profesa Mbawala, Katibu Mkuu na Watendaji/wataalam wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Mkoa/Wilaya ya Singida ni miongoni mwa Mikoa na Wilaya zenye ukame mkubwa kutokana na uhaba wa mvua. Hivyo nashauri Serikali itupe *priority* katika suala zima la umwagiliaji maji. Nilishawasilisha Wizarani Vijiji ambavyo vinafaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji lakini hadi sasa sijaona utekelezaji wake. Nasisitiza maeneo haya yapewe umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji. Maeneo hayo yasaidiwe kupatiwa mabwawa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Keenja na hasa Naibu wake, Profesa Mbawala kwa kufufua *scheme* ya Mang'onyi katika Tarafa ya Ikangi. Kazi ya ukarabati wa sehemu hizo ya Mang'onyi imeanza lakini inasuasua kwa sababu ya uhaba wa fedha. Hivi sasa kazi imesimama kwa sababu fedha imekwisha. Kiwango kinachotolewa kila mwaka ni kidogo sana. Naomba fungu linalotolewa liongezwe ili sehemu hii imalizike mapema iwezekanavyo. Niliahidiwa kuwa, Wizara imeomba uhisani wa *write up,* ilishatayarishwa na kutumiwa huko kwenye Asasi inayosaidiwa fedha na Balozi wa Japan. Naomba kujua suala hili la uhisani/ufadhili wa *scheme* hii.

Mheshimiwa Spika, *SUDECO* waliniahidi kusaidia mashine ya utengenezaji wa sukari kwa wakulima wadogo wadogo. Mashine hizi zinapatikana katika Chuo cha Utafiti Morogoro, naomba suala hili likamilishwe. Mkurugenzi Mkuu wa *SUDECO* analifahamu tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE**: Mheshimiwa Spika, mimi na wananchi wote wa Mwanga tumeipokea hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa furaha kubwa. Kila mwaka tangu mwaka 2001nimeilalamikia Serikali kwa ufinyu wa bajeti ya Wizara hii. Bajeti iliyotolewa jana na Waziri ni nzuri sana na mwaka huu imefikia karibu Shilingi bilioni 120. Tunaipongeza sana Serikali kwa hatua hii.

Mheshimiwa Spika, nimeiangalia bajeti yenyewe na mipango ya Wizara, kwa kweli bajeti na mipango iliyowekwa ni mizuri. Hivyo napenda niunge mkono Hoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Charles Keenja kwa kazi hii nzuri sana. Nichukue fursa hii nimpongeze pia Prof. Mbawala kwa kazi nzuri. Tunapopata mipango mizuri, hapa kuna wataalamu walioitengeneza, hivyo napenda nimpongeze sana Ndugu Wilfred Ngirwa na wataalamu kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2004/2005, Katibu Mkuu wa Wizara alifanya juhudi kubwa ya kutupatia zao mbadala la kilimo, viazi mviringo. Utafiti wa Wizara ulionyesha kuwa zao hili linafaa sana katika maeneo ya milimiani. Tuliomba tani

tano ya mbegu, lakini kutokana na mbegu hiyo kuwa adimu, tulipatiwa na Wizara tani moja ya mbegu. Tunashukuru sana. Mbegu hiyo imepelekwa katika Kijiji cha Vuchama – Ndambwe, hata hivyo mbegu itakayozalishwa haitoshelezi kutokana na mahitaji makubwa. Hivyo, tunaomba tani 10 zaidi za mbegu hiyo. Nategemea kuwa kwa bajeti kubwa iliyopatikana, hili litawezekana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mwanga imekuwa eneo la ukame kwa miaka mitano mfululizo. Inaelekea kuwa hali ya hewa ya *Horn of Africa* imeivamia Wilaya yetu na Wilaya za jirani za Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Manyara. Hata hivyo, tunao utamaduni mkubwa wa kujenga madimbwi na kutengeneza mifereji. Lakini kutokana na ukame hakuna maji kwenye mito wakati wa kiangazi. Hivyo, tunahitaji msaada wa haraka wa kutengeneza sayansikimu za umwagiliaji katika mabonde ambapo maji ya mvua yanaweza kuvunwa kama ifuatavyo:-

(i) Bonde la Kwakoa, kutengeneza makinga maji na mifereji kuelekea mashambani (ha150);
(ii) Mto kutoka Kizungo, kujengewa makinga maji ili kunyeshea eneo la Toloha (ha 110);
(iii) Bonde la Mvureni, kukinga mto Ndurumo na kuendeleza mradi wa kumwagilia wa Kampiso (ha220);
(iv) Mradi wa Kivurumo, eneo la Butu Usangi na Butu Ugweno (ha180);
(v) Mradi wa mwanjo (ha 540);
(vi) Kukamilisha miradi ya Mabashula, Kivisini, Kituri na Kisangiro –Mforo (ha70);
(vii) Miradi ya Kirisi, Kiruru (ha70);
(viii) Kukamilisha mradi wa Kivulini na Kivya (ha 2200).

Mheshimiwa Spika, tuliahidiwa mwaka 2004/2005 kuwa miradi namba (i) – (iv) tungepata msaada wa kuanza miradi miwili au mitatu. Lakini hii haikuwezekana, nimeambiwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kuwa timu ya kuyaangalia maeneo haya imeishapelekwa Mwanga na hivyo Wizara inaijua miradi hii na Mkurugenzi wa Umwagiliaji anayaelewa sana maeneo ya miradi hii. Tunafarijika pia kuwa Bajeti mwa hii ni kubwa. Natoa rai mtusaidie kuitekeleza miradi hii hata kwa awamu ili tuondokane na tatizo la ukosekanaji wa chakula Wilayani kwetu. Niombe rasmi ruzuku ya Shilingi milioni 350 kama hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwapeleka wataalamu wake Mwanga wiki iliyopita ili kuiona miradi ya kilimo niliyoitaja wamekagua mradi wa kukinga maji (kuvuna maji) katika Kijiji cha Kifaru. Wananchi wamefarijika sana wakatembelea mradi wa Kituri, Kileo, Kivisini, mradi wa Sungo na Kampiro, nawashukuru. Sasa mnayo bajeti inayotosha kutekeleza miradi hii. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ESTERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Nawapongeza Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Profesa Mbawala pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri ufuatao kwa mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Mabwawa Mbarali:-

(a) (i) Kutokana na maji kupungua kwa kasi sana wakati wa kiangazi au mvua zinapopungua, nashauri mradi wa kujenga bwawa la Lugoda ufanywe kwa jitihada kubwa ili kilimo kiweze kufanywa mara mbili kwa mwaka.

(ii) Kinu cha kukobolea mpunga kinatumia *diesel*, gharama ambayo ni kubwa sana. Nashauri utafiti wa haraka ufanywe ili kutafuta njia mbadala ya kuzalisha umeme, kufanya kinu hiki kifanye kazi muda wote kwani kwa sasa hakifanyi kazi kwa muda wote kwa kukosa *diesel*.

(iii) Watumishi wa Wizara walioko katika Mradi huu wanahitaji motisha mpya ili waweze kufanya kazi zao kikamilifu. Hali ni mbaya sana kwa sasa.

(IV) *Power tiller* kama 50 zipo pale, nashauri wauziwe wakulima ili waweze kuzitimia.

(b) Mikopo ya Mfuko wa Pembejeo imekuwa ni tatizo kwa Mbarali hatuelewi tatizo ni nini. Maombi ya matrekta mapya, matengenezo ya matrekta yamekuwa yakipelekwa lakini mikopo hii haipatikani.

(c) Jitihada ya Wizara kuhusu kubihafsishwa mashamba ya Kapunga na Mbarali ziendelee kufanywa kuhakikisha kuwa yanabinafsishwa kwa wananchi badala ya mtu mmoja mmoja.

(d) Usafiri wa gari kwa Idara ya Kilimo Mbarali imekuwa ni tatizo kubwa sana. Ni lini Mbarali itafikiriwa kupewa usafiri ili Mkuu wa Idara ya Kilimo afanye kazi vizuri kama Wilaya nyingine zilivyopewa usafiri?

(e) Mwisho, maombi ya *Power tillers* kwa wakulima wa Mbarali ni makubwa sana pamoja na *spare* zake. Naomba Wizara ifanye jitihada ya kutafuta trekta zisizopungua 200 ili wananchi waweze kununua.

**MHE. EDSON MBEYALE HALINGA:** Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Wizara ya Kilimo hususan Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wao wote kwa kuandaa bajeti muafaka kwa lengo tunalolitarajia. Naomba nitoe mchango wangu katika baadhi ya maeneo.

Kwanza nashukuru kwamba mbolea aina ya *CAN* imeongezwa kati ya zile zilizopewa ruzuku na Serikali. Huu ni uungwana mkubwa kwa wakulima wa Wilaya ya

Mbozi kwa mazao ya biashara na chakula. Naomba mbolea iwahi mwezi Agosti hasa *DAP* ya kupandia ili kuwahi majira ya mvua za kupandia.

Tatizo lililojitokeza huko nyuma ni Kamati ya Mkoa na Wilaya kugawa hizo mbolea. Kila Kamati iliwapangia bei wachukuzi (wasafirishaji) na ilisababisha bei kupanda na kuiuka bei zilizotangazwa na Serikali kwa mbolea ya ruzuku. Naomba mbolea yote ipelekwe kwa Wakurugenzi na wanayo maghala ya Halmashauri na kwa Wilaya ya Mbozi hatuhitaji mikopo, wakulima watanunua kwa fedha taslimu na kwa muda mfupi sana.

Pili, wakulima wa kahawa Mbozi wako tayari kuwezesha kahawa bora kama wangesaidiwa mashine za kisasa *(pulpary)* ili kuboresha zao hilo na wapo watu binafsi wanaweza kununua. Aidha, tatizo kubwa ni wanunuzi binafsi ndio wanaokatisha tamaa wakulima kwa kuwadhulumu. Hawa wanunuzi binafsi hulipa bei ndogo na kufuatia kahawa majumbani. Imejitokeza kuwa, wananunua kahawa mbichi kwa kuwa wanapewa vibali na Bodi ya Kahawa kwa Sh.100/= kwa kilo wakati kilo tano za namna hiyo hufanya kilo moja ya *patchments*. Hiyo ambayo huuzwa karibu Sh.3,000/= kwa kilo.

Naomba Bodi isitoe leseni za namna hiyo. Sisi tunashauri wakulima waungane na wauze wenyewe na wapate bei ya soko. Hili limeleta mafanikio mno mwaka jana 2004. Tunaomba Kituo cha Mbimba kiongezewe nguvu kuzalisha mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, tatu, pareto inastawi sana katika Tarafa ya Iyula lakini hakuna utaratibu wa kuwekeza na kusimamia. Huko nyuma walihudumiwa na ndiyo mwisho wa kulimo hicho. Naomba lifufuliwe wananchi wako tayari.

Nne, mbegu za mahindi zinazouzwa ovyo madukani aina ya Parnina na Hybrid ya Kenya, tunaomba kwa sasa ufuatiliaji wa uingizaji mbegu hizi, kwani zinaharibu sana zao hili kwa kutoa mahindi zeruzeru yasiyo na uzao kabisa hata ukitumia mbolea.

Tano, katika Jimbo la Mbozi Mashariki maeneo mengi ya kilimo hayatoshi. Shamba la mahindi la Magamba limezungukwa na Vijiji nane na wananchi wanalilima kwa kulikodi kwa Sh.10,000/=. Ninaomba wafikiriwe wananchi wa Vijiji hivyo na wako tayari kulichangia na kulilipia kama itabidi kwa uzalishaji wa mahindi, maharagwe na kahawa.

Sita, maeneo ya umwagiliaji ni mengi, hasa Itaka, Namwangwa na mengine kama Kamsamba kwa kutega maji ya mito. Naomba Mtaalam usaidie kuyawezesha maeneo haya yazalishe zaidi. Zipo skimu ndogo ndogo ambazo wananchi wamechepusha maji ya mito na uzalishaji wake ungezidi zaidi kama yangepata msaada.

Saba, Wilaya ina tatizo la upungufu mkubwa wa Wagani wa Kilimo. Naomba Wizara itusaidie sana ili utalaam uwe ndio msingi wa uzalishaji. Zao la ufuta linastawi vizuri katika Tarafa ya Kamsamba. Kwa hiyo, kama kutakuwa na uhakika wa soko, basi

zao la ufuta lingeweza kubadili hali ya maisha ya wakulima wa eneo hilo. Tunaomba msaada wa kuwawezesha wananchi kwa mbegu na masoko.

Nane, tunaomba madawa ya kuzuia bungua wa mahindi zipatikane ili kuwa na uhakika wa kuhifadhi mazao, ziwafae wananchi. Mbozi iko mpakani mwa Malawi na Zambia. Kwa hali hii, uingizaji wa madawa feki ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba udhibiti wa madawa feki ya kuhifadhi mazao na kupulizia wadudu waharibifu wa mazao ya chakula na biashara yachukuliwe umuhimu wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba sana msaada wa Wizara kwa kutumia Vituo vyetu vya utafiti itusaidie kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJI SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri sana katika Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula mwaka huu kutenga Sh.10,099,598,500/= kwa ajili ya Umwagiliaji na Huduma za Kiufundi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shabaha nzima ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji ni kutaka Sekta ya Kilimo iweze kuchangia ipasavyo katika kuendeleza uchumi na kuondoa umaskini na ukue kwa zaidi ya asilimia 10. Ili shahada hiyo ikamilike kwa kutekelezeka, ni muhimu miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji imwezeshe mkulima kuwa na mfumo wa kilimo wa ama *double cropping* au *multiple cropping*.

Kwa miundombinu inayojengwa sasa, kilimo cha umwagiliaji kinafanyika wakati wa mvua za vuli au mvua za masika. Kipindi hicho cha mvua inaponyesha, haja ya kilimo cha umwagiliaji kinafanyika kimsingi huwa haipo na hata kama ikiwepo mkulima atalima kilimo cha *mono cropping* tu, kwa sababu mvua zinapokwisha kwa kawaida kina cha ujazo wa maji ya mto kinapungua na upunguaji huo unafanya maji katika *surface canal* nayo kupungua hali ambayo inapelekea eneo kubwa lililolimwa na kupandwa kukosa maji na hivyo kubaki *fallow*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, kama miundombinu ya umwagiliaji itakayojengwa kwa fungu hili la fedha lililotengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na huduma za kiufundi itafuata mfumo wa zamani. Kwa maoni yangu miundombinu hiyo ya umwagiliaji haitatosheleza kuwa na *impact* katika kilimo cha umwagiliaji kutosheleza *double cropping* au *multiple croppin*g. Kwa ajili hii, nashauri *if the Ministry of Agriculture and Food is to follow the Asian lead* ikubali Idara ya Huduma za Kiufundi ifuate mtindo wa miundombinu ya *South East where tube wells or dams* zimejengwa ku-*supplement surface canal water'*wakati wa kina cha mito kinapopungua.

Mheshimiwa Spika, nimeona pia katika *River Basin Management and smallholder irrigation improvement* imetengewa katika Bajeti ya mwaka huu Sh.200,000,000/= fedha za ndani. Inaposemwa *smallholder irrigation improvement* na *River Basin Management* ieleweke kuwa *Smallholders* ndiyo wazalishaji wakubwa katika Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, Sh.200,000,000/= haziwezi kuwezesha uzalishaji wa Sekta ya Kilimo kukua kufikia asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji katika nchi yetu kinalenga sana katika kuinua uchumi wa *smallholders*. Kwa hiyo, inapoelezwa *smallholder irrigation Improvement* na *River Basin Management* Wizara ya Kilimo na Chakula ifafanue kwa hawa *smallholders* nini maana ya *Economic Function, Financial function* na *Social Function* ya kilimo hiki cha umwagiliaji. Pia, ieleze kwa hawa *smallholders. If the total rainfall plus irrigation water are insufficient to leach the residual salts from the crop root zone, salt concentrations will in time build up to harmful units however small the quantities of salt that were brought in at each irrigation.* Nashauri Wizara ya Kilimo na Chakula *in planning irrigation development, provision has to be made for leaching of existing and future deposit of salt and adequate control of ground water table must be managed to restrict upward movement of salts.*

Mheshimiwa Spika, najua shabaha moja kubwa ya *irrigation schemes* ni ku-s*ettle landless farmers.* Shabaha hii huchukuliwa *largely on the basis of what could be achieved by irrigation. In this approach the nature and magnitude of the employment problem is all important* lakini nionavyo, *the merit of the means selected to solve the problem escapes careful economic scrutiny* kwani ni muhimu sana zikapata *economic analysis.* Kwa ajili hii, Wizara itoe maelezo kwa *smallholders* kuwa *economic impact of irrigation schemes should be judged largely on their direct costs and returns.*

Mheshimiwa Spika, najua *in the rush* ya kuongeza na kupanua na kuleta mageuzi katika kilimo, naona ipo hatari ya kilimo cha nchi yetu ku-*over look or relegate economic consideration and thus farmers banquet may turn to be simply and engineering picnic.*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana Wizara ya Kilimo na Chakula ku-*develop interest in protecting the soil from either water logging or salivation because salivation of soil surface is serious a consequence of upward movement of salt bearing water from the water table.*

Mheshimiwa Spika, *irrigation project should include leaching component to ensure that sufficient water passes the soil to depress salt toxity.* Kwa ilivyo sasa, uzoefu unaonyesha miradi yote ya miundombinu ya umwagiliaji hujengwa bila kufanyika *lining* na ikimalizika huachwa kwa wakulima bila wakulima kupewa elimu ya uchumi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji. Nashauri kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka huu katika jedwali Na. 6 inayohusu matumizi ya kawaida, Serikali imetoa fungu la huduma za kiufundi. Badala ya huduma hizo kuangalia huduma za miundombinu inayohusu *engineering* ya umwagiliaji peke yake, nashauri huduma za kiufundi pia ihusishe na miundombinu ya uchumi wa Kilimo cha *irrigation*. Nashauri hiyo kwa sababu s*everal of the technical issues considered in water resource planning have*

*important economic implication* kwa mfano *where and when to release irrigation supplies, how to cope with peak demands how to integrate individual project areas to achieve main benefits and how to benefit from the new agricultural technology.*

Taarifa kama hii ni muhimu katika kilimo cha umwagiliaji. Lakini muono wa *Engineering Work* katika *Irrigation Scheme* peke yake hautakuwa na manufaa kwa mkulima kama atakosa kuwa na elimu ya uchumi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, *if the total rainfall plus irrigation water are insufficient to leach residual salts from the crop root zone, salt concentrations will in time build up to harmful units however small the quantities of salt that are brought in at each irrigation* kwa ajili hii katika fungu la Huduma za Kiufundi. Nashauri, *in planning irrigation development, provision has to be made for leaching of existing and future deposits of salt, and groundwater table must be arranged to restrict upward movement of salts and ensure that sufficient water passes through the soil to depress salt toxity.*

Mheshimiwa Spika, nimeona pia *research development* imetengewa katika Bajeti ya mwaka huu fedha za ndani Sh.571,339,990/= na *Eastern Zone Client Oriented Research and Extension* imetengewa fedha za nje Sh.827,400,000/=

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu, *the biggest single constraint is the difficulty in establishing effective extension system* na pale ambako kuna *poor record of research,* hoja ya kuwekeza katika *extension appears to be weak.*

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengewa kwa ajili ya *research extension* ni ndogo sana. Kiasi hicho cha fedha hakiwezi kuwawezesha watafiti wetu kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Kwa kawaida *a more successful research effort is likely to require the use of extension staff in generating information on existing practices and how should these influence research design and recommendation.* Kwa sababu ya fungu dogo lililotolewa litasababisha kuwa na *weak link in extension organization* na kukosa *transfer of useful information on farm operations and the transfer of this information through the extension service and the research station.*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya umuhimu wa kitengo hiki cha *extension*, napendekeza Wizara ya Kilimo na Chakula ianzishe Uwakala wa kazi hii ya *extension*. Kwa utaratibu wa sasa *extension officers* wote wanawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, lakini Maafisa Ugani walio wengi hawaifanyi kazi yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka huu nimeona upo mpango wa kuimarisha shughuli za mafunzo kwa wakulima na wataalam katika ngazi ya shahada ya uzamili *(post graduates)* na shahada ya falsafa. Huu ni mpango mzuri sana na hivyo utekelezaji wa mpango huu nashauri uwe chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula moja kwa moja badala ya utekelezaji wa mpango huu huachwa kusimamiwa na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpango huu unakusudia kuondoa umaskini na kuongeza ajira, naIshauri Serikali ieleze Wizara yenye jukumu la kuondoa umaskini na Wizara inayosimamia ajira, nazo zihusishwe katika mpango huu kwa maana ya kuchangia fedha kwa Wizara ya Kilimo na Chakula katika kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mpango huu ni mzuri sana, kwa sababu kilimo chetu kwa sasa kinategemea sana wakulima wasio na taaluma ya kilimo kipana cha kitaalamu. Kwa hatua ya kuhusisha *graduate farmers* kutaongeza ajira kwa vijana wetu wanaomaliza elimu ya Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu. Vile vile, mpango huu utasaidia sana kupanua Elimu ya Ugani *(extension services)* kwa wakulima watakaokuwa wanalima kando kando ya mashamba hayo ya *graduate farmers.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri unaovutia wa mpango huu, nashauri kabla ya kuanza kuutekeleza Wizara ya Kilimo na Chakula ianze kwanza kufanya maandalizi ya ujengaji wa miundombinu yake. Kwanza mashamba lazima yaandaliwe kwa maana mashamba hayo kwanza lazima yalimwe. Pili, lazima miundombinu ya maji ijengwe, tatu, uwepo mpango wa kuwajengea nyumba za kutosha familia ya baba, mama na watoto wawili, nne, uwepo mpango wa kuwakopesha fedha na wapewe muda wa miaka mitatu kabla ya kuanza kulipa. Mkopo huo uwe na riba isiyozidi asilimia tatu. Pia, mpango ujenge miundombinu ya umwagiliaji ama kwa kutumia mabwawa, mito, *tube wells* au kutumia *micro drip irrigation.*

Mheshimiwa Spika, kama nilivosema awali, mpango huu ni mzuri sana kwa sababu utaongeza chakula na kuwezesha kufikia lengo la asilimia 10 ndani ya kipindi kilichowekwa. Mpango huu pia utapanua Elimu ya Ugani kwa wakulima kwa kasi kubwa sana kwa sababu *graduate farmers* wataeneza kwa haraka kilimo cha kitaalamu kwa wakulima. Lakini ni vizuri Serikali isiachie utekelezaji wa mpango huu kwa Wizara moja tu ya Kilimo na Chakula, kwa sababu mafanikio ya mpango unahusisha Wizara yenye dhamana ya kazi kuondoa umaskini na kupanua ajira, Wizara ya Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono Bajeti hii ya Wizara ya Kilimo na Chakula, lipo jambo moja nashauri Wizara ya Kilimo na Chakula ichukue hatua za haraka kulitatua jambo hilo linalohusu Wizara ya Kilimo na Chakula kushindwa kuwalipa mshahara wafanyakazi wa mashamba ya mbegu ya Msimba na Mwele/Mramba.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa nilizonazo sasa, imefikia zaidi ya miezi sita wafanyakazi wa mashamba haya yanayozalisha mbegu hawajalipwa mishahara yao. Tatizo hili likiachwa bila kutatuliwa haraka linaweza kabisa kuathiri uzalishaji wa mbegu na itapelekea wakulima kukosa mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye Sekta ya Kilimo. Pia, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji, kwa kuwa nchi yetu ina mabonde mengi ya umwagiliaji yakiwemo mabonde ya Matomondo, Inzomvu, Godegode, Msagali, Lumuna, Malolo, Mbuga Wilayani Mpwapwa na hivi sasa kuna mradi mkubwa unajengwa katika Kijiji cha Msagali kwa gharama ya zaidi ya Shilingi milioni 400. Mradi huo ukikamilika Wananchi wa Msagali watanufaika sana kwa kilimo cha umwagiliaji na kuondoa tatizo la njaa katika maeneo hayo. Mradi huo umechukua muda mrefu bila kukamilika. Je, ni sababu zipi zinafanya mradi huo usikamilike hadi sasa? Je, fedha kiasi gani zimelipwa kwa mkandarasi huyo? Je, Serikali imeweka mikakati gani kuhakikisha kwamba mabonde yote yanalimwa hapa nchini ili kuondoa tatizo la njaa? Je, ni mabonde yapi yanalimwa na yapi ambayo hayajalimwa kwa hekta zote zilizopo za mabonde hayo? Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa Bajeti ya mwaka 2005/2006?

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Vituo vya Utafiti: Je, ni Vituo vingapi vya utafiti vimefanyiwa ukarabati na kuwekewa vifaa vya kisasa *computer*, mawasiliano ya simu, matrekta kwa ajili ya kilimo na nyenzo nyingine za kufanyia kazi? Je, Serikali imetumia fedha kiasi gani kwa shughuli za ukarabati? Je, katika ukarabati huo na nyenzo za kufanyia kazi Vituo vya Utafiti vya Hombolo na Makutupora vimo katika utaratibu huo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri kwa Maafisa Kilimo: Je, Serikali ina mpango gani kuwapatia usafiri Maafisa Kilimo wote nchini na Wilaya ya Mpwapwa?

Mheshimiwa Spika, maslahi ya watumishi wa Sekta ya Kilimo: Je, Serikali ina mango gani wa kuboresha maslahi ya watumishi wa Sekta ya Kilimo na Serikali itafanya lini *job evaluation* ya watumwa wake na kuboresha maslahi na hii itasaidia kuboresha utendaji wa kazi.

Je, ni watumishi wangapi wamepandishwa vyeo katika kipindi cha Bajeti ya mwaka 2004/2005? Je, wamekwishalipwa au kurekebishiwa mishahara yao kulingana na vyeo vipya? Ni sababu zipi zinazofanya watumishi wa Wizara hii kukaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo na hawana tatizo lolote kikazi?

Je, Serikali imejiandaaje kutatua tatizo la upungufu wa chakula katika Mkoa wa Dodoma ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Charles Keenja Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Waziri wake na

Katibu Mkuu Ndugu Ngirwa kwa jinsi walivyoiandaa Bajeti hii. Wote hao pamoja na watumishi wote wa Wizara, wanastahili pongezi. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zote hizo za Wizara, bado yapo mambo ambayo ingefaa Wizara iyatafutie majibu ili kufanikisha kazi nzuri katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, bado ninaona nia ya Serikali kuzipa madaraka Wilaya, umeanza kuacha mwanya wa utendaji kazi kati ya wataalamu wa Wizara na wale wa Halmashauri. Uwajibikaji unazidi kudorora na hata utaalamu una kila dalili ya kupungua kwa kukosa *linkage*. Ipo haja ya kuangalia upya muundo wa utendaji wetu kati ya Wizara ya Kilimo na ile ya TAMISEMI ili kila mmoja apendekeze njia nzuri ya kuimarisha utendaji bora.

Katika Mkoa wa Rukwa, pamoja na kuwa ni Mkoa wa uzalishaji sana wa mazao ya chakula, lakini miradi michache ya kilimo imekuwa haijapata msukumo unaostahili. Je, Wizara inaweza kuelezea ni miradi mingapi ya Wizara ya Kilimo iliyomo Mkoani Rukwa na nini mafanikio yake?

Fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya ruzuku kwa ajili ya gharama za kusafirishia mbolea hadi Mikoani: Je, kwa nini zisifikie katika ngazi ya Wilaya na baadaye kwa kupitia moja kwa moja kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika. Pia, tunaiomba Wizara iwahi kuleta mbolea. (Wakati wa mavuno ndiyo mzuri wa kuleta mbolea maana watu wana fedha).

Ununuzi wa mahindi mwaka huu ni kidogo sana ukilinganisha na uzalishaji unavyozidi kuongezeka katika Mkoa wa Rukwa. Je, Mkoa wa Rukwa utakuwa na mgao gani wa hizo tani 41,000? Je, mahindi yaliyoko Rukwa tani 32,000 zitaondolewa lini ili kutoa nafasi ya kununua tena mahindi mengine ya msimu huu wa mwaka 2005/2006?

Mheshimiwa Spika, bado suala la maslahi na hata malimbikizo ya madeni kwa baadhi ya watumishi yameendelea kuwa ni kero. Je, Wizara ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo ambayo imekuwepo kwa muda mrefu hivi sasa kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya miundo ya Wizara yenyewe? Ni kwa kiwango gani hadi sasa marekebisho ya hali hii yamefanikiwa?

Mheshimiwa Spika, mikopo ya pembejeo imeendelea kukusanywa. Napenda kuwapongeza wahusika wote, walijitahidi kukusanya madeni hayo. Ningeshauri jitihada hizo ziendelee na kuanzia sasa Halmashauri zetu za Wilaya zishirikishwe kuona njia nzuri za kufanikisha matumizi bora ya fedha hizi za mkopo wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, suala la mbegu bora lingepewa kipaumbele katika kuongeza uzalishaji wa mazao yetu. Hivyo fedha za utafiti wa mazao zipewe umuhimu wa kutosha, ili tusije tukakosa mbegu bora mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wote, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam, Maafisa na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni leo hii.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hotuba hii kwa kuelezea kuwa Sekta ya Kilimo ilikuwa kutoka asilimia 2.1 hadi asilimia 6.0 kutoka mwaka 1994/1995 na mwaka 2004/2005. Ninaipongeza sana Wizara hii kwa ukuaji huu na ninaomba iendelee kusimamia na kuiongoza Sekta hii ya Kilimo ili iweze kupiga hatua zaidi na kuongeza ukuaji wa sekta hii kwa asilimia kubwa zaidi ili kuleta maendeleo ya kweli ya Taifa letu hili la Tanzania na kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vilevile niombe Wizara kuisimamia sekta hii vizuri zaidi kwa kuwapelekea wataalamu wake wote wa ndani ya nchi na hata kutoka nje katika Wilaya na Vijijini mwetu ambako ndiko kwenye maeneo ya kilimo na wakulima.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara hii na wataalamu wake wasimamie vizuri suala zima la kilimo kwa kutoa taaaluma iliyo nzuri kwa wakulima wetu ili waweze kuzalisha mazao yaliyo bora hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimefarijika sana kuona katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kuwa uzalishaji wa chakula hapa nchini umeongezeka kutoka tani milioni 7.7 mwaka 1994/1995 hadi tani milioni 9.79 mwaka 2004/2005. Kwa kweli ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa ujumla kwani ongezeko hili linatuondolea hofu kubwa ya nchi yetu kupata balaa la njaa lenye kutisha na ambalo linaweza kuhatarisha maisha ya wananchi wa Tanzania na Taifa kwa ujumla. Ninaomba Serikali kutoa taaluma iliyo nzuri ya kutunza chakula kwa wananchi walioko Vijijini ambako ndiko kwenye wakulima na wazalishaji wakubwa wa chakula hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tukisoma hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, pamoja na hotuba nyingi ambazo tayari zimeshawasilishwa hapa Bungeni, kwa kweli hakuna anayeweza kubisha juu ya umuhimu wa suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ni muhimu sana kwa Taifa letu, kwa hivyo ni lazima tuwe makini sana katika kulisimamia vizuri kwa faida na maendeleo ya Taifa letu. Tunaelezwa kuwa Sekta ya Kilimo inatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kilimo kinachangia asilimia 48.8 ya pato la Taifa, vilevile kinachangia asilimia 66 ya mapato ya fedha za kigeni na pia kutoa ajira kwa asilimia 70 ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hapa tukiangalia utaona umuhimu wa suala zima linahusiana na kilimo. Ni vizuri tukaacha mzaha na ubabaishaji tuongeze juhudi kuimarisha kilimo hapa nchini kwa kuwawezesha wakulima wetu na pia kuwataka wataalam wetu waende

kwa wakulima Wilayani na Vijijini ili kuwaongezea taaluma iliyo bora zaidi ya uzalishaji wa mazao yaliyo bora ili yaweze kuongeza pato la Taifa na pia kuongeza mapato ya fedha za kigeni kutoka asilimia hii ya 66 hadi asilimia 80 na zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama tutaongeza uzalishaji wetu hapa nchini na kama tutaweza kuongeza asilimia zaidi ya upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na kilimo kutoka mapato haya ya asilimia 66 ya pato la fedha za kigeni, tunaweza kupunguza utegemezi katika Bajeti yetu kwa asilimia 41.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa Serikali itachukua hatua zaidi kuongeza uzalishaji katika kilimo ili kuleta maendeleo zaidi ya nchi yetu na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia mchango wangu huu, ninaiomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulimaliza tatizo la mgomo wa madaktari wa Muhimbili kwa uangalifu sana. Ni vizuri Serikali ikakaa na madaktari hawa na kulimaliza suala hili kwa faida ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara hii ya Kilimo na Chakula katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, nashauri Wizara iwe na mkakati wa kitaifa wa kuziba mito na vijito vyote nchini ili maji yatumike kwa kilimo na matumizi mengine baada ya kuiacha.

Pili, Wizara iandae ramani ya kilimo ili kuonyesha sifa ya ardhi kwa nchi nzima na aina ya mazao yanayofaa tena kwa kila aina ya ardhi.

Tatu, Mabonde yote nchini kama Usangu, Dakawa, Kilombero, Pangani na kadhalika, yatumike kwa kilimo badala ya mifugo. Wakati umefika wa kugawa ardhi kati ya wakulima na wafugaji ili kuondoa migongano kati yao na kutumia vizuri ardhi.

Mwisho, naomba Serikali itoe ruzuku (usafirishaji wa mbolea) kwa mbolea za aina zote na mwaka mzima. Mtindo wa sasa unasababisha wafanyabiashara kuficha mbolea na kuiuza bei ya juu baada ya muda uliowekwa.

**MHE. MOSSY SULEMANI MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa rambirambi zangu kwa familia za waliofiwa na Wabunge wenzetu. Hapa cha kusema hakipo, ila tu ni kuwaombea roho zao ziwekwe Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuipongeza Wizara hii hasa wataalam wake kwa ushirikiano mkubwa waliompa yeye Mheshimiwa Waziri na Naibu wake katika kuiendesha Wizara hii kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, lazima Wizara hii tuichangie kwa mambo angalau kidogo. Kilio cha Watanzania ni namna gani Wizara hii ibuni njia mbadala wa kilimo ili Watanzania walio wengi waweze kufaidika na ardhi nzuri kama ajira binafsi? Maana halisi ya msemo huu ni kwamba kilimo cha wakati huu kibadilike na kiwe cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kumnukuu Balozi aliyemaliza muda wake kutoka Japan, Balozi Sato alisema: "Watanzania mtakamatana uchawi wa kiuchumi na msipozingatia Serikali pamoja na Mawaziri wa Fedha wa Kilimo mtawaona ni Viongozi wanaojitosheleza wenyewe bila kujali wanyonge ambao ni maskini wa kutupwa. Bila kuangalia upya kilimo chenu na kuitunza ardhi yenu nzuri aliyekupeni Mwenyezi Mungu." Mwisho wa kunukuu. Maneno haya aliyasema Morogoro muda mfupi kabla ya kuaga kurudi kwao na ilikuwa katika *pilot project* ya mpunga wa umwagiliaji.

Hii inamaanisha wataalam wa kilimo lazima wakea pamoja ili kupanga mkakati wa kuwekeza katika mabonde ya umwagiliaji kwa lengo la kukuza soko la nje.

Pamoja na utendaji mzuri wa kazi katika Wizara hii na wataalam wazuri waliopo Wizarani, haitaonekana ufanisi wake bila mpango mahsusi wa kuboresha kilimo cha umwagiliaji ambapo kikiboreshwa, naamini hata bajeti yetu haitakuwa tegemezi. Mfano; Angalia tu lile Bonde la Ruvu, kama litakuwa linazalishwa muda wote, bonde ambalo linatusuta tunapokwenda na kurudi safari zetu, hebu watalam *keep it up your professionals* nchi ibadilike.

Mwisho, Bunge lote litachangia hoja hii lakini zaidi itazungumzia suala kuonyesha Wizara hii haina matatizo pindi tu itakapobadilika kwenye kilimo, hifadhi ya maji na ufuatiliaji katika masuala ya mbolea.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa hotuba nzuri inayoeleweka na kulenga katika kilimo cha kumwondoa Mtanzania katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, ili kilimo nchini hapa kiwe cha maana na kuthaminiwa, ni lazima kwanza Watanzania waelimishwe kwamba kilimo ni mwajiri wao mkubwa kwa asilimia 80, hutoa pato kubwa la Taifa kwa asilimia 48 na wananchi wengi (85-85%) huishi Vijijini. Kwa bahati mbaya elimu hii imewekwa kama ni siri. Ni vyema ipelekwe mashuleni na itangazwe na vyombo vya habari licha ya majarida kuwekwa katika maktaba mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kilimo kuimbwa kwa karibu nusu karne kuwa ni Uti wa Mgongo wa uchumi wa Tanzania na uhai wa Watanzania, bado Serikali haijakipa umuhimu wa kwanza. Kilimo chetu hakitaendelea kutoka hapa kilipo maana hakuna watumishi hasa wa Ugani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupunguza *retrenchment* miaka iliyopita, wengine kustaafu, kufa na kadhalika, mapengo hayo hayakuzibwa nchi nzima. Wilaya ya Ngara

ina Kata 17 lakini Kata nne tu ndizo zina Mabwana Shamba. Wale wachache waliopo hawana usafiri kabisa. Kwa Wilaya ya Ngara iliyo na misitu, Kata kubwa na kukithiri kwa ujambazi wa wakimbizi wa Rwanda, Burundi na Congo, watumishi hawa hawawezi kazi. Wagani wachache nchi nzima hawana vifaa vya kutendea kazi na maelekezo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha kumwagilia ndiyo mkombozi wa Tanzania. Wilaya ya haijapata kuomba chakula tangu dunia iwepo. Kuna misimu mitatu ya mavuno ya nafaka na mazao aina ya mikunde. Msimu mmoja kati ya hiyo mitatu, Juni - Agosti ni kilimo cha kumwagilia mabondeni. Hata hivyo, pamoja na taarifa nyingi toka Ngara kuja Wizarani, pia ziara ya Wataalam wa Kanda na Wizara ikiwemo ya Mheshimiwa Prof. Mbawala - Naibu Waziri, Desemba, 2003 ambaye alishuhudia wingi wa mabonde mapana, marefu na yenye maji mengi ya kudumu, kama vile Bigombo, Mpanula, Mwiruzi Nyakabande Ntobeye, Chivu, Nzaza, mabonde ya Mto Kagera na Ruvubu, bado taarifa za Ngara zimepuuzwa. Ngara haikupewa *scheme* yoyote. Nimeambiwa kuwa Ngara ni mbali. Maana yake ni nini ikiwa Ngara ni sehemu ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, Wizara haimsaidii mkulima maana haimfikii. Ofisi za Wilaya ni budi ziwe na Maktaba ili matokeo ya utafiti yasomwe na watumishi na wakulima Wilayani na Mikoani.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha Adamu na Hawa kinachoendelezwa Tanzania ni kebehi kwa wakulima na aibu kwa Serikali yetu baada ya miaka takribani 44 ya uhuru wetu. Serikali lazima ikubali kushauriwa kwamba ni kilimo cha kisasa cha mashamba makubwa na cha kumwagilia ndicho kitaleta tija.

Mheshimiwa Spika, matrekta ni muhimu sana kuwawezesha wakulima, siyo kuwa Serikali inafanya biashara. Kwa mfano Wilayani Ngara kuna vituo vitano vya mafunzo kwa wakulima *(Farmers Training Centres)* visivyo na kazi, kumbe yapo majengo ya kudumu na ardhi kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iviimarishe Vituo hivyo na vingine viwe *Farm Mechanization Centres* ili wakulima na wafugaji waelimishwe na kukodi matrekta, walime.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ishawishi wawekezaji katika kilimo kikubwa hasa katika Mikoa ya Magharibi ya nchi; Kagera, Kigoma na Rukwa, mvua zake ni za kuaminika na za miezi mingi ya mwaka. Mazao ya aina nyingi kwa chakula na biashara yanastawi na Serikali inafahamu. Kinachotakiwa ni Serikali kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Ngara inayo nafasi nzuri kwa wawekezaji katika kilimo cha kahawa, ngano, mpunga maharage, migomba, mahindi, karanga na kadhalika bila kusahau mboga na matunda. Miundombinu na vivutio sasa vipo Ngara, mawasiliano/uchukuzi, umeme, uwanja wa ndege mzuri, mapori ya wanyama na mandhari ya milima, mito ya Kagera na Ruvubu, maporomoko ya Rusumo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mkulima hataweza kuondokana na umaskini kwa sababu kilimo chake ni *subsistence*. Ni *subsistence* kwa sababu hana mtaji. Mkulima hana mtaji kwa vile hana dhamana ya kuombea mkopo toka vyombo vya fedha. Serikali inapongezwa kwa kuifanya ardhi iwe mtaji/dhamana lakini mkulima wa kawaida hatatumia ardhi kwa wepesi. Serikali inashauriwa kufungua Benki kwa makusudi kabisa ili mkulima na mfugaji wapate kimbilio kwa kilimo chao kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Wizara za Kilimo na Ushirika na Masoko zikiunganisha juhudi kufungua Benki ya Wakulima na kuongeza na kuimarisha *SACCOS* nchini, kilimo kitapata sura mpya. Hapa vijana wengi wanaohitimu Shuleni na Vyuoni, pia wakulima Vijijini na watumishi wastaafu wataamka, watafumbuka macho na kuachana na kasumba ya kuzika mitaji midogo na viinua migongo katika biashara ndogondogo ambazo zimeshamiri Mitaani.

Mheshimiwa Spika, biashara hizi zimekuwa nyingi na zinakufa haraka sana maana wenyewe hawana ujuzi wa biashara. Kinachofuata ni wafanya biashara kufa haraka hususani wastaafu ambao ni akiba kwa busara na hekima zao.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Wizara ibuni maarifa ya kupeleka mbolea moja kwa moja Wilayani walipo wakulima. Mikoa na Wilaya za mbali hazitanunua mbolea kwa mtindo wa sasa maana gharama za uchukuzi kupitia Mikoani, pia ucheleweshaji usiolingana na majira halisi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Bajeti ya Kilimo na Chakula.

**MHE. SIJAMINI MOHAMMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa na huzuni kubwa kwa msiba huu mzito ambao ni kazi yake Mungu isiyo na makosa kwa kifo cha mwenzetu aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum CCM, kupatwa na kifo cha ghafla Mheshimiwa Margareth Bwana kilichomfika asubuhii hii ya leo tarehe 23/6/2005.

Nawapa pole sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara nyingine kumpoteza mwenzetu katika kipindi hiki kifupi. Tuwe wapole sana na Mola ampe malazi mema, Peponi. Aidha, naomba wawe na subira familia ya Marehemu na marafiki na wenzake wote kwani *"Inna lillahi wa inna ilaihi Rajiwn."*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kwa ufupi sana niipongeze hotuba hii nzuri ambayo inaeleweka na kila mwanadamu mwenye akili timamu, hotuba ambayo imejaza maudhui ambayo yako wazi.

Aidha, naomba nichukue fursa hii maalum na kwa makusudi kabisa niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wale na Wasaidizi wao wote kwa namna ambavyo wanafanya kazi kwa pamoja na utayari wao wa kuwatumikia wananchi na wakulima wa Tanzania, kazi ambayo kwa bahati mbaya inategemea hali ya hewa inayopangwa na kudra ya Mungu ambayo mwanadamu hana uwezo wa kuiandaa wala kuipanga.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba sana Serikali yetu ya Muungano kwa makusudi kabisa ifanye utaratibu wa kuiwezesha Wizara hii ya Kilimo na Chakula iwe inafanya mambo yake kwa kuwa karibu sana Wizara ya Kilimo ya Zanzibar kama zilivyo Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Utalii na Wizara ya Elimu katika kushauriana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa katika *scheme* zinazogharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa msaada wa chakula *(Food Aid Counterpart Fund).*

Mheshimiwa Spika, nashauri hili kwa kuwa Zanzibar ni visiwa vyenye maeneo madogo ya ardhi ya kilimo tofauti na huku Bara na ni imani yangu kuwa kwa namna ambavyo Wizara hii inafanya kazi ni dhahiri mfumo huu ukiwepo Zanzibar, wananchi watakomboka na suala zima la uchache wa chakula hasa mchele.

Mheshimiwa Spika, ni budi niipongeze Wizara hii katika kuichagua Zanzibar hasa Wilaya ya Kaskazini ingawa si Jimbo langu la Kitope katika mradi shirikishi wa kilimo, kitu ambacho nategemea huko tuendako wananchi wangu wa maeneo halisi ya kilimo ya Kilombero, Upenja watapata fursa hii kama wenzao.

Mheshimiwa Spika mimi kwa hakika ninaridhika kabisa na mfumo mzima wa kuinua kilimo Tanzania na kwa maana hiyo ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuyapitisha matumizi haya waliyoomba yote bila kikwazo chochote ahsante.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ninao ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa umakini wake. Hifadhi ya chakula *SGR*, hivi ni kwanini pamoja na Wizara ya Kilimo kuhimiza kilimo cha mtama *SGR* hainunui na kuweka kwenye Hifadhi ya Chakula na kupata soko la uhakika kwa wakulima wa mtama ambao hauliwi sana na dumuzi? Wananchi hawatuelewi kabisa kwa suali hili.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo cha umwagiliaji maji kwa kuziba mito ili maji yaende kwenye majaruba ya mipunga badala ya maji hayo kupotea ovyo. Naomba miradi iliyoanzishwa kwa Jimbo langu ya Ibadakuli (Bugweto), Mwamalili (Seseko), Kizumbi (Mwamashele), Ngokolo (Ndembezi) na Mwawaza (Negezi). Ninaomba sana miradi hii ikamilishwe. Wizarani ulishatuma wataalam wako kuja kuiona miradi ya Bugweto, Seseko na kadharika, naomba zipatikane fedha za kujengea mitaro hii ili kuifanya iwafaidishe sana wananchi.

Naomba Wizara itoe kwenye Manispaa yetu angalau Sh.100,000,000/= kwa miradi hii ili kupambana na njaa na umaskini. Wakulima wako tayari kushirikiana na Serikali.

Naomba kwa mara nyingine tena Serikali itupatie mbegu za ufuta angalau tani 10 kwa ajili ya kuwapatia wananchi zao mbadala badala ya pamba. Pia, naomba mbegu ya

mtama tani 10 wenye suke refu sana kutoka Kituo cha Utafiti cha Ilonga. Mheshimiwa Waziri, nakuomba unisaidie.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha pamba na bei yake; baada ya kulegalega ushirika katika Mkoa wetu amekosekana mtu wa kuweka msimamo juu ya bei ya pamba. Kwa msimu huu msimu haujachangamka hata kidogo. Naomba Vyama vya Ushirika viimarishwe, kama pamba haitanunuliwa kwa heshima, wakulima wanaweza kukata tamaa.

Kilimo cha sasa badala ya matuta na *tyridges* (Masono) ni mbaya na kuharakisha kuharibu ardhi maana mvua zinaponyesha huzoa udongo mzuri hadi mtoni. Ni vyema kabisa kilimo cha namna hii kikapigwa vita. *Elephant glass* (Mabingo bingo) sharti yakarudishwa na kusaidia utunzaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba nisaidiwe suala hili la umwagiliaji kwa miradi niliyoomba.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu kwa msaada na nawatakia kheri na fanaka kwa utekelezaji wa malengo mliyojiwekea kwenye Bajeti 2005/2006.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kama nilivyoeleza mapema asubuhi, leo ndiyo siku iliyopangwa ya kumaliza mjadala huu. Kwa hiyo, tutakaporejea jioni, wenye hoja yao wataanza kuhitimisha hoja tukianza na Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu Mtoa Hoja mwenyewe, halafu Kamati ya Matumizi. Baada ya hapo tutaendelea na ratiba yetu kama ilivyopangwa ili Jumatatu tuingie kwenye Wizara inayofuata ya Ujenzi.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni.

*(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kwanza kutamka rasmi kuwa naiunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya mwaka ujao. Tunaiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Pili, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Namtumbo napenda kuungana na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi kwa familia na wapiga kura kwa misiba ya Wabunge wenzetu waliotutangulia mbele ya haki. Wabunge hawa ni Marehemu Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira wa Ulanga Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati wa Kasulu Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan

Diria wa Rahaleo na Marehemu Mheshimiwa Margaterh Bwana wa Viti Maalum aliyetuaga jana, Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa wote mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nachukua fursa hii kwa furaha na kwa dhati kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuteuliwa na CCM kwa kura nyingi sana kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM mwishoni mwa mwaka huu, hongera sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya uteuzi wake kwa kura nyingi zimepokelewa Tanzania kote kwa nderemo na vifijo ambayo ni kuashiria kupata ushindi mkubwa wa kimbunga hapo 30 Oktoba, 2005. Tunamtakia Mheshimiwa Jakaya Kikwete, mafanikio makubwa katika kazi nzito ya kuiongoza nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa Mkutano Mkuu kuidhinisha uteuzi wake kwa kuwa mgombea mwenza na nampa hongera sana. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa kugombea urais wa Zanzibar kwa awamu ya pili, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipe pia fursa ya kushukuru kwa namna ya pekee wafuatao, Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo na Mkuu wangu wa kazi ambaye amenifanya niboreke katika kutumikia umma kwa kuwa yeye ni mtu mwenye hazina nyingi ya uzoefu wa uongozi na utumishi mrefu wa umma. Aidha, nimenufaika sana kwa ushauri mwingi na maelekezo kazini mazuri aliyonipa na nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Napenda vile vile nimshukuru Katibu Mkuu Wilfred Ngilwa, Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na Asasi zilizoko chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula na watumishi wengine wote kwa ushirikiano na udugu ulioniwezesha kumsaidia Waziri wetu kutekeleza majukumu, nyote asante sana kwa misaada hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyie Waheshimiwa Wabunge wenzangu pia pokeeni shukrani nyingi za ushirikiano wenu, urafiki na kwa ushauri mlionipa humu Bungeni, Wizarani na katika majimbo katika kufanikisha kusimamia na kuendeleza sekta ya kilimo ambayo ni sekta muhimu katika kutekeleza mkakati wa MKUKUTA. Tutakiane heri katika Uchaguzi Mkuu ujao na hatimaye tukutane tena katika Bunge jipya hapo Novemba, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila bila kuwashukuru kwa dhati kabisa viongozi wote wa CCM Wilayani, Katani na katika Matawi yote Jimboni nikijumuisha wapiga kura wote wa Wilaya ya Namtumbo ambao ndio walionileta hapa Bungeni na kunipa heshima ya kuwawakilisha kwenu nyote huko Namtumbo shukrani nyingi ziwafikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa kusaidia kutoa machache ya ufafanuzi kutokana na michango mizuri na ushauri mzuri sana uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mengi yatajibiwa na Mheshimiwa mtoa hoja mwenyewe Mheshimiwa Waziri, lakini mengine yatajibiwa kwa maandishi na kwa yale nitakayochangia ni kama ifuatavyo:-

Kwanza nishukuru sana kwa pongezi tulizopata kwa kuendesha majukumu yetu katika Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa mwaka huu uliopita, asante sana kwa pongezi tulizopewa kama Wizara. Lakini hapo hapo napenda kusema machache ya ufafanuzi kuhusu kughushi takwimu, hili lilisemwa na Mheshimiwa mmoja, tunataka kusema hivi Wizara haighushi takwimu, kinachotokea ni kuwa kila sekta ina takwimu zake, kukua kwa takwimu katika sekta ya mifugo, sekta ya uvuvi, sekta ya ushirika na kadha wa kadha kuna asilimia zake za ukuaji huo. Kwa hiyo, ndio maana utaona kati ya *sub-sector* na sekta. *Sub-sector* kuna tofauti, lakini kwa ujumla takwimu ile ya sekta yote kama ilivyosema ni sahihi kabisa asilimia sita na kadhalika na vile vile nilitaka kutoa mfano, kwa kweli tukikuwa kwa sekta, kwa mfano kwa upande wa *irrigation* tumepiga hatua sana, mwaka 2001/2002 tulikuwa na hekta 191,900 na tani za mpunga zilizozalishwa ni 767,000.

Lakini mwaka huu uliopita tumekuwa na uzalishaji katika hekta 249 karibu 250,000 na kuzalisha mpunga tani 999,968, kwa hiyo, liko ongezeko la dhahiri kabisa na hiyo katika sekta mbalimbali ya pamba na mazao mengine. Kwa hiyo, tunachotaka kusema kuwa takwimu zetu ni za uhakika sio za kughushi na tuna kitengo maalum kinashughulikia masuala haya.

Vile vile tunaahidi kuendeleza na kupanua kilimo cha umwagiliaji maji kwa sababu huko mbele mipango iliyoko ni kuwa angalau kila mwaka azma yetu ni kutenga shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kupanua kilimo na hapo tutakuwa na *impact* kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

Kuhusu wastaafu, tunajua tatizo lipo lakini tatizo hili si letu sisi peke yetu linaanza huko Mikoani au Wilayani linafika Wizarani na hatimaye likifika Utumishi linaweza likakwama. Kwa mfano, mtu anapoanza kazi anaitwa Joseph Shija, lakini hapo katikati anaweza akaongeza tena akasema mimi ni Joseph Bundala Shija, sasa watakapoandika taarifa zake itaonekana kuna watu wawili, kuna Joseph Shija na kuna Joseph Bundala Shija, hawa wanaweza kuwa watu wawili tofauti, sasa tunawaambia rudisha tunataka uape na hii inachelewesha sana na wakati mwingine tu *file* lenyewe likionekana Joseph Shija, huoni Bundala basi unafikiri sio huyu, unazidi kutafuta na kutafuta.

Kwa hiyo, tunaomba kuwa na umakini sana katika kuandaa taarifa na wakati mwingine ikibadilishwa sana itabidi pengine hata kuapa kwenda Mahakama kuapa mimi ni Joseph yule yule Joseph Shija na baadaye niliongezea Bundala. Kwa hiyo, tunaomba masuala haya yakiletwa uwe na umakini fulani kusudi kurahisisha kazi hiyo ya kutoa mirathi. Hata hivyo Wizara imejitahidi sana, huko nyuma mpaka mwaka 1990 palikuwa

na tatizo kubwa sana la watu kupata *promotion* na mengineyo. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri jana ni kuwa watumishi waliopandishwa vyeo wamekuwa 1,474 na 392 waliothibitshwa kazini, 77 waliorekebishiwa ajira zao na 46 waliajiriwa upya. Kwa hiyo, tunachotaka kusema ni kuwa Wizara imejitahidi kutimiza wajibu wake kama mlivyoona.

Kuhusu suala la pamba Wizara inatambua umuhimu wa zao katika uchumi wa nchi yetu, tatizo la malipo kwa mwaka uliopita limetokea zaidi kwa makampuni machache na zaidi kwa vyama vya ushirika vifuatavyo; *SHIRECU, KACU, BSU* na *NSU Inyaza.* Hivi vyama vyote vya ushirika vilikopa toka *CRDB* fedha zipatazo bilioni mbili na milioni mia moja, sasa kwa bahati mbaya hela zile hazikurudi *CRDB* baada ya manunuzi na hivyo *CRDB* imeshindwa kukopesha upya hapo limeanza tatizo. Sio la Serikali yenyewe tu moja kwa moja na makampuni yako machache lakini hata hivyo bodi ya pamba imejitahidi sana kufuatilia madeni hayo kusudi kupunguza tatizo kwa wakulima wanaushirika, hadi sasa wamepata zaidi ya shilingi milioni 500. Lakini kama mnavyojua deni ni bilioni mbili na milioni mia moja, kwa hivyo tatizo lipo tunalitambua sasa ndivo lilivyo hali ilivyo mpaka sasa hivi.

Kuhusu *irrigationi,* nataka kusema tena *irrigation* imetiwa mkazo sana tangu mwaka 2001 mpaka kutengeneza *irrigation master plan* imefanyika kwa kipandi hiki na kuainisha karibu mabonde yote mliyoyataja yamo kwenye *irrigation.* Wakati ilipofika mwaka 2001 hivi tulijua tuna hekta zipatazo milioni *plus* lakini ule utafiti na *study* hiyo ya *irrigation master plan* tumegundua kumbe tuna hekta milioni 29, hilo nalo ni mchango mkubwa kwa Wizara yetu, tunaomba mtupongeze. *(Makofi)*

Vile vile tulianzisha miradi mingi ya *Green Belt* kuzunguka Ziwa ikijumuisha kule kwa mtani wangu Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Najua huko nyuma alivyochangia alisema kidogo kuwa mambo hayakuwa vizuri katika Wizara ya Kilimo na Chakula, kumbe kilichotokea ni hiki kilichomfanya yeye alifikiri Wizara ya Kilimo hatufanyi kazi pamoja na mimi mwenyewe kuwa tulipojenga ule mradi pale Chamgasa wengi walipendekeza tutumie mashine ya *diesel* lakini wataalam wa Wizara ya Kilimo wakaona sio vizuri kutumia *diesel* kwa sababu baada ya kukamilisha mradi wanakijiji wangepata taabu sana kupata fedha za kununua *diesel.* Kwa hiyo, wataalam wakapendekeza tutumie *wind mill,* mashine inayokwenda kwa upepo, lakini *wind mill* nzuri inapatikana Kenya. Zile taratibu za kuagiza mpaka kufika ilichukua muda mrefu kidogo, kwa hvyo Mheshimiwa Dr. Chegeni, akafikiri pengine tunazembea na ilipofika kuna chuo kimoja cha *air chamber* kilileta utata kidogo na kuunganisha, mtaalam alikuwa mmoja mwakilishi wa ile kampuni Kenya, nchini Tanzania ambayo anahudumia maeneo mengi tunawasiliana naye kutaka kumpata afike, ashughulikie suala hili na hivi tunaonekana tumechelewa sababu hiyo, tunaomba radhi na asifikiri kuwa sisi tunajaribu kuzembea hata tunatambua wajibu wetu.

Kuhusu mbolea, tatizo hili lilisemwa na Mheshimiwa kutoka Kigoma rafiki yangu Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, tunataka kusema hivi mbolea zilikuwepo kwa kila mkoa pengo lilikuwepo, lakini Wizara baada ya kuainisha wale ma-*agent* hao watakaouza mbolea kule, Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake zote zilitakiwa ziwe na

Kamati ya Mkoa na Kamati za Wilaya. Hizo ndio zingefanya mawasiliano na *centre,* kwa bahati mbaya ilivyotokea baadhi ya Wilaya inawezekana ikawa Kigoma unakotoka Mheshimiwa waliona jukumu hili ni la Wizara yenyewe moja kwa moja, si rahisi sana kufanya. Wengine waliunda hizi Kamati na zilifanya kazi vizuri, tatizo halikuwa sugu kiasi kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tunaomba radhi kwa usumbufu uliopata lakini tunaomba Mheshimiwa ikiwezekana tuzikumbushe zile Kamati za Mkoa na Wilaya ikumbuke wajibu wake wa kushughulikia masuala kuainisha ni nani atakaye kuwa wakala pale tulipo kama ni ushirika au mfanyabiashara binafsi au inawezekana kabisa ikawa mfuko wa pembejeo wa Mkoa na kadha wa kadha wakaleta zile mbole na wakazisimamia na hata usambazaji wake. Huo ndio utaratibu na tunaomba jambo hili lisimamiwe kwa uangalifu kama tulivyokwisha kulitaja na mbolea hasa zinazopewa ruzuku ni *UREA, DAP* pamoja na *CAN.*

Kuhusu huduma za *extension* tunatambua kama ugani ni huduma muhimu sana katika kuendeleza kilimo, sasa tangu mwaka 1998 kutokana na Azimio la Bunge lililopitisha kuwa watumishi waimarishwe katika ngazi ya Wilaya kwa hivyo watumishi karibu wote wa sehemu kubwa ya watumishi wako Wilayani. Kwa bahati mbaya watumishi hawana ratiba ya kazi na wala maelekezo jinsi ya kufanya kazi yao kila siku wakiwajibika kwa Halmashauri, kutokana na tatizo hili kuna uzembe na udhaifu.

Ushauri, ni kuwa ratiba za kazi ziwepo, zipitiwe na Halmashauri na Halmashauri isisimamie na ikiwezekana pawe na mkataba baina na *extension workers* au mtumishi wa ugani katika eneo husika akielezea mpaka mwisho wa mwaka atafanya hili, atafanya hili halafu anatia saini. Unakuwa mkataba yeye na Halmashauri, kusudi mwisho wa mwaka, mwisho wa kipindi anaulizwa mtumishi umefikia yale malengo uliyoahidi hapana, tatizo ni nini? Lakini hivyo leo wengi wako tu kule wanakaa bila ratiba na kadhaa wanategemea labda Wizara au Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wawasimamie, si rahisi sana kumsimamia mtumishi aliyeko Mikoani kutoka Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo nirudie tena kusema kuwa imekuwa furaha sana kufanya kazi katika Wizara ya Kilimo na Chakula na imefikia wakati sasa ndio tunatoa Bajeti na inabidi wengi turudi Majimboni tutakiane heri katika vinyang’anyiro huko na hatimaye tukutane na *Inshallah* Mwenyezi Mungu akitujalia tutakutana Novemba. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema haya naona nitoe muda mwingi zaidi kwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, aendelee kuelezea mengi kwa ufafanuzi wa sekta nzima ya kilimo na chakula na asanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Wabunge wenzangu kukupa pole na tunaomba utufikishie pole zetu kwa Mheshimiwa Spika, kwa kumpoteza tena ndugu yetu mwingine Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, jana tunawapa pole wafiwa na sisi wote tupeane pole na tumwombee Mwenyezi Mungu alaze roho yake mahali peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana na hakika Rais alikuwa anasikiliza mazungumzo yaliyokuwa yanafanyika hapa Bungeni na nina hakika atakuwa amefarijika sana kwa sababu kilichofanyika hapa ni kuangalia tatizo, kuangalia hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama cha Mapinduzi, kuangalia matatizo ambayo bado yapo na kutoa ushauri kwamba nini kifanyike ili kilimo kiendelee kuboreka. Nashukuru sana kwa mapendekezo na maoni mazuri sana yaliyopatikana kutoka kwenye kikao hiki, asanteni sana. *(Makofi)*

Kwa kipindi kilichobakia tutayafanyia kazi na wenzetu watakao tupokea nina uhakika watayafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinaendelea kukua na kinaendelea kuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ambazo sote tunazielewa hatukupata wazungumzaji wengi sana, lakini naomba niwataje wale ambao walizungumza. Mheshimiwa Musa Lupatu, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, namshukuru sana kwa maoni mazuri sana yaliyotolewa na Kamati na maagizo ambayo yametolewa na Kamati nitajaribu kufafanua baadhi kadri tunavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia ni Mheshimiwa Hamis Jumanne Nguli, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Dr. Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Paul Makolo na Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya tena, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Mossy Suleiman Musa, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa John Chiligati, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga na Mheshimiwa Christopher Wegga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote nawashukuru sana kwa michango yenu kwa kuzungumza hapa Bungeni na kwa maandishi, wako pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia wakati Waziri Mkuu alipowasilisha hoja yake hapa Bungeni, naomba nao niwataje, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa

Leonard Shango, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Dr. James Msekela na Mheshimiwa Lidya Boma. *(Makofi)*

Wakati wa hoja ya TAMISEMI walichangia Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa George Lubeleje. Hao nao nawashukuru sana na kadri muda utakavyoruhusu tutajitahidi kujibu hoja zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi 28 wamegusia eneo la umwagiliaji, kwa hiyo, naelekea ndio eneo lililopewa uzito mkubwa kuliko maeneo mengine yote na mimi nitajaribu kulipa uzito ambao linastahili. Lakini kabla ya kujibu hoja hii kuna hoja moja ambayo nimeletewa kutoka kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo ilitaka mfuko wa pembejeo uhamishwe kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula uende Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, sababu za pendekezo hilo sikuelezwa, lakini ningependa nieleze tu hivi kwamba huu mfuko ulianzishwa kama njia ya kujaribu kumfikishia mkulima mbolea na lengo lake lilikuwa ni kumwezesha *stockist* msambazaji wa mbolea apate mkopo wa kumwezesha asambaze mbolea. Huu mfuko haukuanzishwa kwa ajili ya kumkopesha mkulima mmoja mmoja na mpaka leo pamoja na jitihada zote tunazofanya hatujaweza kuufikisha hapo.

Kwa hiyo, kazi yake ni kuwakopesha *stockist* ili *stockist* waweze kufikisha mbolea kwa mkulima na *stockist* anaweza kuwa anakaa Dar es Salaam, anaweza kuwa anakaa Mkoa mmoja na anasambaza katika Mkoa mwingine, hilo ndio lilikuwa lengo la kwanza.

Lakini kutokana na matatizo ya kuwahudumia wakulima tumepanua huduma za huu mfuko ukawa unatoa mikopo ya matrekta, mikopo ya kutengeneza matrekta, mikopo ya dawa za kuogeshea mifugo na kadhalika kwa sababu hatuna chombo kingine cha kufanyia kazi hiyo, lakini tukubaliane kwamba mfuko huu ni tatizo zaidi kuliko msaada yaani katika chombo kinachonipa matatizo Wizara ya Kilimo na Chakula ni mfuko wa pembejeo, wanaokopa hawarudishi hata tulipopeleka benki wakikopa kutoka benki wakijua ni fedha za Serikali bado kurudisha kuna kuwa kugumu kwelikweli. Kwa hiyo, mfuko huu hauwezi kuwa ni jawabu la utoaji wa mikopo kwa wakulima, jawabu ni lile pendekezo ama agizo lililotolewa na Kamati ya Kilimo na Ardhi kwamba ianzishwe benki ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazi imekuwa ikifanyika, Waziri wa Fedha mwaka jana alitoa taarifa kwamba Serikali ipo mbioni kuanzisha benki hii ya maendeleo ya kilimo ambayo itaunganishwa huko na ushirika na masuala yote yanayohusika yalilikuwa inashughulikiwa na Wizara ya Fedha na Benki Kuu. Tutafuatilia kuhakikisha kwamba kasi ya kuandaa benki hiyo inaongezwa ili benki hiyo ianzishwe na vifedha hivi vya mifuko mbalimbali viingizwe katika benki hiyo iwe ndio chombo cha kuwakopesha wakulima na kwa hiyo, mfuko uache kuwepo.

Sasa hii ya kuhamisha mfuko ambao ni *transitional* ni mfuko tu wa muda ni mfuko wa mpito kutoka Wizara moja kwenda Wizara nyingine si jambo ambalo litatusaidia sana, isitoshe kwa maoni nafikiri kwamba hivi vyombo vinagaiwa katika

Wizara mbalimbali kulingana na mahitaji yaliyopo ya wakati na inaweza kuja Serikali ya awamu ya nne ikaamua kuwa na utaratibu wa tofauti kabisa na huu ambao tumeutumia katika awamu ya tatu. Kwa vyovyote vile ni mfuko wa mpito na sioni sababu ya kutupotezea muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo ambayo yamezungumziwa na nataka niligusie kidogo ni ukweli kwamba Serikali imekuwa ikiongezea sekta ya kilimo fedha, Wizara ya Kilimo na Chakula imekuwa ikipata nyongeza ya fedha kama ifuatavyo:-

Mwaka 2000/2001 tulipata 32 bilioni, mwaka uliofuata tukateremka tukaja 25 bilioni, mwaka uliofuata wa 2002/2003 tukapata 33 bilioni, mwaka 2003/2004 tukapata 54 bilioni, mwaka 2004/2005 tukapata 64 bilioni, mwaka huu kama Bunge hili Tukufu likipitisha makisio ninayowasilisha mbele yake tutapata 118 bilioni. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi pesa tumeongezewa chini ya MKUKUTA, huu mpango wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini, ndio uliosababisha hii sekta ya uzalishaji ikaongezewa fedha ili iweze kutekeleza malengo haya na mimi nafikiri kwa kweli Serikali imejitahidi sana, hasa tukikumbuka tulikotoka, maana tulitoka mahali pagumu kweli kweli ambapo upatikanaji wa fedha ilikuwa ni kazi ngumu kabisa.

Mimi naipongeza Serikali kwa hizi juhudi ambazo inafanya, lakini naomba iendelee kufanya juhudi hizi ili tufikie ile asilimia kumi ambayo wakuu wa *AU* walikubaliana Maputo. Kwa kiasi hiki cha fedha tulichopewa na ambacho kimepewa kwa Wizara nyingine za kilimo tumefikia asilimia 7.2, tunatakiwa tufikie asilimia 10 tufikapo mwaka 2007/2008, kwa hiyo tuko katika mwelekeo sahihi kuelekea kufikia kiwango hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pia Kamati ya Kilimo na Ardhi ilisema na wajumbe walizungumza hapa wapo wamesema kwamba kumekuwepo utegemezi katika mipango ya maendeleo maana kiasi ambacho kinatolewa kutoka kwenye bajeti ya Serikali kinaonekana ni kidogo na kiasi ambacho kinatolewa kutoka nje kinaonekana ni kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa niseme hivi katika fedha zinazotoka nje nyingi ni mikopo si misaada, kwa mfano tunapata pesa kutoa *ADB* bilioni nne, kutoka benki ya dunia bilioni tisa, kutoka *IFAD* kwa ajili ya *PIDP* ule mradi wa umwagiliaji bilini mbili, kutoka *IFAD* tena na benki ya dunia kuna ule mradi niliowaambia wa kuhamisha teknolojia kutoka kwenye vyombo vyetu vya utafiti kwenda kwa mkulima ni bilioni 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna zile fedha za *STABEX* ambazo zimezungumzwa sana hapa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na hata rafiki yangu Mheshimiwa Aggrey Mwanri amezigusia ambazo nazo ni pesa nyingi, kwa hiyo, hizi ndizo pesa zinazokuja kuunganishwa zikatupa kile kiasi cha shilingi 63 bilioni ambazo zinatufanya tuonekane kwamba ni tegemezi sana, lakini nyingi kwa kweli ni fedha ambazo tunakopa kutoka nje na wote ninyi mnajua kama unataka kuendelea hata kama

mtu binafsi inabidi utafute mikopo ya kukusaidia ili uweze kufikia malengo yako, kwa hiyo hali sio mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, amezungumzia kidogo hili suala la kukua kwa sekta ya kilimo. Mimi nafikiri lazima tufike mahali tujipongeze, unajua kilimo kinapokua kinatokana na juhudi zetu sisi wote humu, juhudi za wananachi, juhudi za viongozi wao wakiwepo Waheshimiwa Wabunge na mambo mbalimbali ambayo tunafanya. Sasa mkisema kimekua tu kwa sababu mvua zinanyesha kwani huko nyuma zilikuwa hazinyeshi? Mbona hakikukua, maana huko nyuma badala ya kukua kilikuwa kinashuka mpaka tukafikia asilimia 2.9 yaani ikawa *actually 2.1,* kilimo kikawa kinakua kwa kasi ndogo zaidi kuliko idadi ya watu. Sasa kinakua kwa asilimia 6 na sekta ndogo ya mazao inakuwa kwa asilimia 6.2, lazima tujipongeze kwa mafanikio ambayo tumepata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati tunajipongeza tukubali vile vile kwamba bado kazi ipo na hatujamaliza kazi. Mheshimiwa Aggrey Mwanri, anasema tunachofanya ni shughuli, bado hatujaanza kufanya programu ya kilimo, lakini shughuli ukiiweka kwenye makaratasi ukiandika vizuri inakuwa ndio programu. Kwa hiyo, anasema tunachofanya zaidi ni shughuli, bado programu hazijafanyika kwa hiyo, kazi bado ipo, lakini tumeweza kuongeza kasi ya kukua mpaka tukafikia asilimia 6.2, si haba. Tunafikiri sasa tuko njiani kuelekea, maana tunasema ili kilimo kiweze kutoa mchango wa kutosha kwenye kukuza uchumi na kuondoa umaskini lazima kikue kwa asilimia 10. Kwa hiyo, tumefika asilimia 6.2 tuko njiani kwenda kwenye asilimia 10 hiyo ili kitupe manufaa hayo tunayofikiri ndio yatakayotuokoa. *We are on course,* tusikate tamaa, tuendelee kujitahidi Mwenyezi Mungu akijalia siku itafika, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, anasema tunasali ili mvua ije na isipokuja inakuwa ni balaa. Naomba tuendelee kusali tupate mvua, maji yawe kwenye Mito na Maziwa tuyatumie kumwagilia ili tuweze kwenda vizuri zaidi. Wazungumzaji 28 wamesisitiza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na mimi nakubaliana nao *100 percent* wala sina haja ya kuongeza wala kupunguza katika yale waliyozungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Leonard Shango, raia wangu anakaa pale Temboni, nakubaliana na wewe *100 percent* kwamba ni lazima tuzuie yale maji yanayopita Iramba ambayo ni mengi sana wakati wa mvua ili tuweze kuyatumia wakati wa kiangazi. Hiyo kazi tumeanza na wewe mwenyewe umekubali kwamba kuna miradi ambayo imejengwa, unaitoa tu makosa kwamba haikusimamisha maji ya kutosha, nitarudisha wataalam wangu, wako hapa waende wakaangalie kwa nini hayo maji yako yanavuja. Lakini jitihada zimefanyika na nataka nisema hivi, katika maeneo ya ukame tutatoa umuhimu wa juu sana kuvuna maji. Kwa sababu yana kazi tatu, kazi ya kwanza ni matumizi ya binadamu, kazi ya pili ni matumizi ya mifugo na kazi ya tatu ni kumwagilia mashambani ili tuweze kuvuna. *(Makofi)*

Katika maeneo ya ukame usipovuna maji wananchi watakuwa na maisha magumu sana. Kwa hiyo, lazima tufanye kazi ya kuvuna maji, katika maeneo yanayopata mvua nyingi kwa mfano Ngara kwa Mheshimiwa Gwassa Sebabili na Mkoa wa Kagera, Kigoma na hii Mikoa mingine, jitihada zetu zitakuwa ni kutumia maji ya Mito na maji

yaliyoko katika Maziwa kumwagilia na kuvuna kutapewa umuhimu wa chini zaidi kuliko kutumia yale maji ambayo yapo tayari. Kwa hiyo, tutakwenda kwa *strategy,* lakini *strategy* ya tatu ni kuhakikisha kwamba tunaanza na miradi inayohudumia watu wengi kwa gharama ndogo halafu tunakwenda kwenye miradi ya gharama kubwa. Miradi ya umwagiliaji ni ghali sana na wale ambao wametekeleza rafiki yangu Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe angekuwa hapa angetuambia, atakubali kwamba inatumia pesa nyingi sana kuweza kuyachukua tu haya maji na kuyafikisha kwenye mmea.

Kwa hiyo, ukipata mahali ambapo unaweza ukahudumia wananchi wengi ni mahali pa kuweka fedha zako na pale ambapo gharama ni kubwa sana tutapafikia baadaye. Lakini tukubaliane kimsingi kwamba kama tungeweza kumwagilia hekta 29.4 milioni ambazo zinawezekana kumwagilia hali ya Tanzania ingekuwa tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi kwamba sisi wote tushirikiane kutafuta rasilimali za kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Ukienda ukikutana na mtu ambaye tunashirikiana naye katika kilimo mkumbushe kwamba jawabu letu la kilimo liko katika kuongeza eneo linalomwagiliwa maji mashambani. Sasa hivi tunamwagilia maeneo madogo mno na tukifanya hivyo tutapiga hatua kwa haraka zaidi kuliko ambavyo tumekuwa tukifanya.

Kwa hiyo, katika eneo hili kwa kweli halina ubishi ni eneo la kupewa kipaumbele na Serikali imekuwa ikijitahidi sana kulipa kipaumbele, mwaka kesho tutakuwa na shilingi bilioni 8 ambazo zitatumika kuboresha umwagiliji katika maeneo mbalimbali. Sasa ile miradi yote mliyotaja hapa huu haujakamilika, huu ni mbovu naomba mtukumbushe tuelekeze hizi shilingi bilioni 8 katika kufanya ile miradi ambayo imeshajengwa ifanye kazi kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo cha pamba, mwaka huu pamba imeongoza kwa mbali sana katika kutupatia fedha za kigeni, imetupatia pesa nyingi sana. Nakubaliana na Mheshimiwa Dr. William Shija, kwamba kuna matatizo mengine yasiyokuwa ya lazima katika zao hili na mengine yanasababishwa na sisi wenyewe, maana Vyama vya Ushirika si vyetu sisi wenyewe, ile nyongeza ambayo Serikali iliagiza mwaka jana karibu wanunuzi binafsi wote walilipa. Vyama vya Ushirika havikulipa, Vyama vya Ushirika mwaka jana vimekopa pamba na sasa hivi vinafuatiliwa vilipe. Nina hakika atakapokuja Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko hapa atatuambia hatua ambazo anachukua kuhusiana na vyama hivi ambavyo mwaka jana vilikopa havijalipa na vingine tuna matatizo navyo sasa hivi kwamba visaidiwa namna gani ili viweze kuendelea kununua pamba.

Kwa hiyo, baadhi ya matatizo kwa kweli ni matatizo ya usimamizi hafifu wa Vyama vya Ushirika na mimi naomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na kusimamia masuala mengine kwenye Majimbo yetu tusivisahau Vyama vyote vya Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile ni vyombo vya ukombozi kwa wananchi wetu kwa sababu vinaunganisha nguvu zao na kuwawezesha kufanya mambo makubwa. Kwa hiyo,

tusijiachie, tukafikiri ni vya wale waliochaguliwa peke yao, hapana ni vyombo vyetu na tusipovisimamia vinaweza kutuathiri na kuathiri maendeleo ya maeneo yetu, nitashukuru sana tukifanya hivyo, kwa hiyo, ni kweli kabisa. Lakini ningependa nieleze hapa kwamba Serikali imekuwa ikilipa hili zao uzito unaostahili na Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Ushirika na Masoko mwaka jana walitumia muda mrefu sana kuhakikisha kwamba wamefuatilia matatizo yale ya ununuzi wa pamba yaliyokuwepo. Lakini mtakumbuka hapa tulipokuwa tunapitisha Sheria ya Pamba mlikataza Serikali isiuze mali ya Bodi ya Pamba ili kulipa madeni, Serikali ikakubali, tukaondoa kwenye ile *draft* ya Muswada ule tulioleta Bungeni hapa. Nafurahi kuwaambia kwamba mwaka huu Serikali itamaliza kulipa madeni yote yale na kwa hiyo mali zetu za Pamba hazitauzwa. *(Makofi)*

Narudia tu kusema kwamba hii Serikali ya CCM ni sikivu kweli kweli. Wabunge mkisema inasikia na inakwenda kuweka mikakati ya kutekeleza. Kwa hiyo, mali zetu hazitauzwa ili kulipa madeni yale, mkikuta nyumba imeandikwa *Pamba House* ni nyumba yenu, ingieni kifua mbele bila wasiwasi.

La pili ni ruzuku ya mbolea tuliyotoa kwa kweli tulikusudia kiasi kikubwa kitakwenda kwenye pamba pia, nilitembelea Bariadi wakati mmoja nikawa *impressed* sana na *mechanization,* kule Bariadi kilimo chao kinafanyika kwa wanyama kazi na matrekta. Nilipokwenda kule waliniambia upungufu wao ulikuwa ni matrekta manne tu kukamilisha mahitaji yao ya mashine za kulimia. Lakini nitakuta kuna tatizo moja kubwa, *technology* ya kupanda na kutunza pamba mashambani ilikuwa ya chini kabisa. Waliniambia mtu anasimama mahali palipoinuka halafu unatupa hizo mbegu zitakakoanguka ndiko huko huko Mwenyezi Mungu azijalie zikue halafu tutakutana kwenye palizi yaani sijapata kuona *extremes* kubwa kama hizo, *technology* ya kulima kwa kutumia ng’ombe unakwenda kwenye shamba unakuta kuna seti 4, 8 zinalima, sehemu nyingine matrekta yanalima lakini tukija kwenye kupanda hali ni tofauti kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa naomba tutakapokwenda tufanye hili la kuhakikisha kwamba *technology* ya kupanda pamba na kuitunza inakuwa ya hali ya juu kabisa, kwa sababu unaweza ukaongeza uzalishaji kutoka kilo 250 za sasa mpaka kilo 1,500 na katika eneo lile lile kwa kutumia tu *technology* nzuri ya kupanda basi na kuna wananchi wanaofanya hivyo sasa hivi. Sasa tukitumia ile na tukaongeza mbolea huyu mwananchi kwa kweli hali yake itabadilika haraka sana, lakini tukiendelea na hii tukutane kwenye palizi nafikiri itatuchukua muda mrefu sana kufika huko tunakotaka kwenda.

Sasa kuna aliyeuliza akasema sasa mbona isipatikane ruzuku kwa ajili ya samadi? Hii ruzuku tunajaribu kutoa kuwashawishi wananchi watumie mbolea kwa wingi zaidi ili tuongeze uzalishaji. Ile samadi ambayo tayari wanayo tuendelee kuwahimiza waichukue kwenye mazizi na kuitumia. Lakini napenda niseme kwamba tutaangalia lile la dawa za pamba, uwezekano wa kutoa ruzuku kwenye dawa za pamba na vile vile kwenye dawa za mazao mengine ili kumpunguzia mwananchi gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kama tulivyoeleza kuwa korosho tumeamua kwamba tutatoa ruzuku ya kusafirisha dawa za korosho. Dawa za korosho zile ambazo zinakubalika na asilimia 50 ya bei ya dawa zile ili kuhakikisha kwamba mwananchi

anatapa kwa bei nzuri na anatumia ili kuongeza uzalishaji wa korosho. Nina hakika kabisa kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja, miwili ijayo, korosho zitakuwa ndio zao linaloongoza kwa kutoa pesa nyingi za kigeni na Mheshimiwa Edger Maokola-Majogo Waziri wangu na rafiki yangu ameniambia amepanda mikorosho 5,500, huyu bwana hapa anangoja kuwa tajiri. *(Makofi)*

Naomba na wengine tufanye hivyo hivyo, kwa hiyo, hili naomba tafadhali sana tulifanyie kazi, lilikuwepo suala la bei ya pamba. Mwaka huu tumejaribu sana kuepuka kutangaza bei, kwa sababu ukishaitangaza wananchi wanachukua ndio bei yenyewe. Lakini masuala ya bei naomba nimwachie mwenzagu Waziri wa Ushirika na Masoko aje azungumze na vile vile azunguzie matayarisho ambayo Serikali inafanya kuhakikisha kwamba haya mambo yanafanyika vizuri.

Ninachoomba Vyama vya Ushirika ambavyo havijawalipa wakulima viharakishe sana kuwalipa halafu tuendelee kushirikiana navyo kutafuta fedha kwa ajili ya kununua pamba katika msimu huu. Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, amelalamika juu ya kutokufika kwa mbolea, nitaomba nifuatilie kuhakikisha kwamba mbolea ya Kigoma inapatikana maana nilipokuja kule niliahidi na kama ulivyoeleza nilikaa kule miaka nane, watoto wangu wengi walizaliwa kule, kwa hiyo, nina deni nitafuatilia hilo.

Lakini la pili ulilozungumzia ni kwamba wananchi waruhusiwe kuuza mazao nje, sasa mimi napenda niseme hivi tatizo letu kubwa sana Watanzania ni kutokuwa wafanyabishara na tunatakiwa kwa kweli tujitahidi sana kufanya biashara kuuza nje badala ya kwenda nje kununua soksi ambazo vijana wetu wanatembea nazo wamening'iza kwenye mkono, tufatute nini tuzalishe humu ndani tutakachouza kitupatie fedha za kigeni kwa ajili kuendeleza Taifa letu. Alikuja mama mmoja anataka kuuza mahindi Kenya akaniuliza je, ruksa? Nikamwambia nenda ukachukue kibali uza, akasema mbona nasikia kuna upungufu, nikamwambia siyo juu yako hiyo ni juu ya Serikali. Wewe kauze mahindi yako Kenya lakini unihakikishie kwamba utapata fedha za kigeni. Sharti peke yake ni hili kwamba umepata soko zuri lenye bei nzuri na litakalokupa fedha za kigeni utakazoleta humu nchini. Lakini kama unataka kwenda kuuza kahawa ili upate *tooth paste,* hapana, maana tunazalisha *tooth paste* humu ndani kama hupendi nunua *Colgate,* nunua aina nyingine tunazalisha *tooth paste* huku ndani au unakwenda kuuza mazao yetu ya biashara ili ulete mitumba, huku mitaani tayari kuna mitumba mingi na viwanda vyetu vingi vya nguo vimefufuka.

Kwa hiyo, sharti moja tu ni kwamba fanya biashara kwa misingi sahihi ya kibishara na nilipokuwa Kigoma niliwaambia watu wa Kigoma badala ya kuvuka na mitumbwi usiku kupeleke masufuria Zaire na Burundi sasa nenda tu kifua mbele mchana ukauze, maana tunataka ufanye biashara upate pesa, utajirike, nchi itajirike, kutokana na hilo. Kwa hiyo, hakuna kizuizi cha kuuza, hata mahindi tuliyonunua *SGR* ambayo yako Rukwa, yako Ruvuma kama akipatikana mtu anataka kununua Zaire sijui Zambia tutamuuzia atupe fedha za kigeni, siyo atupe shilingi alizotorosha kutoka huku. Kwa hiyo, hakuna kizuizi cha kuuza nje hata kahawa tumesema kama unazalisha kahawa ya ubora wa juu na umepata soko zuri ruksa kuuza hiyo kahawa yako katika soko hilo zuri tuletee *foreign exchange. (Makofi)*

Matokeo ya hili kuna shamba moja sasa pale Arusha limetoa kahawa ya ubora wa juu kabisa wanauzia *STABEX,* Marekani wale wanaokuuzia kikombe kimoja cha kahawa kwa *Pound* 2. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kufanya hayo mambo, lakini kwa misingi sahihi ya kufanya biashara siyo ile ya kutoroka na punda usiku ama kwenda kule unabadilisha mazao yetu kwa vitu visivyokuwa na maana hakuna *restriction* ya kufanya hivyo na mimi ningekuwa Kigoma ningeweka *depot* moja kubwa sana ya kufanya biashara na Rwanda, Burundi na Kongo.

Sasa lingine ambalo limezungumzwa sana na Mheshimiwa Prof.esa Jumanne Maghembe, ni la mbegu bora. Tulikuwa na chombo kilikuwa kinaitwa *TANSEED* ambacho kilikuwa kinachukua mbegu kutoka kwa watafiti, mbegu mama inaitwa halafu wanakwenda wanaizalisha ama kupitia kwa mawakala halafu wanaisambaza, kile chombo kilisambaratika, hakipo. Kwa hiyo, tulichofanya kuanzia mwaka 2001 ni kuviambia vituo vyetu vya utafiti vizalishe mbegu mama, mashamba yetu ya Serikali ya-*multiply* zile mbegu halafu baadaye tunazisambaza, kwa hiyo, ndio hizo tani mnazoona kidogo 6,000 na tumekuwa tegemezi sana kutoka nje kwa sababu utaratibu wetu wa kuzalisha mbegu ulivurugika. Kuanzia mwaka huu tunaanzisha *agency* ya mbegu, *Tanzania Seed Agency. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sasa itachukua jukumu la kusimamia mashamba yetu ya mbegu, lakini vile vile itachukua jukumu la kutafuta mawakala watakaozalisha mbegu kwa wingi kwa ajili ya kusambaza huku ndani.

Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwamba mbegu zinazozalishwa huku ndani ni za ubora mkubwa zaidi kuliko mbegu zinazotoka nje kwa sababu zinazingatia mazingira yetu. Kwa hilo tutahakikisha kwamba linafanyika na kwamba tunazalisha mbegu kwa wingi sana, lakini tuna njia nyingine ya kuzalisha mbegu ambayo tunaitumia, wakulima walioteuliwa kwa ajili hiyo kuzalisha mbegu ambayo tunaita ni *quality declared seed,* tofauti na ile *certisfied seed,* ambayo wanazalisha na wanaweza wakauza kwa wakulima wenzao zikasambazwa na zikawawezesha kuzalisha vizuri zaidi.

Kwa hiyo, hili suala la mbegu linafanyiwa kazi na tuna uhakika kwamba litakamilika mwaka huu, miaka inayokuja tutatilia mkazo sana uzalishaji wa mbegu. Lakini pamoja na kutilia mkazo uzalishaji wa mbegu, lazima tulinde zile mbegu tunazozalisha, alikuwa anazungumza mwenzetu hapa akasema tulizalisha mbegu nzuri sana ya maharage ikauzwa Kenya ikaenda kuzalishwa kule sasa inaitwa Nyayo. Kule Malawi wanazalisha mpunga wanaouita Kilombero ambayo ina maana walichukua mbegu kutoka Kilombero. Kwa hiyo, sisi tunazalisha mbegu kwa gharama kubwa sana halafu wanakuja hapa watu wanachukua wanakwenda kupanda, India sasa hivi karibu wanaongoza kwa kuzalisha korosho nina hakika mbegu walichukua kutoka Tanzania, Vietnam hivyo hivyo. Kwa hiyo, zile mbegu tunazozalisha lazima tuzilinde kwa sababu kwa kweli ni haki ya yule aliyezalisha ambaye *in this case* ni Serikali. Kwa hiyo, lazima tulinde sana zile mbegu tunazozalisha

Mheshimiwa Talala Bana Mbise, amezungumzia juu wa wananchi wanaohamia Handeni, mimi nawashukuru sana wananchi wale. Wale wananchi wa Meru walifika mahali wakanijia na tatizo kwamba wanataka yale mashamba ya Serikali wagawane vihamba vidogo vidogo, lakini tukawaambia sasa mkishagawana si yatakuwa yamekwisha? Mtabakia pale pale, jawabu ni kuhama na naona vikundi vingi sana vya wananchi kutoka Meru wamekubali kuhama. Mimi nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara itakupa *support* na kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanakaa katika maeneo yale wanaota mizizi na wanakaa pale pale. Lakini sasa na wao wanihakikishie kwamba wakishahamia pale wanahama kabisa na kuacha yale makaburi ya kwao maana wanaweza kuwa wanahama na huku wanataka warudi kwenye makaburi yao. Tutakupa *support* na nafikiri tuna pesa kiasi kwenye Bajeti mwaka huu kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alitaka nizungumzie kidogo juu ya viini tete yaani *germs.* Hili tumepata kulizungumza siku nyingi sana lakini kuna *aspects* mbili. La kwanza ni kwamba hii ni *technology* ambayo sidhani kama kuna nchi itakayoweza kuikwepa, unaweza ukaendelea ukaipigapiga chenga lakini ni *technology* itakayokuja itakuwa kama *Information Technology.*

Nakumbuka wakati mmoja hapa ilikuwa hata huruhusiwi kuwa na *computer.* Sasa hivi kama huna *computer* kwa kweli uko katika ulimwengu wako wa mbali kabisa, usiostahili. Hii *technology* ya *breeding* kwa kutumia *gene* ambazo zina sifa maalum katika mimea itakuja na itabidi tui-*adopt,* lakini kinachotuzuia sasa hivi tusichukue hatua ni kwamba zile kanuni na taratibu za ku-*adopt techonolgy* hii hazijakamilika. Zitakapokamilika tutaweka utaratibu utakaotuwezesha kupata hii *technology.* Afrika ya Kusini wanayo hii *technology,* Kenya wanayo India, China wanayo na wako katika *very advanced stage.*

Kwa hiyo, na sisi tuko katika *stages* mbalimbli za kujindaa ili tuweze ku-*adopt technology* hii na tuweze kui-*adopt* bila kuchukua madhara ambayo inahisiwa kwenda nayo maana ukiuliza wanakwambia hii *techonogy* ina madhara haya, basi sisi tunataka tupate ile *technology* lakini bila ya yale madhara ambayo yanajulika kwenda na *technology* hiyo. Itatuchukua muda kidogo sio jambo tunaweza kufanya kesho au kesho kutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aggrey Mwanri amezungumzia tena fedha za *STABEX* na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, alizizungumza sana. Nilikutana na mwakilishi wa *EU* na nikamwomba sana kwamba sasa tu-*speed up* matumizi ya hizi fedha na nafikiri ombi langu lilikuwa sahihi kwa sababu bila kuli-*speed up* ukija hapa Bungeni utapata matatizo hasa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ili mwaka huu angalau tuanze kutumia zile fedha. Lakini Mheshimiwa Thomas Ngawaiya nataka nikwambie jambo moja kwamba ile *Regional Roads* inatokana tu na maneno ya Kiingereza, *Regional* kwa maana ya Mkoa, *Road* kwa maana ya barabara, haitokani na *classificationa* ya barabara ya ujenzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wana *classification* ambayo wana *feeder roads,* wana *District roads,* wana *Regional roads,* wana *Trank roads,* sasa hawa wanazungumza tu Kiingereza kwamba ni barabara zilizoko huko Mikoani siyo zilizoko Mijini kama Dar es Salaam na hayo Majiji mengine tuliyoyaanzisha juzi, ndiyo tofauti. Ukiangalia hizi ni barabara ambazo kwa kweli ni *rural* ni barabara nyingi sana, ni za Wilaya ndizo zinazoshughulikiwa, kule kwa Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, watatengeneza barabara kutoka Kasulu mpka Manyovu itakuwa nzuri sana na mara ya mwisho nilipokuwa pale walikuwa wanajenga barabara kutoka Kigoma kwenda mpaka Manyovu pia.

Kwa hiyo, hali inazidi kuwa nzuri ndizo barabara tunazozungumzia sio *Regional Roads* kwa maana ya ile ya *classification* ya ndugu Hamza Mwenegoha, hapana. Ukiangali katika orodha hii utaona ni barabara gani ambazo zipo na nafikiri moja ya barabara hii iko kule Hai bila shaka kwa Mheshimiwa Aggrey Mwanri na nafikiri wananchi wake wanasikia anavyotetea mambo hapa bila shaka watakupa kura zao zote maana kazi unayoifanya ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya hizi fedha za *STABEX* ni ile sehemu inayohusu *Agricultural Sector Development Program* na nafikiri Mheshimiwa Talala Mbise, alitaka kujua kama *pulpery* yake itapatikana, nimewauliza wataalam wangu kabla hujaondoka hapa naomba ufuatilie ili tuhakikishe hiyo *pulpery* yako ni moja kati ya mambo yatakayofanikiwa katika hili.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, alizungumzia vile vile mashamba ya *NAFCO* na ninavyofahamu kuna shamba moja ambalo limeshapimwa kwa ajili ya kuwagawia wananchi pamoja na wale waliokuwa wamavamia Mlima Kilimanjaro. Sina hakika lakini nafikiri ndilo hilo shamba unalolizungumzia la *Journey End*, ambalo lilikuwa limevamiwa kiasi na wananchi watagaiwa sasa kihalali kabisa tutawaomba tu vile vihamba watakavyopata walipie ili kuondoa hili tatizo.

Mheshimiwa Paul Makolo, alizungumza sana juu ya Kweleakwelea, napenda niwahakikishie kwamba kwa kweli katika kupambana na hawa wanyama na wadudu wanaoharibu mazao. Wizara imejizatiti na imeweka utaratibu mzuri sana namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, alikuwa anasimamia utaratibu huu mwenyewe ili kuhakikisha kwamba kabla msimu haujaanza ndege ziko nchini, zinasubiri kuagizwa ziende wapi. Nina uhakika hata sasa ndege zinasubiri kuambiwa ni wapi kuna matatizo ya Kweleakwelea zikapambane nao, ni wapi kuna matatizo ya viwavi jeshi zikapambane na viwavi jeshi, kitu ambacho hatuwezi kupambana nacho kwa ndege ni panya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi tupeleke watu kwa miguu kwenda kupambana nao hasa kule Lindi na maeneo mengine. Lakini Kweleakwelea, viwavi jeshi na nzige tuko imara sana kupambana nao. Wakati nzige walipotokea *West Africa* waliniuliza watu, je hawa nzige watakuja Tanzania? Nikawaambia hapana hawawezi kufika hapa, kwa nini? Nikawaambia kwa kuwa tumejidhatiti kuhakisha kwamba nzige hawawezi kuja Tanzania. Sisi ni wananchama wa Mashirika yote ya nzige, *DLCO-EA* ambayo ina Makao Makuu yake Addis Ababa na hili lingine la *IRLCO-SCA* ambayo makao yake

makuu yamehamishiwa Zambia, tunalipa michango yetu kila mwaka na sasa hivi tunasauti katika Mashirika yale.

Kwa hiyo, kama kukitokea *outbreak* ya nzige yale mashirika yako *stand by* kupambana nao na walipotokea nzige *West Africa* waliweka ndege zao kwenye mipaka tayari kupambana na nzige hao kama wangekuja, kwa hiyo, hakuna nzige ambayo angefika kwetu huku na hawa nzige hawaonekani, sio kwa sababu hawapo, lakini kwa sababu wanadhibitiwa, ukiacha kuwadhibiti tu unapata *outbreak. West Africa* Mashirika yao yalikufa kwa hiyo matokeo ndiyo hayo mliona juzi, kwa upande wa Kweleakwelea naomba msiwe na wasiwasi kama wapo toeni taarifa, tuko imara kupambana nao.

Mheshimiwa Jacob Shibiliti, alizungumzia juu ya kituo chetu cha Utafiti cha Ukiriguru na akataka kujua maendeleo ya upatikanaji wa maji kwa chuo kile, lakini vile vile maendeleo ya upatikanaji wa maji kwa vijiji vinavyopakana na chuo kile ambayo watafaidika na maji yale. Nafurahi kumwambia Mheshimiwa Jacob Shibiliti, kwamba mradi ule wa maji utakamilika katika muda usiozidi miezi miwili kuanzia leo na kwamba yale maji yatakapopatikana yatatatua tatizo la chuo, lakini vile vile yatatatua tatizo la vijiji vile vinavyopakana na chuo. Tuna hofu kidogo tu kwamba watu watakapokuwa wamehamia kwa wingi katika eneo lile si ajabu wakakausha yale mabomba chuo kisipate maji, lakini mradi lile Ziwa liko pale tutakwenda kuchota maji mengi zaidi na kuyapeleka chuoni pale. Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo ni la muda na baaada ya muda si mrefu litakuwa limemalizika. Napenda nigusie suala moja muhimu, kwanza kwa taarifa, lakini pili kwa sababu limegusiwa gusiwa na Waheshimiwa Wabunge, nalo ni suala la mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanza mwaka 2001/2002 matumizi ya mbolea nchi hii yalikuwa madogo sana, chini ya tani 83,000. Tumepanda msimu huu unaokuja tutafikia tani 385,000, nafikiri ni jambo kubwa kidogo, maana tulikuwa tunalenga kufikia tani 300,000 lakini tunafikiri tutavuka na kufikia tani 385,000. Lengo letu ni kufikia tani 600,000, maana tukifikia tani 600,000 tutakuwa sasa tunatumia wastani wa kilo kama 60 kwa hekta. Kwa sasa kwa hiki kiasi kidogo ambacho tumekuwa tukitumia *eighty three* sijui *one hundred and twenty* ni sawa sawa na kilo sita saba za mbolea kwa hekta kwa wastani yaani ingekuwa ni chumvi umeweka kwenye chakula usingesikia hata radha yake, ni kidogo sana.

Kwa hiyo, tunafikiri kwamba kwa utaratibu tunaokwenda nao tutafika tani 600,000 za mbolea kwa mwaka. Utaratibu huo ni upi? Kwa huu mwaka unaokuja kuna ule mkopo wa *ADB* wa *BADEA* wa tani 13,000 ambazo tunatarajia kuzipata wakati wowote, kwa hiyo, zitajazia utaratibu uliopo wa upatikanaji wa mbolea. Lakini kuna makampuni mawili makubwa ambayo yanakuja nchini kuanzisha maghala ya kuuza mbolea na makampuni haya ni *YARA* ambayo *actually* ni Kampuni ya Kiholanzi, lakini imetafuta na kupata fedha kutoka *Norway* kuiwezesha kuja kuanzisha hiyo biashara hapa. Wakija wanakusudia kuwa na maghala ambayo yatahifadhi tani laki moja za mbolea wakati wowote *a revolving amount* ya laki moja. Kwa hiyo, ikipunguka watajazia na lengo lao ni kwamba watauza hiyo mbolea nchini kukidhi mahitaji ya nchi, lakini wakauza vile vile kwa nchi za jirani. Kwa hiyo, ile mbolea ambayo Wamalawi walikuwa wanachukua kutoka Mbeya itakuwa siyo lazima tena wanaweza wakachukua ya kwao

moja kwa moja kutoka Dar es Salaam na Zambia pengine Kongo, Rwanda na Burundi watachukua kutoka hapa. Tunafikiri haya makampuni yatakapokuwa yameji-*establish* yatakuwa yametutalia tatizo kubwa sana na upatikanaji wa mbolea na vile vile tatizo la bei za mbolea. Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, anazungumzia tatizo la mbolea anazitaja kwa wingi Kata za kule kwake, lakini tatizo linakuwa ni *supply,* ile *supply* kutoka nje si kubwa vya kutosha, hivyo tutakuwa tume-*solve* hiyo *problem* na nafikiri ni hatua moja kubwa sana tutakayokuwa tumepiga katika kuendeleza kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo moja ambalo inabidi tukubaliane ni kwamba kama tunataka kilimo chetu kiwe ni kilimo kinachoondoa umaskini, kinacholeta kukua kwa uchumi ni lazima tuongeze tija. Tuongeze kiasi cha mazao ambacho mkulima anapata kwa hekta moja. Kwa sasa hivi kiko chini mno na tunakisia kwamba kwa mazao yaliyo mengi tungeweza kupata zaidi ya mara tano hata mengine mara kumi ya kiasi tunachopata sasa hivi, hili la kwanza.

La pili ni lazima mashamba yetu yawe makubwa zaidi kuliko yalivyo wakati mwingine unakwenda unakuta mtu ana nyumba yake anakwambia ana shamba karibu na nyumba ile ukilitafuta hulioni, unahitaji kitu cha kukupanua macho kidogo ili uweze kuona shamba hilo. Lakini shamba hilo linatakiwa limlishe, lisomeshe watoto, limwezeshe kutibu familia yake na kadhalika. Kama sasa hivi hatukupanua mashamba haya tunayolima kwa kweli katika nchi hii tuna tatizo kubwa sana la kilimo. Kupanua mashamba haya ndio unatumia mkakati wa kutumia zana bora zaidi za kilimo kuliko tunavyotumia sasa hivi tukianza na zinazokokotwa na wanyama kazi kwenda kwenye matrekta ya mikono na matrekta makubwa ili kuhakikisha haya mashamba yanakuwa makubwa zaidi na kwa hiyo, kilimo kinakuwa cha kibiashara na chenye manufaa kwenye familia.

Lazima tuzipeleke familia zetu ndogo hizi zitoke kwenye kilimo cha kujikimu na ambacho kwa kweli hawajikimu hata vya kutosha kwa sababu mavuno wanayopata ni kidogo sana. Ndio kile kilimo ambacho Mheshimiwa Aggrey Mwanri, anakiita shughuli, kitoke kuwa shughuli sasa kiwe ni *economic activity* yenye mapato kwa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini linalofuata ni tuwe na wakulima wa kati. Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliagiza kwamba Serikali ichukue hatua kuhakikisha kwamba wanakuwepo wakulima wa kati, wakulima wenye mashamba makubwa kuliko haya tuliyonayo wanaolima kibiashara. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge mliopo hapa mwoneshe mfano, ile ya kumlalamikia mtu kwamba ana eka 20, achana nayo, jilalamikie kama huna eka 200 na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri itabidi tufanye sensa kama kuna Mbunge ambaye hana eka 200 kwa kweli ana *problem.* Nataka niwatahadharishe baada ya muda sio mrefu ardhi hii itakuwa wamegawana imekwisha. Utakwenda kutafuta eka 200 hutazipata kwa hiyo, kazitafute sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Morogoro Mito ni mingi, Mito 176 isiyokauka kwa hiyo, unaweza kulima mwaka mzima. Watu wanahamia Morogoro sasa hivi kwa wingi kweli kweli wala sijui wanatoka wapi, wafugaji, wakulima na kadhalika. Kwa

hiyo, tujitahidi kuhakikisha kwamba tunakuwa na wakulima wa kati na sisi tuonyeshe mfano. Ile ya kuoneana gere kwamba fulani eti ana eka 200, aeleze amezipataje, umezipataje si umwekwenda kuomba kijijini au umenunua mahali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mie pale Iringa nina eka zangu nyingi tu kwa Mheshimiwa Venance Mwamoto, ndio alikuwa ananiambia hapa kwamba baada ya miaka kumi huenda nikagombea uchaguzi kule. Unapata haya maeneo kwa kuwa sasa yapo, baada ya muda hayatakuwepo halafu ndio tuwe na wakulima wakubwa. Kwa hiyo, malengo yetu lazima yapangike hivyo kupata mahitaji ya kilimo lakini kuhakikisha vile vile kwamba mashamba yanayolimwa ni makubwa na yanalimwa kitaalamu, yanazalisha kwa wingi na tunafanya biashara na nje ili kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nifafanue haya machache lakini nirudie kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo nawahakikishia yote itafanyiwa kazi na vile vile tutakwenda kukaa na kuandika majibu ya hoja zote ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na kuzisambaza kabla hatujatawanyika katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 - Wizara ya Kilimo na Chakula**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ...Sh.2,215,634,700/=

**MHE. HALIMENSHI K. R MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nipate maelezo kuhusiana na mbolea. Msimu wetu wa mvua ni huu mwezi wa sita, saba, mwezi wa nane tutakuwa tumetayarisha mashamba.

Sasa kama mbolea hatuwezi kuipata katika muda unaofahamika sisi tutakuwa tumeshapata tatizo, itakuja mwezi wa kumi na mbili ni wakati wa mavuno na ndio hapo mbolea huwa inaanza kufika. Kwa sababu hizo taratibu alizozieleza kwamba tulikuwa tumekwama Wilayani na sisi Wilayani tulikaa na Mkurugenzi na tukawa tumemteua mtu maalum anaitwa Yotam Kibabi, kama ndio mtu wa kufuatilia hiyo mbolea na alikuja kule Wizarani na hajapata majibu mazuri mbali ya kupoteza nauli yake ya kwenda na kurudi. Sasa, je, katika hilo anaweza kunipa maelezo sahihi kwamba niweze kufuatilia lini?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri la ndugu yangu Mheshimiwa Halimenshi Mayonga. Mimi nimekaa Kigoma na najua mvua zinaanza lini. Zikiwahi sana zinafika katikati ya mwezi

Novemba. Tutahakikisha kwamba mkishatupitishia bajeti hii, tunaanza mipango ya kuhakikisha kwamba mbolea inaelekea Kigoma ili mvua zitakapoanza zikute mbolea imeshafika.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Wakati nimechangia kwa maandishi nilitaka nifahamu kwamba Serikali inahimiza tuwaambie wananchi walime mazao ya chakula yanayostahili ukame hasa mtama lakini kumekuwa na tatizo kubwa kwenye *SGR* sijawahi kuona hata Mkoani Shinyanga pale ambapo tunahimizwa sana kulima mtama Serikali ikinunua mtama. Ni kwa sababu gani za msingi ambazo zinasababisha Serikali kuhimiza watu walime mtama halafu usinunuliwe? Kwa kufanya namna hiyo tunadhoofisha kilimo hiki, mtama ungekuwa unanunuliwa wananchi wangeweza kuhamasika na kuongeza kilimo hiki. Napenda kupata maelezo.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali hili. Mwaka jana tuliweka fedha za kununua mtama lakini hatukupata mtama wa kununua. Tulikuta wafanyabiashara binafsi wanalipa bei za juu sana kwa mtama kuliko ambavyo tungeweza kununua. Mwaka huu tumeweka shilingi milioni 120 kwa ajili ya kununua mtama. Namwomba Mheshimiwa Leonard Derefa, kama ataweza kunipatia mtama huo nitashukuru sana. Tunataka kuanza kuweka mtama kwenye *SGR* kwa ajili ya chakula lakini vile vile kwa ajili ya mbegu kama tutahitaji. Kwa hiyo, iko *covered* katika bajeti yetu ya mwaka huu.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu nilikuwa nimeuliza maswali kama mawili, matatu, ambayo sikumsikia Mheshimiwa Waziri akiyajibu. Yeye amesema tu kwamba unaweza kupata eka 200 lakini nilikuwa nimegusia shamba la Mwakinyumbi lililoko Hale ambalo watu waliomba muda mrefu, nilitaja kwenye hotuba yangu sikusikia jibu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hili suala la *STABEX.* Majibu ya Waziri yanatofautiana na ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya tarehe 13 Juni kwamba barabara za Mikoani *(Regional Roads)* ni za Mkoa zote. Lakini ukisoma majibu ya Mheshimiwa Waziri hapa yanasema kwamba katika mapendekezo yaliyowasilishwa na uongozi wa Mkoa wa Arusha hakuna barabara za Wilaya ya Kiratu zinazoainishwa kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati. Hii inatokana na barabara za Wilaya ya Karatu kutokidhi vigezo au sifa za barabara zinazotakiwa kufanyiwa ukarabati. Chini ya utaratibu wa *STABEX,* sifa hizo ni pamoja na kuwa barabara za Kimkoa *(Regional Roads)* na kuwa na mzunguko wa kuunganisha barabara za Kimkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo swali la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Wilfred Lwakatare bado alijibiwa kwamba Bukoba barabara walizoomba za Kimkoa tayari zilikuwa zina lami kwa hiyo, itabidi waombe tena, *that things is there,* ikabidi waombe tena ili waruhusiwe kwenye barabara za Wilaya. Kwa hiyo, kuna kitu

hapo ambacho leo majibu ya Mheshimiwa Waziri basi ndio tutafanya *final* badala ya kuzingatia haya ambayo tayari yako kwenye *Hansard.* Ningeomba majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema hizi hela za *STABEX* mwaka juzi ziliwekwa kwenye bajeti, mwaka jana zimewekwa kwenye bajeti, mwaka huu zimewekwa kwenye bajeti na zote tunasema bajeti inakua, inakua. Sasa hizi hela mbona zinakuwa *carried forward* kila mara zinawekwa kwenye bajeti tunaambiwa bajeti imeongezeka na ni zile zile za Wajapan za mwaka uliopita wa 2003? Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwa maswali yake mawili na halikukosekana la *STABEX.*

Shamba la Mwakinyumbi liliombwa na viongozi wa Mkoa wa Tanga kwa ajili ya kupanua Mji wao. Kwa hiyo, tukaiomba Serikali iruhusu lile shamba wapewe. Serikali ikaruhusu wakapewa. Sasa Mheshimiwa Joel Bendera, angekuwa hapa angetueleza wanalifanyia nini. Kwa hiyo, sasa wanalifanyia nini shamba lile kwa kweli ni jukumu la wakazi wa Mji wa Hale wajitengee eneo kwa ajili ya kupanua Mji wao, wakishamaliza eneo litakalobaki wagawane kwa ajili ya kuliendeleza kwa shughuli za kilimo. Hili tena haliko mikononi mwa Wizara yangu wala haliko mikononi mwa Serikali liko mikononi mwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *STABEX,* naomba nirudie kusema kwamba hakuna tatizo, orodha ya barabara zitakazoshirikishwa katika *STABEX* zipo na kama Mheshimiwa Mbunge anataka nakala nitampa. Sasa hakuna haja ya kushughulikia na *initial* ya maneno wakati maneno haya yameshaainishwa katika mapendekezo ya barabara zitakazohudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako nimtengenezee nakala nitakapotoka hapa ili naye awe nayo aweze kui-*consult* muda hata muda. Lakini nashukuru kwamba anakubali maelezo niliyotoa basi yawe ndio ufafanuzi wa suala hili na basi tukubali yaishe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ili tusionekana kama tunaanzisha mjadala mwingine, kanuni yetu inatudai tuseme ni kifungu gani tunachozungumzia, maana sasa tunazungumza kama tumebadilisha, tumekaa hapa sasa tunafanya mjadala mwingine tu.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hicho hicho, *Sub-vote 1001,* kifungu kidogo cha 250100, mshahara wa Waziri. Nataka nifahamu mambo mawili.

Kupitia Wizara ya TAMISEMI nilizungumzia labda bahati mbaya tu Mheshimiwa Waziri hakunipata vizuri, lakini kikubwa nilichozungumzia ni suala la Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Nimepitia kwenye hotuba yake baada ya yeye kusoma sikuona jambo lolote linalozungumzia mazao haya mfano nazi, mtama na mengine yanakuwa

hayasemewi sana kwa sababu hayana msemaji. Sasa Waziri angetufahamisha kwamba hii bodi kila siku wanasema itaundwa, itaundwa, ni lini itaundwa ili haya mazao yaweze kupata msemaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika Mfuko wa Pembejeo tulizungumzia kwamba sasa hivi wenzetu wanapata, inazungumzwa tu Mikoa ile ambayo inapata pesa hizi za ruzuku lakini ukiangalia kwetu Mkoa wa Pwani tuna matatizo sana hatujawahi kuona mfuko huu. Kwa mfano, pale Mafia tunashindwa kuupata kwa sababu uwezo wa mtu wa kutaka kwenda kukopa kutoka Mafia kuja Dar es Salaam ni mtihani mzito na mfuko huu kila tunapoufuatilia hatuelewi. Sasa Waziri haoni katika kipengele hiki aangalie uwezekano wa kutenga kiasi kidogo cha fungu katika Mkoa wa Pwani lakini kwa Wilaya ya Mafia aongee na uongozi wa Benki ya *NMB* ambapo tawi lake lipo kule ili wananchi wa Mafia waweze kupata ruzuku hii na kuweza kukopa ili kununulia mbolea pamoja na matrekta ambayo sasa hivi Mafia hatuna trekta hata moja na tumelizungumza? Kama tutapata matrekta hali ya mazao Mafia itakuwa nzuri na kuweza kupunguza tatizo la kuchukua chakula kutoka Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Abdulkarim Shah. Kwanza juu ya Bodi ya Mazao. Bodi hii ya mazao ilishughulikiwa mpaka tukafika kwenye Baraza la Mawaziri lakini kulikuwa na matatizo tuliyotakiwa turekebishe ili tuweze kurudia tena mchakato wa kuanzishwa kwa bodi hii. Lakini suala hili bado linafanyiwa kazi, bado halijapotea, nafikiri tulighafirika kutokulizungumzia kwenye hotuba kama unavyosema, nakubaliana na wewe.

Hili la Mfuko wa Pembejeo, anatumia maneno mawili ambayo kidogo yananichanganya. Anatumia ruzuku na mkopo, hivi ni vitu viwili tofauti. Mfuko wa Pembejeo unatoa mikopo na kama kuna mwananchi ambaye anahitaji mkopo wa kununua trekta naomba aelekezwe tu aje awasiliane na mfuko na kama akipata matatizo, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, tumewasiliana kwa mengi hili moja halitatushinda, tutalishughulikia vile vile kama tulivyoshughulikia hayo mengine na kwa mafanikio kama hayo mengine tulivyoyashughulikia. Ahsante sana.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nina maswali mawili. Kwanza natoa shukrani sana kwa mwaka jana kututengea shilingi milioni 20 kwa ajili ya Bonde la Lundo. Sasa hiyo pesa ilikuwa ni ya kuanzia tu. Nimeangalia kwenye makabrasha humu kwenye mahesabu sijaona pesa zilizotengwa kwa ajili ya bonde hili ili liweze kukamilika kabisa. Kuhusiana na hilo hilo, mabonde mengine haya kama Lundo, Lituhi, Lwekei na Chuulu yataanza lini kufanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni juu ya ruzuku kwa zao la korosho. Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake anaeleza kuwa ruzuku kwa ajili ya pembejeo kwa zao la korosho itatolewa kwa Mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, kidogo Ruvuma, Tunduru lakini sijasikia hali halisi kwa ajili ya mbolea kwa Wilaya ya Mbinga,

Songea na Namtumbo. Tuna korosho nyingi sana kule wakulima wanashindwa kupata pembejeo. Je, Wizara hilo inalifanyia kazi kwa kiwango gani?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, kwa maswali yake mawili. Hili la kwanza nilitaka nilijibu wakati nahitimisha mjadala hapa lakini bahati mbaya lilinitoroka. Moja ya mabonde ya mito ambayo tunayashughulikia katika mwaka unaokuja ni pamoja na mwambao wa Ziwa Nyasa na tunarajia kwamba tutakuwa na miradi kama mitatu kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa.

Sasa Bonde la Lundo imeshaanza kwa hiyo tutaendelea nao tutachagua mingine miwili katika hii aliyotaja ili iweze kufikia mitatu. Namshukuru sana kwa sababu wameshughulikia sana hili Bonde la Lundo, nilianza kulishughulikia nikiwa *RDD* kule hatukwenda mbali sana, natarajia yeye amefanikiwa kuliko nilivyofanikiwa mimi. Kwa hiyo, wapo katika orodha ya miradi itakayotekelezwa na hakuna tatizo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya ruzuku ya korosho, kwa kweli tulichofanya ni kuangalia yale maeneo ambayo ni wazalishaji wakubwa na kwa Mkoa wa Ruvuma tukachukua Tunduru kwamba kitakuwa ndicho kituo cha Mkoa cha kusambaza pembejeo za korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ni mbali kidogo kutoka Mbinga lakini ni suala ambalo tunaweza kuliangalia, tutashughulikiaje haya maeneo ya Songea, *Mbambabay* na Namtumbo ambayo yanazalisha korosho lakini hakuna tatizo la kuwaunganisha katika uzalishaji huu wa korosho.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*
*bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 448,666,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*
*bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh.1,489,394,200/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Ngawaiya ni *Policy and Planning!*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** *Okay.*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kupata ufafanuzi kuhusu *Policy and Planning* kwa sababu niliomba kujua kama mashamba yatakuwa yanapimwa kwa sababu hiyo ni *planning,* katika mazungumzo ya *plan*

mashamba yapimiwe watu. Nilitaka kujua Waziri ana mpango gani kwa hayo mashamba kupimwa ili na sisi tuingie kwenye hayo mashamba?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maelezo ya namna mbili hapa kwanza chini ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alitueleza kwa kirefu kabisa hatua ambazo amechukua na kwamba walishaanza kupima mashamba katika baadhi ya Wilaya na alitoa mfano wa Mbozi kwamba ni moja ya Wilaya ambazo zilishapimiwa na lengo ni kuwapimia wananchi wale ardhi ili kuweza kuwapa hati za kuwawezesha kwenda kukopa.

Lakini kuna upimaji wa mashamba ya namna ya pili ambao huo ndio unahusiana na kilimo kwamba tungetaka wakulima wetu wawe na ardhi ya kutosha na Mkoa wa Singida ulituonyesha njia kwa kupima mashamba. Waliweka *minimum acreage* halafu wakapita wakipima kuangalia ni wananchi gani wenye kiasi kile cha ardhi ambacho wanahitaji ili waweze kuzalisha chakula cha kutosha na waweze kuwa na ziada ili waweze kujipatia fedha kwa shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *unit* ya *Land Use Planning* katika Wizara na inashirikiana na Halmashauri za Wilaya kuhakikisha kwamba kazi hii itafanyika. Katika mwaka 2005/2006 kama umesoma kwenye hotuba tumesema tutafanya kazi hiyo kwenye vijiji karibu 300 kwenye Wilaya nyingi kidogo ili tuanze kupima mashamba kuhakikisha kila mtu ana ardhi ya kutosha halafu Mheshimiwa Gedion Cheyo, atakuja na watu wake kupima kwa utaalamu wa kiardhi ili kumpa *document* ya kumwezesha kumiliki ardhi ile.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Crop Development* ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh.22,591,824,000/=

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa nafasi hii. Katika mchango wangu nilikuwa nimeomba kwamba Wizara itusaidie kuwa na programu ambayo itawezesha zao la viazi mviringo kuwa sasa ni zao la chakula mbadala katika maeneo ya Mwanga yale ya Mlimani. Ningependa kwa kweli nisikie Mheshimiwa Waziri akisema watachukua hatua gani ili kufanya hivyo. Hii ni muhimu kwa sababu eneo letu limekuwa la ukame sana na kwa kweli chakula kimekuwa ni tatizo kwa muda wa miaka minne mfululizo.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwa swali lake. Kwa miaka miwili mfululizo alitaka viazi, tukampelekea. Mwaka ule uliofuata chakula hakikuwa kingi wakala mpaka ile mbegu na mwaka uliofuata tukawapelekea tena wamepanda na ile mbegu wamekula, tutapeleka tena lakini tunaomba wakati huu wasile tena mbegu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni!

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Kaa kwanza, ni zamu yangu.

**MWENYEKITI:** Nadhani Profesa umeridhika?

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Tafadhali Mheshimiwa Dr. Raphel Chegeni.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** *Okay.*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema tumekula mbegu, hapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Mwanga kumekuwa na ukame kwa muda wa miaka minne mfululizo na kwa kweli kumekuwa na matatizo makubwa sana ya chakula na tumeona kwamba zao hili linaweza kutukwamua katika tatizo hili.

Sasa ni kweli tulipewa tani saba za mbegu hiyo lakini kwa Wilaya nzima kwa hiyo, walipewa wakulima 250, isingewezekana kwamba mbegu hiyo kutosheleza Wilaya yote. Mwaka huu tumepewa tani moja na isingewezekana kutosheleza kwa Wilaya nzima. Tunachoomba ni kwamba sasa kwa sababu zao linaonyesha matumaini basi kuwe na programu kabisa ambayo itahakikisha kwamba zao hilo sasa linaweza kulimwa na wananchi kwa wingi wanaokaa mlimani na liwe ndio ufumbuzi wa tatizo la chakula katika Wilaya yetu.

**MWENYEKITI:** Nadhani ndivyo alivyosema Waziri, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hicho hicho cha 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda tu kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala la pamba na hasa ukizingatia kwamba zao hili ili liweze kuendelezwa zaidi lakini linakuwa na matatizo mwaka hadi mwaka na matatizo haya yanabadilika. Mkulima analima sana pamba akitaka kuuza bei inateremka, anakabiliwa na gharama kubwa za pembejeo na kadhalika.

Katika maelezo yangu nilisema kuna michango mingi sana karibu shilingi 60 ambazo mkulima anakatwa licha ya bei ya pamba kuwa inashuka zaidi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa ufafanuzi kwa nini michango hii isiondolewe ili kusudi mkulima aweze kupata unafuu na aweze kujikomboa na kuondokana na umasikini?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kwa swali lake ambalo limenipa nafasi kujibu swali lingine alilouliza Mheshimiwa Dr. William Shija, ambalo sikulijibu kuhusiana na mbegu ambazo hazikuota. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Dr. William Shija, kwamba mbegu tunazogawa sasa zinaota kwa sababu zinakuwa

*mechanically delinted,* hatutumii tena *acid* ile ambayo iliua zile za mwaka ule. Kwa hiyo, hatujapata tena tatizo na hatutarajii kupata tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la michango mingi, hata sisi kwa kweli inatusikitisha sana kwa sababu kuna michango inawekwa kwenye mazao ambayo haibadiliki na bei na ambayo inakiuka maagizo yaliyotolewa kwenye Bunge hili. Sasa naomba tusimamie suala hili maana sasa huu ni uvunjaji wa sheria. Tulikubaliana kwamba mkulima asitozwe zaidi ya asilimia tano ya bei ya mazao sasa kama anatozwa shilingi 21, 7, shilingi nyingine sijui ngapi mwisho unakuta asilimia 50 ya bei yake imekwenda, huyu mkulima anatarajiwa azalishe kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo tumeanza kuchukua hatua kuhakikisha kwamba katika kipindi kifupi iwezekanavyo bodi za mazao zitagharamiwa na Serikali na siyo makato kutoka kwa wakulima. Kwa hiyo, hili tunalifanyia kazi kama kutakuwepo na makato yatakuwa madogo sana mwaka huu, mwaka unaofuata hakuna makato kwa ajili ya uendeshaji wa bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, tushirikiane, kule ambako jambo hili bado linaendelea hebu tuwasiliane, tumshirikishe na Waziri wa TAMISEMI ili tulikemee, haya makato yapungue.

**MHE. HASNAIN MOHAMED MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Ni *Sub-vote 2001, Crop Development,* kifungu kidogo 280700 kinahusu *subsidy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali inatoa ruzuku katika pembejeo ya korosho lakini sisi tuna aina mbili za pembejeo tuna pembejeo ya maji na tuna pembejeo ya unga ambayo inaitwa *Sulphur.* Lakini sasa hatuelewi kwa nini.

Lakini sasa hatuelewi kwa nini Serikali inatoa ruzuku kwenye pembejeo ya maji na ile pembejeo ya *powder* haitoi ruzuku na wakati wakulima wengi sasa huvi wanatumia pembejeo ya *powder.* Sasa nilitaka hayo maelezo.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu mbili za kutoa ruzuku. Sababu ya kwanza ni kumwezesha mkulima atumie teknolojia itakayomwezesha kupata mazao mengi, sababu ya pili, ni kumwezesha mkulima amudu gharama za teknolojia ambayo Serikali ingetaka atumie kwa sababu ya manufaa ya teknoloji hiyo.

Sasa kwa upande wa mbolea, tunatoa ruzuku kwa mbolea zote isipokuwa mbolea zinazoharibu udongo kama *Sulphate of Ammonia,* kwa hiyo ukija na *Sulphate of Ammonia* hatutakupa ruzuku, utanunua kwa bei iliyo katika soko maana hatutaki uitumie lakini tunashindwa kutoa amri ya kusema usitumie.

Kwa upande wa mbolea za korosho hatutoi ruzuku kwa *Sulphur* kwa sababu tunajua *Sulphur* inaharibu udongo, *Sulphur* ukiinyunyizia kwenye majani ni lazima majani hayo yawe na unyevu kwa wakati ule kama hakuna unyevu basi haishiki na kwa hiyo, inateremka yote inarudi kwenye udongo kuharibu udongo itafika siku udongo wetu utakuwa na tindikali kiasi ambacho hatuwe kuutumia. Kwa hiyo, ni teknolojia ambayo ina madhara na Serikali haingetaka kusaidia wananchi watumie teknolojia hiyo yenye madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe hizi dawa zenye maji mengine yanaingia kwenye mimea ni *systemic,* yanaingia kwenye mimea yanatibu magonjwa haya yakiwa ndani ya mimea na kwa hiyo yanakuwa *effective* zaidi kuliko haya. Isitoshe kwa kuwa ni ya maji unaweza ukanyunyizia wakati wowote tu bila kujali kama kuna unyevu au hakuna unyevu.

Kwa hiyo, tunaomba tukubaliane kwamba hii ruzuku tuitumie kwa ajili ya kupunguza bei za dawa zile zenye madhara madogo kwa mazingira na kwa yale ambayo yana madhara makubwa na inajulikana hivyo kwa mazingira tusi-*encourage* kuendelea kuyatumia kwa kuyapa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu tu hiyo.

**MHE. HASNAIN MOHAMED MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bodi ya Korosho iliandaa kikao cha washikadau wa zao la korosho na kwa kuwa hii sensa ilifanyika kwa wakulima wenyewe kwamba ni dawa gani inafaa na ilipofanyika ile sensa ikaonekana dawa ya poda ndiyo inafaa zaidi kuliko ya maji.

Na kwa kuwa, wakulima wengi waliotumia pembejeo ya maji uzalishaji wake unakuwa ni mdogo zaidi ya ile ya *powder,* sasa sijui Mheshimiwa Waziri atatufikiriaje kwamba angalau angetoa mle ruzuku pia lakini tukawa tunatoa elimu wakati huo wa kuweza kupunguza kwa sababu ni kitu ambacho kinapendwa na kinachoweza kuzalisha kwa wingi korosho.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inapeleka teknolojia sahihi kwa wakulima. Suala la kupenda peke yake haliwezi kuwa msingi wa Serikali kupendekeza teknolojia kwa wakulima, sisi tuna vituo vya utafiti na vituo vya utafiti vimetuambia dawa nzuri za kutumika na ambazo zimepitishwa na vituo hivi ndizo hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianza na *Sulphur* kwa sababu wakati ule hakukuwepo na dawa nyingine, kwa hiyo, tukatumia *Sulphur* na tunawashukuru waliotuletea *Sulphur* maana ilitusaidia kwa muda mpaka hiiz dawa nyingine sasa zikaja kwenye soko. Sasa kwenye soko kuna dawa ambayo tunafikiri kwamba ni mazuri zaidi kuliko *sulphur* na hata wanaotangaza sasa hivi wanatangaza wakisema kabisa kuliko wale wakulima wanaoendelea kung'ang'ania yale matumizi ya *Sulphur. Sulphur* ina madhara kwenye udongo, sasa mnataka tuharibu udongo wa Mikoa yote inayolima korosho?

**MBUNGE FULANI:** Hapana.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Kama jibu ni hapana basi tutumie hizi dawa ambazo zina madhara madogo na Serikali yenu iwasaidie kupunguza bei za madawa haya ili muweze kuya-*afford.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kusema ni kupenda tu unaweza kukutana na mtu anapenda kuvuta sigara lakini sigara zinaleta kansa kwa hiyo usimsaidie anunue sigara, msaidie anunue kitu kingine cha kumsaidia. Katika hili la *Sulphur* msingi ni ule ule.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimhakikishie Waziri kwamba wale watu wa Lushoto hawatakula mbegu kama wenzetu wa Mwanga walivyokula mbegu.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Kifungu Programu 20, *Subvote 2001* kifungu kidogo 261100. Swali langu ni kwamba wakati Naibu Waziri anajibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, kuhusu kilimo cha ngano kama zao la chakula katika Wilaya ya Lushoto, alijibu lakini kwa kweli majibu haya hayakutosheleza kwa sababu sisi kama viongozi wa Wilaya tunaamini ngano ndiyo zao linaweza kuwa zao la chakula mbadala badala ya wananchi kulima mahindi. Tatizo linalojitokeza ni kwamba niko Bungeni humu miaka 10, kila mwaka tunajaribu kuiomba Serikali itenge fedha za mbegu na ifanye utafiri mbegu za ngano ambazo Lushoto zinaweza kukua lakini wenzetu wanapelekewa angalau wanakula sisi hatujala tuleteeni basi mwaka huu. Waziri unasema nini kutuletea mbegu ya ngano inayofaa kwa Lushoto.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Nimesimama hapa kueleza kwamba Wizara ilituletea mbegu za viazi mviringo ambazo hazitoshi, hatukula mbegu na ninamwomba Mheshimiwa Henry Shekiffu, afute usemi wake. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge huo siyo kuhusu utaratibu. Kuna kifungu kinachohusu maelezo binafsi kama kuna mtu amekuambia kitu ambacho wewe hukusema na unataka kusikika basi unapata nafasi wakati inasemekana kabisa kwamba sivyo ilivyo.

Mheshimiwa Waziri kuhusu hoja ya Mheshimiwa Henry Shekiffu.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwa swali lake na napenda nifafanue tu kwamba tulipojibu lile swali kwa kweli tulikuwa na matatizo mawili.

Moja, udongo wa Lushoto wanakolima ngano umechuja kiasi ambacho haustawishi ngano kwa teknolojia inayotumika sasa hivi.

Pili, wanalima ngano mwisho wa msimu na wanachelewa kiasi kwamba kunakuwa hakuna unyevunyevu wa kutosha kuwezesha hiyo ngano kuota.

Sasa nikubaliane na Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwamba tutafanya mambo mawili.

Kwanza, tutapeleka watafiti wetu wakatafiti mbinu bora za kilimo cha ngano kinachofanana na mazingira ya Lushoto. *(Makofi)*

Pili, wakati huo tunafanya hivyo tutawapelekea mbegu kiasi maana kwa mfano mwaka ule walivuna tani kama 13 tu kwa hiyo, mbegu wanayohitaji si nyingi sana. Tutawapelekea mbegu kiasi waendelee kulima chini ya ushauri wa Maafisa Ugani walionao wakati utafiti nao unaendelea ili tuweze kupata aina sahihi ya mbegu na utaratibu mzuri wa kuilima mbegu hiyo. Tutashirikiana na Mheshimiwa Shekiffu kuhakikisha linafanikiwa.

**MWENYEKITI:** Naona ameridhika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 -*Directorate of Irr. and Tech. Serv...* ... ... Sh. 10,099,598,500/=

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri, niliomba Serikali itamke na ikubali kuwa ....

**MWENYEKITI:** Kifungu cha kipi?

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Kifungu kidogo 6474 na 6475.

**MWENYEKITI:** Tupo kwenye *Supply Vote,* huko bado hatujafikia huko.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Research Development* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 8,545,686,100/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Samahani nasimama sana kwa sababu mchango wangu karibu maswali kumi sikusikia yanajibiwa. Katika hii *research* nilikuwa nimeuliza kuhusu mashine za kutengeneza miche ya kahawa kwa njia ya majani ambayo sikujibiwa, sasa nilisema kwamba kuna mashine imeombwa ya shilingi milioni 3, watu wa *research* wanahitaji. Vile vile

nilizungumzia kuhusu mashine ya kuchuja sumu ya Pareto ambayo nayo inahitajika katika nchi hii, sasa sikusikia majibu ya Waziri. Ningeomba majibu hayo.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa natoa majumuisho hapa niseme mengi yaliyotolewa ni mapendekezo tuliyoyakubali, sasa kama jambo unalikubali halihitaji tena maneno marefu. Hili la *tissue culture* kwa ajili ya kuzalisha miche ya kahawa kwa wingi ni suala tunalolikubali na tutalifuatilia ili baadhi ya pesa za *STABEX* zitumike kulishughulikia na nawaambia hii mashine imekwishaagizwa kwa hiyo wewe jiandae tu sasa na lile shamba na sijui una ekari ngapi. Hili la pili analouliza ni suala la kimsingi sana. Kilimo cha Pareto katika nchi hii sasa hivi kinapata matatizo kwa sababu hatuna teknoloji ya ku-*process* maua ya pareto mpaka kutoa sumu, tunatengeneza *pyrethrum bulk* ambayo siyo sumu yenyewe inabidi uipeleke mahali ikasafishwe ikishasafishwa ndiyo ipatikane sumu ambayo tunaweza kuitumia.

Hii teknolojia ni *percentage,* huwezi kwenda tu na kuichukua unakununua tu mashine ukaja ukaitumia na kwa kuwa tumekubaliana kwamba *Private Sector* ndiyo yenye jukumu hili tulitegemea *Private Sector* wangechukua jukumu hili na kulitekeleza na kuna wawekezaji ambao walitoka Arusha na wakaja wakatuambia kwamba moja ya mambo wangefanya ni kuweka mashine ya kuchuja sumu ya *pyrethrum.* Kwa bahati mbaya utekelezaji wa suala hili ni kwamba walitaka wauziwe shamba moja kule Makete kwa ajili hii, tulishawakubalia kwa hiyo tunawasubiri tutawafuatilia kuhakikisha kwamba hii teknoloji inapatikana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipishwa na Kamati*
*bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *National food Security* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 895,897,900/=
Kifungu 5002 - *Strategic Grain Reserve* ... ... ... ... ... ... Sh. 8,348,122,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati*
*bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 43 - Wizara ya Kilimo na Chakula

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... Sh. 100,000,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 12,070,000,000/=
Kifungu 2001 - *Crop Development* ... ... ... ... ... ... ... .. Sh. 10,256,152,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati*
*bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Directorate of Irr. and Tech. Serv*. ... ...Sh. 2,959,674,200/=

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati ....

**MWENYEKITI:** Kifungu unakitaja tafadhari.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 2002 kifungu kidogo 6474 na 6475, wakati nikichangia hoja ...

**MWENYEKITI:** Kifungu 6474 *Soil and Water Conservation.* Endelea Mheshimiwa Leonard Shango.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri niliomba kuwa Serikali itamke wazi wazi kuwa suala la kuvuna maji ndilo linalotangulia kabla hujaanza kumwagilia mashamba na nilisema hivyo kwa sababu *scheme* ambazo tuliambiwa sasa zinaendelea kama *scheme* za kumwagilia mashamba nyingi ni za wakati wa msimu tu, mabwawa ambayo yapo sasa ambayo mengine yanafufuliwa mengine yalijengwa zamani ni mabwawa ambayo kwa kweli yalikuwa kwa matumizi ya mifugo, binadamu na mambo mengine. Lakini suala la matumizi ya kilimo cha kumwagilia kinahitaji kujenga mazingira na miundombinu ambayo itawezesha maji yafikishwe mashambani. Sasa mimi nilikuwa nimeomba Mheshimiwa Waziri atamke wazi na pia atueleze kama kuna *Long Term Strategic Planning* katika kuleta mabadiliko kwenye kilimo kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Sina hakika kama nimeelewa swali sawa sawa. Lakini tumeeleza hapa Bungeni na tuligawa vitabu vile vya mpango kabambe wa umwagiliaji maji mashambani na katika mpango ule nafikiri Serikali inakubali kwamba kutekelezwa kwa mpango kama ule wa umwagiliaji maji mashambani ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo na ndiyo maana hata katika bajeti ya mwaka huu Serikali imetenga shilingi bilioni 8 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji maji. Kama Mheshimiwa Leonard Shango angekuwa ameniambia kwamba kuna miradi kule kwake yenye matatizo anataka kuirekebisha ningekubaliana naye haraka sana kwamba atakapoondoka hapa ataondoka na wataalam waende wakaangalie miradi hiyo na kuangalia ni kazi gani inahitajika kufanyika ili kuirekebisha. Lakini suala kwamba miradi ya umwagiliaji, ya uvunaji maji, kutumia maji yaliyopo kwenye mito na maji ambayo yako kwenye maziwa ni ya muhimu wa hali ya juu kabisa na si suala ambalo linalohitaji tena matamshi zaidi ya haya ambayo yameshatolewa na Serikali.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana haki kabisa ya kutokunielewa, lakini ukweli uko pale pale. Hapa tunapoongelea kilimo cha kumwagilia unaanza na kilimo cha kumwagilia hivi kama hakuna maji tunamwagilia wakati gani? Wakati wa masika au wakati wote?

Shughuli ya kilimo siyo shughuli ya miezi kumi na mbili hapa tunapovuna, tunavuna kwa msimu mmoja kwa sababu wakati wa mvua ndiyo tumepata mvua ya kubahatisha ndiyo tunavuna. Lakini tunasema kuwa umaskini wetu utaondokana na utapungua kwa sababu kama wananchi wanaweza wakawa katika shughuli za kilimo kwa miezi kumi na mbili wakati wote. Sasa suala la kusema kuwa umuhimu uko pale pale,

mbona kuna kiangazi, tunasema kuna kiangazi tunaweka majembe uvunguni. Kwa hiyo, mimi siyo suala la kuwa na nilimwomba Waziri pia atoe *road map* au *plan* kwa kila Wilaya maeneo ambayo yanafaa kumwagiliwa na maeneo ambayo maji yanaweza kuvunwa, hiyo ndiyo tulikata kuelewa kuwa Serikali ikubali kwa sababu hakuna njia ya mkato katika suala la kuendeleza kilimo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naona sasa Waziri kaelewa. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Leonard Shango, kwamba tulipokuwa tunaandaa *Irrigation Master Plan,* hatukwenda tu Wilaya kwa Wilaya, tulikwenda Bonde kwa Bonde, Mradi kwa Mradi na kuonyesha nini kinachohitajika kuutekeleza na kwa kuwa anatoka Jimboni kwangu nitamtafuta pale nimpatie nakala ya andiko hilo ili aone ni maeneo gani tumeainisha katika eneo lake, la pili mimi napata tatizo la kumuahidi kwamba tutajenga miradi ya kumwagilia maji kwa mwaka mzima kwa sababu sijui chanzo cha hayo maji wala sijui ni nini kinachohitajika kuyasimamisha ili yaweze kutumika kwa mwaka mzima. Katika mashamba ya Mbarali, Kapunga na kadhalika haya ya Kusini na eneo la Pawaga tunamwagilia maji wakati wa masika kuongeza maji kwenye mashamba ili tuwewe kuvuna mpunga. Kwa hiyo, tunamwagilia *actually* wakati wa masika na imekejeliwa sana hapa lakini huwezi kulima mpunga bila kuupa maji ya kutosha. Ikifika kiangazi hakuna maji ya kutosha kwa hiyo kilimo kinasitishwa mpaka yatakapopatikana maji tena ya kutosha. Sasa mimi nikitoa ahadi hapa kwamba kule Iramba nitakwenda kuwapatia maji ya kulima mwaka mzima ili wasiweke majembe uvunguni mwa kitanda nitakuwa nasema uongo. Kwa hiyo, naomba anilinde, nisiseme uongo mbele yake maana atakuja kunikosoa Jimboni pale pale wala hana taabu ya kunitafuta. Kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba Serikali ina mpango mahususi katika *Irrigation Master Plan* ya kuhakikisha kwamba tunapanua umwagiliaji maji mashambani katika nchi hii ili tupate mchango mkubwa zaidi kutokana na umwagiliaji maji mashambani. Sasa kitakachofanyika kwenye kila mradi itategemea kiasi cha maji kilichopo kwenye eneo lile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leonard Shango, nadhani mnasema lugha moja isipokuwa hamwelewani. Nakupa nafasi kwa mara ya mwisho.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nililokuwa naongelea siyo kuwa kama kuna matatizo ya kumwagilia katika Jimbo langu au katika Wilaya yangu, lakini nilikuwa nimeongelea kuwa tunahitaji tuwe na Programu au *Master Plan* ambayo kila mahali, kila kijiji wanajua kuwa hapa maji ya kidondoka yavunwe hapo hapo na yatumike pale pale ndiyo maana ya kuvuna. Mimi kule Jimboni kwangu nina mradi ambao nimeupeleka mpaka Wizara ya Fedha. Mradi wa kuvuna maji kwenye milima ya Sekenke ambao nusu ya Iramba itakuwa chini ya umwagiliaji kama maji yatavunwa. Mvua zikinyesha maji yale yanakwenda mabondeni, yanakwenda kwenye Ziwa yanageuka kuwa chumvi badala ya kupitia kwenye mashamba na yakamwagiliwa kwenye mashamba kutoka mabwawa ya milimani na yale ambayo yatakuwa ya ziada ndiyo yaende katika Maziwa ambayo yatageuka kuwa chumvi.

Sasa suala la kusema kuwa tuna miradi tayari ile ya kumwagilia, mimi nasema kuwa hatujafanya kazi ya kutosha kwa sababu kama kwenye Mikoa ya ukame inayohitajika sasa hivi ni kuwa na mpango kabambe wa kuvuna maji ya mvua yale ambayo yatamwagika yasitishetishe watu kwenye mabonde, yavunwe kulekule yanakoangukia. Hii ndiyo lugha ninayoongelea mimi, sidhani kama hii lugha nimeiazima mahali pengine lakini inaeleweka vizuri sana. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nadhani ushauri Wizara mmepokea, utakuwa na maelezo Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa maelezo yake ya sasa nakubalina naye lakini ningemshauri pia huo mpango alioupeleka Wizara ya Fedha atupe nakala kwa sababu wataalam wa umwagiliaji wako Wizara ya Kilimo hawako Wizara ya Fedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Research Development* ... ... ... ... ... ... ...Sh. 38,104,173,300/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makisio ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2005/2006 yalipishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Sasa wakati Profesa Jumanne Maghembe alikuwa anazungumza kuhusu kauli zilizotolewa na Waziri na hatimaye Mheshimiwa Henry Shekiffu, kufuatana na kanuni zetu kifungu cha 40 kinakuruhusu wewe kueleza maelezo

baada ya kuahirisha kikao kwa taarifa lakini kwa Spika kwanza. Kwa hiyo, unaweza kujieleza vizuri zaidi kuhusu utaratibu kwa jambo kama lile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa hatuna shughuli nyingine naomba kuahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.56 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 27 Juni, 2005 saa tatu asubuhi)*